# TATHMINI YA SURA ZA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA TOM OLALI *MAFAMBA* (2012) NA *WATU WA GEHENNA* (2012)

**NA**

**Pauline Kamanthe Musyoki**

**C50/CE/28065/2018**

**TASNIFU IMEWASILILISHWA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**NOVEMBA, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijapata kuwasilishwa kwa mahitaji ya kutuzwa shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi:.................................... Tarehe: 28/11/2025.........

**Pauline Kamanthe Musyoki**

**C50/CE/28065/2018**

**MSIMAMIZI**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:.................................... Tarehe: 28/11/2025.........

**DKT:Jesse Murithi**

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Idara ya Kiswahili

KISWAHILI AND AFRICAN LANGUAGES
01 DEC 2025
KENYATTA UNIVERSITY



ii

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mume wangu mpendwa John Mutuse,binti yangu Marian Mutanu na wazazi wangu George Mutua na Rosemary Mutua. Mungu awabariki mnapozidi kuniombea mema katika safari hii ya kitaaluma.

## SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa kuniwezesha kufaulu katika safari hii ya utafiti. Shukrani kwa msimamizi wangu Dkt.Jesse Murithi kwa kunielekeza na kunitia moyo katika kipindi chote cha utafiti. Kongole Daktari kwa kazi yako inayofana na bidii zako dhidi ya mwanafunzi wako. Nawashukuru wahadhiri wote walionifunza na kunielekeza kitaaluma kama vile Prof. Leornard Chacha, Prof. Richard Wafula, Dkt. Miriam Osore, Dkt. Bonface Ngugi, Dkt. Jacktone Onyango na hata Dkt. Edwin Masinde.

Ninashukuru wanafunzi wote tuliosoma pamoja kwa kunielekeza katika mijadala mbalimbali na ushauri wao wakati wote wa utafiti. Natoa shukrani zangu za kipekee kwa rafiki yangu Pauline Wafula kwa kunipa motisha, kunijalia makazi na hata chakula katika kipindi cha utafiti.

Shukrani za dhati ziwaendee walimu wenzangu hasa mwalimu mkuu Bi. Mbithi kwa kufanikisha utafiti huu bila kunihusisha katika zamu za likizo. Aidha, namshukuru mhazili wa shule kwa kunifaa katika masuala ya uchapishaji wa matini. Baraka Everlyne Ndina.

Mwisho naishukuru familia yangu hasa mume wangu John Mutuse kwa kunipa motisha kila mara na kunihimiza nitamatimishe utafiti huu. Shukrani zingine zimwendee baba yangu George Mutua kwa kunipa moyo wa usomi tangu utotoni. Baba, ungependa kuniita Daktari na ndiyo sababu ninaomba Mungu akujalie maisha marefu. Mungu akubariki uishi maisha marefu hadi ushuhudie fanaka za binti yako kuwa Daktari. Mama yangu Rosemary Mutua nakushukuru kwa kunielekeza, kunisaidia kihela na hata kuniombea.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Gehenna:** Jehanamu.

**Mafamba:** Uozo. Nyendo chafu za kichinichini. Ni aina ya ufisadi.

**Sura:** Aina ya kitu fulani.

**Tume:** Kundi la watu lililoteuliwa kwa kazi maalum.

**Ubadhirifu:** Matumizi mabaya ya mali ya umma.

**Ufisadi:** Unyanyasaji katika ofisi za umma, upendeleo, hongo, ulaghai, ukosefu wa uaminifu katika ofisi za umma, kutolipa kodi au kutofuata sheria.

**Umma:** Jumla ya wananchi wote katika nchi.

**Umimi:** Ubinafsi.

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ARA:** | Asset Recovery Agency. |
| **DCI:** | Directorate of Criminal Investigations. |
| **DPP:** | Director of Public Prosecutions. |
| **EACC:** | Ethics and Anti-Corruption Commission. |
| **FOKUS:** | Forum for women and developement. |
| **KANU:** | Kenya African National Union. |
| **KEMSA:** | Kenya Medical Supplies Agency. |
| **NACOSTI:** | National Council for Science and Technology. |
| **NARC:** | The National Rainbow Coalition. |
| **NASCAP:** | National Anti-Corruption Strategy and Action Plan. |
| **NYS:** | The National Youth Service. |
| **ODPP:** | Office of the Director of Public Prosecutions. |
| **TUKI:** | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. |

## YALIYOMO

**UNGAMO** ---------- **ii**
**TABARUKU** ---------- **iii**
**SHUKRANI** ---------- **iv**
**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU** ---------- **v**
**VIFUPISHO** ---------- **vi**
**YALIYOMO** ---------- **vii**
**IKISIRI** ---------- **x**
**ABSTRACT** ---------- **xi**
**SURA YA KWANZA** ---------- **1**
**UTANGULIZI** ---------- **1**
1.1 Usuli wa Mada ---------- 1
1.2 Suala la Utafiti ---------- 2
1.3 Malengo ya Utafiti ---------- 3
1.4 Maswali ya Utafiti ---------- 3
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ---------- 4
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ---------- 5
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ---------- 5
1.8 Misingi ya Nadharia ---------- 11
1.8.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ---------- 11
1.8.1.1 Mihimili ya Uhalisia wa Kijamaa ---------- 12
1.8.1.2 Upungufu wa Nadharia ---------- 13
1.8.2 Nadharia ya Udenguzi ---------- 13
1.8.2.1 Mihimili ya Udenguzi ---------- 14
1.9 Mbinu za Utafiti. ---------- 15
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli ---------- 15
1.9.2 Ukusanyaji Data ---------- 16
1.9.3 Uchanganuzi Wa Data ---------- 16
1.9.4 Uwasilishaji wa Matokeo ---------- 16
1.9.5 Maadili ya Utafiti ---------- 17
1.9.6 Hitimisho ---------- 17

**SURA YA PILI ---------------------------------------------------------------------------18**
**SURA ZA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA MAFAMBA --------------------------18**
**NA WATU WA GEHENNA -----------------------------------------------------------18**
2.1 Utangulizi ------------------------------------------------------------------------ 18
2.2 Muhtasari wa Riwaya ya Mafamba ---------------------------------------------- 18
2.3 Muhtasari wa Riwaya ya Watu wa Gehenna------------------------------------ 21
2.4 Sura za Ufisadi Katika Riwaya ya Mafamba (2012) na Watu wa Gehenna (2012)---------------------------------------------------------------------------- 24
2.4.1 Ubadhirifu----------------------------------------------------------------------25
2.4.2 Unyanyasaji-------------------------------------------------------------------30
2.4.3 Hongo--------------------------------------------------------------------------34
2.4.4 Ulaghai ------------------------------------------------------------------------40
2.4.5 Kuwekeza Akiba Nchi Za Nje ---------------------------------------------45
2.4.6 Ukwepaji Kodi ---------------------------------------------------------------48
2.4.7 Wizi wa kimabavu -----------------------------------------------------------50
2.5 Hitimisho------------------------------------------------------------------------ 53
**SURA YA TATU-------------------------------------------------------------------------55**
**VYANZO VYA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA MAFAMBA NA WATU WA GEHENNA ---------------------------------------------------------------------------------55**
3.1 Utangulizi ------------------------------------------------------------------------ 55
3.2 Vyanzo vya Ufisadi Katika Riwaya za Mafamba na Watu wa Gehenna ---- 55
3.2.1 Umimi Katika Jamii ---------------------------------------------------------56
3.2.2 Tamaa--------------------------------------------------------------------------60
3.2.3 Utovu wa Maadili -----------------------------------------------------------65
3.2.4.Ushindani wa Kupata Madaraka. ------------------------------------------69
3.2.5 Migogoro----------------------------------------------------------------------73
3.2.6 Mapendeleo ------------------------------------------------------------------80
3.2.7 Utovu wa Sheria--------------------------------------------------------------84
3.3 Hitimisho------------------------------------------------------------------------ 91
**SURA YA NNE----------------------------------------------------------------------------93**
**MADHARA YA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA MAFAMBA NA WATU WA GEHENNA. -------------------------------------------------------------------------------93**
4.1 Utangulizi ------------------------------------------------------------------------ 93

4.2 Madhara ya Ufisadi ---------------------------------------------------------------- 93
4.2.1 Umaskini ---------------------------------------------------------------------------93
4.2.2 Mauaji ya Watu -----------------------------------------------------------------97
4.2.3 Kudhoofisha Maendeleo ya Kiuchumi----------------------------------------- 101
4.2.4 Dhuluma Dhidi ya Wanajamii -------------------------------------------------- 106
4.2.5 Kudhoofisha Utawala Bora------------------------------------------------------ 111
4.3 Hitimisho--------------------------------------------------------------------------- 116
**SURA YA TANO ---------------------------------------------------------------------- 118**
**HITIMISHO,MUHTASARI,MATOKEO NA MAPENDEKEZO---------------- 118**
5.1 Utangulizi -------------------------------------------------------------------------- 118
5.2 Muhtasari wa Utafiti--------------------------------------------------------------- 118
5.3 Matokeo ya Utafiti ---------------------------------------------------------------- 120
5.4 Mchango wa Utafiti---------------------------------------------------------------- 123
5.5 Matatizo ya Utafiti ---------------------------------------------------------------- 123
5.6 Mapendekezo ---------------------------------------------------------------------- 123
**MAREJELEO ---------------------------------------------------------------------------- 125**
**VIAMBATISHO ------------------------------------------------------------------------- 130**
Kiambatisho A: Idhini ---------------------------------------------------------------- 130

# IKISIRI

Utafiti huu unafafanua sura tofauti za ufisadi. Mtafiti amefanya hivi kwa kushughulikia riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012). Ufisadi ni suala tata ulimwenguni na hata nchini Kenya. Dhana hii ni pana ila maelezo yake katika fasihi ni finyu kwa kuwa, msisitizo umekuwa kwenye matumizi ya fedha za umma.Kulingana na Tume ya EACC (2016) kipengele cha iv, ufisadi unahusu unyanyasaji katika ofisi za umma, upendeleo, hongo, ulaghai, ukosefu wa uaminifu katika ofisi za umma, kutolipa ushuru au ada yoyote ile na kutofuata sheria zilizohidhinishwa kuteua viongozi katika ofisi za umma. Mtafiti ameangazia masuala hayo kwa kutathmini riwaya teule kwa lengo la kubainisha namna masuala hayo yalivyosawiriwa na kuleta uwezekano wa sura tofauti za ufisadi. Wahakiki kama vile; Muthumbi (2005), Ochenja (2008), Mayieka (2015), Sereti (2016), Mwaniki (2018) na wengineo wameeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya fedha za umma na ndio sababu utafiti huu umeangazia sura tofauti za ufisadi. Riwaya zimeteuliwa kimakusudi na zimeangazia sura tofauti za ufisadi hivyo zilitupa data mwafaka. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na Udenguzi zilitumika. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa inahusishwa na Karl Marx na fikra zake zilitokana na zile za mwanafalsafa Hegel (1971). Waitifaki wake ni Gorky, Baxandall, Terry, James Bisztray na wengine.Kumekuwa na ufisadi katika jamii yoyote ya kitabaka tangu Ujima,Utumwa ,Umwinyi, Ubepari, Ujamaa na Ukumiunisti. Nadharia hii hivyo basi ilitumika kuangazia mfumo wa kiuchumi ambapo kuna tabaka la juu na chini. Tabaka la juu huwa na mifumo ya uzalishaji mali. Njia wanazotumia kumiliki mali ni ufisadi. Tabaka la juu hukiuka maadili ya kiutawala wakijinufaisha na kudhalilisha watu wa tabaka la chini. Kwa kuwa nadharia hii inaelezea uhalisia kama ulivyo, haikuwezesha kutafuta maana zinginezo za ufisadi hivyo nadharia ya Udenguzi ilimfaa mtafiti kuangazia fasiri mbalimbali za ufisadi. Nadharia ya Udenguzi iliasisiwa na Jacques Derrida (1962).Waitifaki wake ni pamoja na Foucault, Roland Barthes, Jean Baudrillard Paul de Man, J.Hillis Miller, Jacques Lacan, Barbara Johnstone na wengineo. Kupitia mihimili ya nadharia hii mtafiti alieleza fasiri mbalimbali za ufisadi. Utafiti huu ulifanywa maktabani kwa kusoma vitabu teule, tasnifu, majarida na makala ya mitandaoni yanayohusiana na mada. Data ya kimsingi ilitolewa kwenye riwaya teule. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo na nadharia zinazoongoza utafiti. Matokeo yamewasilishwa kwa kutumia njia ya maelezo. Utafiti huu utakuwa muhimu kwa wasomi na jamii kwa jumla hasa kwa kuagazia suala tata la ufisadi.

## ABSTRACT

This study adresses various forms of corruption. The novels of *Mafamba* and *Watu Wa Gehenna* has been used for this study. Corruption is a complex and a broad issue but less elaborated in Literature.Emphasis on corruption has been put on management of public funds. EACC (2016) part iv defines corruption as an act of giving bribery, fraud, abuse of public office, embezzlement of public funds, breach of trust, dishonesty in connection with any tax or any levy or dishonesty under any written law relating to the elections of persons to public office. This are some of issues which have beeen highlighted in these novels thus potraying various forms of corruption.Reserchers such as Mayieka (2015), Mwaniki (2018), Sereti (2016), Muthumbi(2005), Ochenja(2008) and among others have explained corruption as misuse of public funds only.There are various forms of corruption despite misuse of public funds. Social realism and Deconstruction theory will guide this research.Social realism theory is associated with ideas of Karl Marx. His ideas were based on thoughts of the philosopher Hegel (1971). Its founders are Gorky, Baxadall, Terry, James, Bisztray and others.Corruption existed from slave society classes to Capitalist society classes.This theory has been used to explain an economic system where there are social classes. A higher social class is associated with power.They posses their wealth in a corrupt way. They are not morally upright. They discriminate the lower class. Since this theory explains realism as it is in society, it will not help in explainig different forms of corruption, Deconsruction theory has thus beeen used to compensate for this shortcomings. Deconstruction theory was associated with Jacques Derrida (1962). Its followers include Foucault, Roland Barthes, Jean Baudrillard,Paul de Man, J. Hillis Millers, Jacques Lacan, Barbara Johnstone and others.Through tenets of this theory various interpretations of corruption are explained.This research has be carried out in library by reading in depth selected books,thesis and journals related to the topic.The data has beeen analysed based on the objectives and theories that guide the study.The findings are presented using explanatory method.This research will be important for academics and society in general by highlighting diffrent forms of corruption despite misuse of public funds.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Suala la ufisadi ni muhimu katika uongozi wa jamii yoyote. Suala hili limeangaziwa na katiba ya Kenya kifungu cha 6 kinachoangazia uongozi na maadili. Ufisadi ni maovu yoyote au ukosefu wa maadili kulingana na Katiba ya Kenya.Tume ya EACC (2016) imeeleza ufisadi  kama unyanyasaji katika ofisi za umma, upendeleo, hongo, ulaghai, ukosefu wa uaminifu katika ofisi za umma au matumizi mabaya ya ofisi hizo, kutolipa ushuru au ada yoyote ile na kutofuata sheria kwa uaminifu. . Jambo hili linatuelekeza kuwa kuna uwezekano wa sura tofauti za ufisadi. Utafiti huu basi umeangazia sura tofauti za ufisadi kama ilivyoelezwa na katiba na tume ya EACC.

Ufisadi umekuwa donda sugu kwa wanajamii hasa katika nchi za ulimwengu wa tatu.Baadhi ya madhara ya ufisadi yamedhihirika katika fasihi ulimwenguni,katika bara la Afrika na hususan katika fasihi ya kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki,ikiwemo Kenya.Madhara ya ufisadi ni kama vile,umaskini,mauaji,dhuluma,uongozi mbaya na kudhoofisha maendeleo ya kiuchumi.

Kimeu (2016), anaeleza ufisadi kama maovu au dhana ya kuharibu chochote kile, matumizi ya madaraka au mamlaka katika ofisi za umma  au za kibinafsi kwa manufaa ya mtu binafsi au kundi la watu. Anaeleza ufisadi zaidi kama usimamizi mbaya wa fedha na mali ya umma, kupotea kwa pesa za umma, kuhama kwa wawekezaji wa kawaida na kwenda kuwekeza nchi zisizo fisadi na uchumi wa nchi kuzorota. Maelezo yake ya ndani ni kuwa ufisadi ni wizi wa pesa tu. Kwa misingi ya EACC(Keshatajwa), ufisadi ni wa aina nyingi si wizi wa pesa tu hivyo utafiti huu  umejaza pengo hilo.

Kulingana na FOKUS (2011), ufisadi ni hali ya kujinufaisha kibinafsi au matumizi mabaya ya madaraka kwa watu waliopewa cheo na wananchi. Ufisadi hupatikana

katika sekta za kibinafsi na katika mashirika ya kiraia. Kulingana nao sura za ufisadi ni kama vile; hongo, ubadhirifu, ulaghai, upokonyaji, upendeleo na undugu. Hata kama wameeleza sura chache za ufisadi, hazijasawiriwa katika riwaya za Kiswahili. Licha ya kufafanua sura hizi za ufisadi, wanasema kuwa watasisitiza kwenye usimamizi wa fedha. Hivyo basi, utafiti huu umefanywa kuziba pengo hilo.

Mayieka (2015) anaeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mali ya chama, shirika, watu wa nchi kupitia hongo kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe. Anaeleza ufisadi bungeni ambapo kuna upokeaji wa hongo, wizi wa mitihani, na viongozi kufuja mali ya umma. Maelezo yake ya ufisadi yanahusu matumizi mabaya ya pesa za umma. Utafiti huu basi umefanywa ili kujaza pengo hilo.

Kwa mujibu wa Sereti (2016) ufisadi unatokana na uongozi usiofaa unaobainika wazi miongoni mwa viongozi. Ingawa mhakiki huyu ameelezea baadhi ya madhara ya ufisadi, anafafanua ufisadi kwa misingi ya wizi wa pesa. Utafiti huu unaeleza ufisadi kwa misingi ya fedha tu. Tumefanya utafiti huu kuziba pengo hilo.

Mwisho, kutokana na maelezo ya Mugwika (2012), Murumba (2013), Mayieka(2015), Sereti (2016), Kimeu (2016) na wahakiki wengineo ufisadi ni matumizi mabaya ya fedha za umma. Ni dhahiri kwamba, ufisadi kama dhana pana haujafanyiwa utafiti katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu umejaza pengo hilo kwa kuelezea sura tofauti za ufisadi kama zilivyobainishwa na Katiba ya Kenya na tume la EACC.

**1.2 Suala la Utafiti**

Utafiti huu umejikita katika utathmini wa sura tofauti za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012) . Hili linatokana na sababu kwamba, wahakiki wengi huelezea ufisadi kama matumizi mabaya ya fedha za umma pekee. Kwa mujibu wa katiba mpya ya Kenya (2010) ufisadi ni ukosefu wa maadili.

Vipengele tofauti katika tume ya EACC (2016) vinaeleza ufisadi kama unyanyasaji katika ofisi za umma, upendeleo, hongo, ulaghai, ukosefu wa uaminifu katika ofisi za umma, kutolipa ushuru au ada yoyote ile, kutozingatia sheria zozote zile zilizoidhinishwa na kukosa maadili katika jamii.Katiba mpya ya Kenya (2010) na tume ya EACC ndizo zimeleta mwamko mpya kuhusu suala la ufisadi ambapo watafiti wengi hawajaeleza ufisadi kama unavyojitokeza bali ueleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mali ya umma tu. Mtafiti ameangazia masuala hayo kwa kutathmini riwaya teule kwa lengo la kubainisha namna masuala hayo yalivyosawiriwa na kuibua sura tofauti za ufisadi katika riwaya teule. Mtafiti ameangazia maudhui, wahusika na lugha ili kuweka suala la ufisadi wazi.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni:

a) Kuelezea sura tofauti za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012).
b) Kufafanua vyanzo vya ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012).
c) Kutathmini madhara ya ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012).

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

a) Kuna sura zipi tofauti za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012)?
b) Je, vyanzo vya ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) ni vipi?

c) Ufisadi umesababisha madhara yepi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehhena* (Olali, 2012)?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mtafiti alichagua mada ili kutimiza malengo matatu. Mtafiti alinuia kufafanua sura mbalimbali za ufisadi, kubainisha vyanzo vya ufisadi na kubainisha madhara yanayosababishwa na sura za ufisadi.

Pili, tafiti za awali zimeorodhesha tu istilahi tofauti za ufisadi bali hakuna utafiti wa kifasihi ambao umefafanua kwa undani sura tofauti za ufisadi kama zinavyojitokeza katika tume ya EACC (2016) na Katiba ya Kenya (2010) . Watafiti mbalimbali kama vile Mayieka (2015), Kimeu (2016) na Mwaniki (2018) wana maelezo tofauti na utafiti wetu. Kulingana nao ufisadi ni unyakuzi wa mali ya umma ili kujinufaisha. Hivyo basi katika tasnifu zao wanasisitiza sura moja tu ya ufisadi ambayo ni matumizi ya pesa kujinufaisha.

Tatu, riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) ni za hivi karibuni na wahakiki wake ni wachache na hakuna mmoja amehakiki sura za ufisadi.Watafiti wa awali hawajahakiki vitabu kwa kutumia Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na ile ya Udenguzi. Murumba (2013) ametafiti mtindo katika *Watu wa Gehhenna* akiongozwa na nadharia ya Uhalisia Ajabu na Umitindo. Mugwika (2012) ametafiti dhana ya uchichimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) akiongozwa na Nadharia ya Urasmi wa Kirusi. Mapendekezo ya Murumba (2013) ni kuwa, watafiti wengine wachunguze maudhui katika riwaya ya *Gehenna* (Olali, 2012) wakiongozwa na nadharia tofauti.

Nne, utafiti huu ulilenga kusaidia watafiti wa Kiswahili watakaoshughulikia mada ya ufisadi.Unalenga pia kuwa faafu katika sekta ya elimu na taasisi za sheria na za kupambana na ufisadi kubainisha sura za ufisadi zaidi ya wizi wa pesa.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafit huu ulifafanua sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Tofauti na tanzu nyinginezo za fasihi, mtafiti aliuteua utanzu wa riwaya kimaksudi. Aidha, mtafiti alishughulikia kigezo cha maudhui, wahusika na lugha katika riwaya teule. Mtafiti aliteua riwaya hizi kwa kuwa ni za hivi karibuni na zilikuwa na data ya kutosha iliyomwezesha kuchunguza mada ya utafiti. Vilevile, riwaya hizo zilikoleza maudhui ya ufisadi.

**1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Katika utafiti wake, Muthumbi (2005) anaelezea ufisadi kama wizi wa fedha. Vilevile, alionyesha namna mfalme Mringwari alivyohonga wazee na wasimamizi wa kesi ili wamwangamize Liyongo. Mtafiti wa awali alieleza ufisadi kwa misingi ya uchumi. Utafiti wa awali ni tofauti na huu kwani, Muthumbi (Keshatajwa) aliangazia suala la pesa pekee ilhali, utafiti huu umeangazia sura tofauti za ufisadi. Utafiti wa awali ulimfaa mtafiti hasa wakati wa kueleza istilahi mbalimbali zinazohusiana na ufisadi.

Ochenja (2008) alitafiti kuhusu ufisadi katika jamii zilizotawaliwa na viongizi wenye ubinafsi. Anaeleza kuwa kampuni ya mawakili haikuwa imefidia wateja wake athari mbalimbali walizopata kutokana na ajali. Pesa hizo walitumia wenyewe na kujaza matumbo yao jambo ambalo lilisababisha malumbano kati ya wateja na mhazili. Huu ni wizi wa fedha. Mtafiti wa awali alitumia nadharia ya Uhalisia sawia na utafiti huu na hivyo basi, mtafiti alipata maelezo zaidi kuhusiana na nadharia tumikizi. Hata hivyo,

utafiti wa Ochenja ni tofauti na huu kwani, hakueleza aina tofauti za ufisadi kijamii na kisiasa.

Kwa mujibu wa FOKUS (2011) ufisadi ni matumizi mabaya ya raslimali za umma au sekta za kibinafsi. Ufisadi unaweza kutokea katika namna mbalimbali; hongo, ubadhirifu, ulaghai, upokonyaji, upendeleo na undugu. Mawazo yao yamekua mwafaka kwa sababu wameainisha baadhi ya sura za ufisadi ingawa wanatilia mkazo sura ya hongo. Kazi hii imefaa kwa sababu imehusisha madhara ya ufisadi. Ingawa wanaibua sura tofauti za ufisadi, wanafasili ufisadi kama shughuli ya mapato. Hata kama wamezingatia sura chache za ufisadi, haya hayajasawiriwa katika fasihi ya Kiswahili.

Mwaniki (2011) anafasili ufisadi kama utumiaji wa njia au mbinu zisizo halali kujipatia mali. Wananchi wapiga kura wanashiriki katika ufisadi kwa kuwa wanalipwa ili kuchagua viongozi. Utafiti wa awali ulimsaidia mtafiti kufafanua istilahi mbalimbali zinazohusiana na ufisadi.Utafiti wetu unatofautiana na wao kwa sababu tumeeleza sura zaidi za ufisadi ambazo hazijafafanuliwa na watafiti hao.Kulingana nao, ufisadi ni matumizi mabaya ya pesa za umma.

Utafiti mwingi haujafanywa kuhusu riwaya za Tom Olali. Kuna watafiti wachache ambao wametafiti vitabu vya Tom Olali. Mugwika (2012), alitafiti kuhusu uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba*. Katika usukaji wa riwaya ya *Mafamba*, matukio ya riwaya nzima yanajitokeza. Wahusika wamefafanuliwa. Mandhari tofauti yamehusishwa ambayo yanajenga maudhui ya ufisadi.. Mtafiti alibaini kuwa, wahusika wa riwaya za kimapokeo kama *Mafamba* wanakaribiana na wanadamu katika ulimwengu halisi. Mugwika (2012) anaifananisha riwaya hii ya kihalisia na historia ya Kenya kipindi cha mwisho cha utawala wa Moi na mateso waliyopata wananchi wakati wa chama kimoja tawala cha KANU. Isitoshe, alilenga

kipindi fulani cha utawala wa  Hayati Kibaki wakati wa chama cha *National Rainbow Coalition* (NARC) ambacho kilipata ushindi mkuu dhidi ya chama cha KANU. Anasema kuwa, maudhui ya ufisadi ambayo yanayojitokeza katika kisa hiki yanabainika sio tu hapa nchini bali mataifa mengine. Suala hili la mafamba ya NUKA NA BORA limesaidia kufafanua sura tofauti za ufisadi, vyanzo na madhara yake. Riwaya ya *Mafamba* inahusiana sana na historia ya nchi ya Kenya. Tarehe mbalimbali katika kalenda ya Kenya zimebainika kibunilizi. Utafiti huu basi utafaa utafiti wetu kwa kuwa kuna istilahi zinazohusiana na ufisadi ingawa hawajaeleza aina za ufisadi.

Mwangi (2013) katika utafiti wake alitumia Nadharia ya Uhalisia na Uhalisia Ajabu kuhakiki riwaya ya *Watu wa Gehenna*. Alijiegemeza zaidi katika nadharia ya Uhalisia Ajabu. Katika maelezo yake  ya mandhari ya riwaya ya *Watu wa Gehhena*; anaeleza mandhari ya kampuni ya THE WORLD CEMENTERS INC ambapo Eks amefanya kazi miaka 40 na akiwa mwaka 20 anapatwa na ugonjwa wa mapafu na kusahau. Badala ya kampuni kumsaidia apate tiba anafurushwa na kutolipwa fidia. Anaeleza pia mandhari ya Chuo kikuu ambapo wanafunzi wanagoma sababu ya utawala wa kidhuluma. Wanabeba bango moja ikiwa imeandikwa THE CORRUPT POLITICIANS CREED. Mwanafunzi aliyebeba bango hili anapigwa risasi na kuumizwa. Hii ni dhuluma inayoendelezwa vyuo vikuu  ambapo wanafunzi ufisidiwa na viongozi wa vyuo vikuu na kunyimwa haki ya kujieleza hadharani. Mandhari haya  kama yalivyoelezewa yamekuwa mwafaka katika utafiti huu kwa kuibua aina tofauti za ufisadi. Tumeongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ambayo itaonyesha hali ya mafukara ambao watakuwa na nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela kinyume naye ambaye ametumia nadharia ya Uhalisia Ajabu.

Murumba (2013), alihakiki mtindo katika watu wa Gehenna akiongozwa na nadharia ya Umitindo na Uhalisiajabu. Katika kazi yake, alishughulikia uhusika na wahusika.

Alidhihirisha usawiri wa wahusika katika kazi ya fasihi. Alichanganua wahusika waliopo katika riwaya teule ya *Watu wa Gehenna*. Aidha, alifafanua sifa za wahusika hao.Kazi hii ilikuwa mwafaka katika utafiti huu kwa sababu wahusika ndio huwasilisha ujumbe wa mwandishi. Baadhi ya wahusika walidhihirisha maudhui ya ufisadi katika matendo yao na mazingira wanamojikuta mfano ni Bi. Saeeda Khan ambaye alishiriki biashara ya kuwasafirisha watu Uingereza kuwapunja. Hikmat ni mhusika mwingine ambaye anaibua suala la ufisadi. Anasema kuwa aliongoza wanafunzi kubeba mabango. Anasawiriwa kama mwanamapinduzi ambaye alikuwa anapinga suala la ufisadi wa viongozi katika chuo kikuu cha Kuhisika. Mhusika huyu anadhihirisha ufisadi, madhara ya ufisadi na namna ya kupambana na ufisadi. Mtafiti pia alitolea mifano ya mandhari halisi kama yalivyojitokeza katika riwaya ambayo yatadhihirisha aina, chanzo na madhara katika maeneo hayo. Mwisho, amependekeza maudhui ya riwaya yahahakikiwe yakiongozwa na nadharia tofauti. Hivyo basi tumejihusisha na maudhui ya ufisadi kwa kutumia nadharia ya Udenguzi na uhalisia wa kijamaa.

Mayieka (2015) aeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mali ya chama, shirika au nchi kupitia rushwa ili kujinufaisha mwenyewe. Anasema kuwa ufisadi unafaa kutangazwa kama janga la taifa nchini Kenya. Amepeana mifano kadha ya ufisadi ambayo itaelekea kuwa sura mbalimbali za ufisadi mfano hongo na ubaguzi. Anaeleza kuwa, taifa la Kenya hupoteza bilioni sitini na tisa kila mwaka kupitia ufisadi. Anaeleza ufisadi katika asasi za elimu kwa misingi ya wizi wa mtihani. Ameelezea madhara ya ufisadi huo kama vile kudunisha viwango vya elimu nchini Tomoko. Tasnifu hii imefaa kwa kuwa inaibua sura tofauti za ufisadi na madhara yake ingawa katika maelezo yake fasili kuu ya ufisadi ni kupitia matumizi mabaya ya pesa.

Kulingana na Sereti (2016), ufisadi ni athari ya uongozi usiofaa kwa vijana na jamii. Kulingana naye, ufisadi ni hali ya kujijali, kujilimbikizia raslimali za taifa ili

kujinufaisha mwenyewe. Anaelezea ufisadi kama dhana ya kutoa pesa. Tasnifu hii imefaa kwa kuwa, imeibua sura tofauti za ufisadi kama zilivyoelezwa na tume ya kupambana na ufisadi. Aidha, mtafiti ameeleza madhara yake ingawa maelezo yake ya ufisadi yanaegemea wizi wa mali ya umma ilhali utafiti wetu umebainisha sura zaidi za ufisadi.

Kimeu (2016) anasema ufisadi umekithiri katika mataifa mengi ya ulimwengu wa tatu. Katika utafiti wake, ameeleza kuwa ufisadi ndio chanzo cha uchumi kuzorota. Kesi nyingi za ufisadi zinahusisha upoteaji wa fedha za umma. Ukombozi dhidi ya ufisadi unaendelezwa na vijana wasomi. Tasnifu hii imefaa kwa msingi wa madhara ya ufisadi na kueleza namna ya kupambana na suala la ufisadi. Utafiti huu unakadiria ufisadi kwa namna ya hela tu. Hivyo basi, utafiti huu umejaza pengo hili kwa kufafanua aina tofauti za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* na *Watu wa Ghenna*. Aidha, mtafiti ameeleza baadhi ya vyanzo vya ufisadi na madhara yake. Utafiti huu ulimfaa mtafiti kwa kuwa, ulidhihirisha vyanzo na madhara ya ufisadi. Tasnifu yake ni tofauti kwa kuwa, ametumia Nadharia ya U-Marx tofauti na utafiti huu ambao umetumia nadharia ya Uhalisia na Udenguzi.

Mwaniki (2018) anaeleza ufisadi kama unyakuzi wa mali ya umma. Katika utafiti wake, anasema kuwa, watu wanatumia njia za ufisadi kujichumia mali bila kuwajali wengine. Anaongeza kuwa, wafisadi wanalemaza uchumi kwa kupora na kujitajirisha hata wale ambao hawajasoma. Maelezo haya yamefaa utafiti huu kwa kuwa, yameibua vyanzo na madhara ya ufisadi. Mtafiti wa awali ameeleza ufisadi kama njia ya kuiba pesa za umma ili kujitajirisha hivyo kubainisha aina moja tu ya ufisadi.

Kwa mujibu wa Ondoro (2021) ufisadi ni wizi au ubadhirifu wa mali ya umma, kudhulumu mtu kimaksudi na kumnyima haki yake, matumizi ya madaraka katika ofisi

za kiserikali au kibinafsi kujifaidi, kutoa au kupokea hongo. Anadhihirisha sura ya hongo katika vituo vya kurekebisha tabia. Wasiokuwa na hatia hulipa gharama kwa kusingiziwa kufanya uhalifu kwa vile wamekosa pesa za hongo. Utafiti huu ulimfaa mtafiti  kueleza vyanzo vya ufisadi. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wa awali kwani huu ulilenga kueleza sura tofauti za ufisadi kando na kutoa pesa ili kupata huduma.

Nyandwaro (2024) anabainisha ufisadi kama unavyojitokeza katika nyimbo.Anainisha sura moja ya ufisadi ya kuwekeza akiba katika nchi za nje .Anabainisha jinsi viongozi wa kanisa uendeleza ufisadi kwa kukubali pesa ambazo ni za ufisadi kama sadaka.Anasema kuwa wananchi wanapaswa kuacha tabia ya kutoa hongo katika ofisi za serikali au za kibinafsi.Utafiti huu ulimfaa mtafiti kwa kubainisha aina za ufisadi na athari ya ufisadi kama vile migomo.Utafiti wake ni tofauti na wetu kwa kuwa hajabainisha aina tofauti za ufisadi.

Kariuki (2025) anaeleza kuwa ufisadi hutokea kupitia matumizi mabaya ya mali ya umma.Anasema kuwa wafanyikazi hulipa kodi ambazo hawaelewi upelekwa wapi.Utafiti huu ulifaa utafiti wetu kwa kuwa amebainisha aina moja ya ufisadi.Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa kuwa amebainisha utafiti kwa njia moja tu.Ufisadi ni zaidi ya matumizi mabaya ya mali ya umma.

Kutokana na tafiti za awali, ni wazi kuwa, wataalam na wahakiki wengi hueleza ufisadi kwa kuegemea misingi ya matumizi ya fedha. Utafiti huu umelenga kueleza ufisadi kama dhana pana inayohusisha vitu vingi kama inavyoelezwa na katiba ya Kenya na tume ya EACC. Tumefanya hivi kwa kuonyesha vile sura za ufisadi zinavyosawiriwa katika riwaya za *Mafamba* (Olali,2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 20112) kama zinavyoelezewa na tume ya EACC(2016)  na Katiba ya Kenya (2010).

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti umeongozwa na nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na Udenguzi. Nadharia ni msingi ambao humuongoza mtafiti au mhakiki wa kazi ya fasihi kuelezea jambo. Wafula na Njogu (2007), wanafafanua nadharia kama jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalum.

### 1.8.1 Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa

Msingi wa nadharia hii ni mawazo ya Karl Marx ambaye fikra zake zilitokana na mwanafalsafa Hegel aliyemtangulia Marx na kuathiri falsafa yake kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya wahakiki wa nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ni Marxim Gorky (1972), Baxandall (1972) Terry na Baxandall (1972) Terry Eagleton (1976), James (1973) na Bisztray (1978)

James (1973) anasema kuwa kama msanii atawakilisha maisha,hatashindwa kuona na kuonyesha kinachoyaelekeza katika ujamaa.Hii itakuwa sanaa ya kijamaa.Uhalisia wa kijamaa umejikita katika Umarx na Ulenin ambao unampa msanii uwezo wa kufahamu kwa undani na kwa udhahiri sheria zinazotawala maendeleo ya kijamii.

Baxandall (1972) anaeleza kuwa fasihi ni kielelezo cha hali halisi za kijamii na haiwezi kutengwa na maswala ya kijamii.Fasihi lazima ichangamshe hadhira yake na izingatie historia ya jamii husika.

Uhalisia wa Kijamaa ni nadharia ya kusanii au kuhakiki kazi ya fasihi ili kuonyesha uhalisia  wa binadamu katika ulimwengu. Husawiri matukio halisi ya kihistoria kwa kutumia wahusika ambao huwa na mshawasha wa kubadilisha hali zao za maisha. Huhusisha utabaka na kwa hivyo, huibua wanyonyaji na wanyonywaji. Wanyonyaji huishia kupigania haki zao na kutaka kuwa washindi dhidi ya unyonywaji. Wataalam

mbalimbali wameelezea maana ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa, hii ni nadharia inayomzingatia binadamu kama chombo muhimu cha kuwa kwa ulimwengu na ndiye huleta maana ya maisha katika ulimwengu. Kwa mujibu wa Wamitila (2007) Uhalisia wa Kijamaa ni nadharia ya kifasihi ambayo inaangazia kazi ya fasihi kwa misingi ya maendeleo ya kihistoria. Nadharia hii huonyesha hatua za kimabadiliko na jinsi jamii hujinasua kutoka unyanyasaji wa kitabaka.

Nadharia hii imekuwa faafu katika uchambuzi wa kazi hii kwani imeeleza mfumo wa uzalishaji mali ambamo kuna tabaka la juu na chini. Tabaka la juu ukiuka maadili ya kitawala na kudhalilisha tabaka la chini.Njia wanazotumia kumiliki mali ni ufisadi katika jamii za kitabaka,ufisadi wa aina mbalimbali huelezwa kisheria ,kidini,kimaadili na kitamaduni.

#### 1.8.1.1 Mihimili ya Uhalisia wa Kijamaa

1. Wahusika wake hudhihirishwa kama wahusika wanaonuia kubadilisha hali yao ya maisha. Ni wahusika ambao huzalisha mali katika jamii yao. Mhimili huu ni muhimu kubainisha njia wanajamii walizoweza kutumia katika kujinasua kutokana janga la ufisadi katika riwaya teule.
2. Wahusika huendeleza utabaka kimaksudi licha ya kuwa wanasawiri matukio ya kihistoria. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuelezea namna wahusika wenye utabaka katika riwaya teule walivyoendeleza ufisadi na hatua inayochukuliwa na tabaka iliyonyanyaswa dhidi ya ufisadi.
3. Huangazia hali za mafukara wa ulimwengu wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela. Mhimili huu ulikuwa mwafaka kuonyesha mabadiliko ambayo huibuliwa na umoja wa mafukara ili kujikomboa dhidi ya dhuluma

inayoendelezwa na mabwenyenye. Ulionyesha pia athari ya ufisadi kwa jamii kama ilivyojitokeza katika riwaya teule.

4. Huonyesha matumaini juu ya maisha ya binadamu na kueleza jinsi mtu atakua mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote. Mhimili huu ulikuwa muhimu kudhihirisha majukumu waliyotekeleza waliopinga ufisadi ili kuwahamasisha wananchi kupata ushindi dhidi ya ufisadi katika riwaya zilizoteuliwa.

#### 1.8.1.2 Upungufu wa Nadharia

Kulingana na Wafula na Njogu (2007), nadharia hii imekolea itikadi sana hivi kwamba masuala ya kisanaa yanaweza kupuuzwa. Lugha inayotumika huwa kavu, ikakosa matumizi ya kunga za kifasihi kama vile sadfa, taharuki na tamathali za usemi ambavyo ndivyo vigeu muhimu vya kudhihirisha malengo ya kazi yoyote ya fasihi. Hivyo basi nadharia ya Udenguzi ilitumika kuibua sura tofauti za ufisadi kwa kutumia vigeu vya lugha, wahusika na maudhui. Nadharia hii imeibua fasiri tofauti za ufisadi kimazingira na muktadha tofauti na tafiti za hapo awali kuhusu dhana ya ufisadi.

### 1.8.2 Nadharia ya Udenguzi

Udenguzi ni nadharia ya kihakiki iliyoanzishwa na mwanafalsafa wa Ufaransa Jacques Derrida (1976) ilichanganuliwa na Foocault, Roland Barthes, Jean Baudrillard, Paul De Man, Hillis Miller, Jacques Lacan na Barbara Johnston.Derrida (1976) anasema kuwa, tafsiri ya matini kwa wahakiki haiwezi kuelezwa kwa namna moja, kila mtu ataieleza kwa namna yake. Maana zinaweza kuendana au kupingana.Kwa mujibu wa Derrida,kila kielekezi huelekezwa na kingine na kuendelea kuelekezana bila kikomo.Hii inamaanisha kuwa hakuna vielekezi wala vielekezwa asilia katika matini kwani ni vielekezi vya vielekezwa,jambo ambalo linaleta dhana kuwa hakuna matini asilia wala ile ya mwisho.Kwa ujumla kulingana naye,maneno na matini huwa na

maana nyingi na hakuna maana asilia ya neno ambayo inaweza kurejelewa na hakuna kitu asili na kizima hivyo hakuna matini asilia ambayo haina utata.

Kulingana na Miller (1979) maana ni telezi. Anaeleza kuwa tafsiri ya kazi yoyote ya fasihi uathiri maana. Matini tafsiriwa huibua kumbukumbu ya maandishi awali. Matini tafsiriwa ni kimelea cha matini asili. Barthes (1977) anaongeza kuwa, mwandishi anapoandika kazi yake jukumu lake huishia pale. Tahakiki ya kazi yake haiathiriki na mtunzi. Mhakiki asome kazi ya fasihi na kutoa fasili yake kwa kufuata mantiki na muktadha wa jamii yake. Aidha, Njogu na Chimera (1999) wameshughulikia vile lugha na maana zinavyoingililiana na kufanya kazi pamoja. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa kutokana na Udenguzi hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Hii ndio inayofanya wahakiki kutoa fasili tofauti tofauti za jambo moja. Udenguzi unaweza kuboresha matini au kuumba upya kwa lengo la kukidhi upya mahitaji ya jamii. Ni wazi kuwa, kila matini huibua maana tofauti kutegemea wasomaji tofauti na hivyo maana ya matini yoyote ile ya kazi ya fasihi ni telezi na tata.

#### 1.8.2.1 Mihimili ya Udenguzi

1. Hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Wahakiki hutoa fasiri tofauti za jambo moja ambazo huweza kuwa tofauti kwa kuwa wana ushahidi unaotosha. Mhimili huu ulikuwa mwafaka katika utafiti huu kwa kuwa ulisaidia kufafanua aina tofauti za ufisadi ambazo wahakiki wengi hawajakadiria.Wahakiki wengi uelezea ufisadi kama hali ya kutoa pesa ili kupata huduma fulani. Utafiti huu umevuka zaidi ya hayo na kuonyesha aina tofauti za ufisadi ambazo kulingana nao si ufisadi.
2. Kazi ya fasihi huwa na maana ya ndani inayopatikana ikifasiriwa kwa umakini. Mhimili huu ulikuwa mwafaka kwa kuwa ulionyesha fasiri tofauti za ufisadi katika riwaya teule.

3. Kazi ya mhakiki ni kuibua na kujumuisha kile kilichonyamaziwa, kilichopuuzwa na kuachwa nje na wahakiki wengine na hata kisichotiliwa uzito na mwandishi. Utafiti huu uliangazia aina tofauti za ufisadi ambazo wahakiki wengine hawajafafanua. Wahakiki wengi hueleza ufisadi kama kigezo cha hongo na kupuuza masuala mengine muhimu ambayo kulingana na utafiti huu ni ufisadi. Hivyo, mhimili huu umefaa utafiti huu.

### 1.9 Mbinu za Utafiti.

Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza kuwa mbinu za utafiti ni muhimu kwa kuwa hudhihirisha sampuli, uwasilishaji na ukusanyaji wa data. Wanaeleza kuwa, ni vizuri mtafiti kufafanua kwanini mbinu ya utafiti ni mwafaka. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Mtafiti alisoma riwaya ya *Mafamba* (2012) na *Watu wa Gehenna* (2012), tasnifu, majarida, makala mbalimbali na hata kusakura mtandao hasa masuala yaliyohusiana na mada ya utafiti. Mtafiti alisoma makala yanayohusisha nadharia teule na kuchanganua sura za ufisadi kwa kutumia mihimili ya nadharia hizo. Utafiti ulikuwa wa maktabani kwa sababu, maandishi mbalimbali yapatikana humo. Tasnifu zilisomwa ili kuelewa nadharia, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data husika.

#### 1.9.1 Uteuzi wa Sampuli

Mugenda na Mugenda (2003) wanabainisha sampuli kama vijisehemu vidogo vya idadi jumla ya utafiti. Kimalu na Marimba (2014) wanasema kuwa sampuli ni kundi ndogo ya watu binafsi, matukio au vitu ambavyo hupatikana katika idadi halisi ya utafiti inayofikika. Mchakato wa usampulishaji kimaksudi uliongoza suala nzima la utafiti. Mugenda (2003) anaelezea sampuli kimaksudi kama aina ya sampuli ambayo humruhusu mtafiti kuchagua wanajumuiya wenye sifa bia na ambao watampa data inayokusudiwa kulingana na malengo yake. Katika utafiti huu mtafiti alitumia sampuli

ya kimaksudi kwa kuteua riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehhena* (Olali, 2012). Baadaye, mtafiti alidondoa sentensi, vishazi na vifungu ambavyo vinaonyesha sura tofauti za ufisadi. Ziliteuliwa kwa sababu ziliaminika kukoleza maudhui ya ufisadi. Mada yenyewe "Mafamba" umaanisha ufisadi.

### 1.9.2 Ukusanyaji Data

Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza ukusanyaji data kama utaratibu wa kukusanya ujumbe muhimu na kuelezea ujumbe huo kwa kina. Kwa kuwa huu ni utafiti wa maktabani pekee, mtafiti alitumia mbinu ya upekuzi. Data ilitokana na riwaya teule. Mtafiti aliteua sentensi, vishazi, wahusika na maudhui ili kuweza kuibua sura tofauti za ufisadi. Data hiyo ilinukuliwa kwenye vitabu au daftari maalum ambayo baadaye ilichanganuliwa.

### 1.9.3 Uchanganuzi Wa Data

Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza uchanganuzi wa data kama kuchunguza ujumbe ambao hupatikana kuhusu suala la utafiti na ufanyaji wa maamuzi. Uchanganuzi wa data humsaidia mtafiti kufafanua data yake ili kusaidia watakaopitia utafiti huo kuelewa. Data hiyo ilichanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Uhalisia wa Kijamii na Udenguzi. Uchanganuzi pia uliongozwa na malengo ya utafiti kuonyesha sura tofauti za ufisadi kama zilivyojitokeza katika riwaya teule, vyanzo na madhara ya ufisadi.

### 1.9.4 Uwasilishaji wa Matokeo

Baada ya kukusanya na kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa njia ya maelezo kufafanua sura za ufisadi vyanzo na madhara yake katika riwaya teule. Mifano mwafaka kutoka riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehhena* (Olali,

2012) ilitolewa kwa unukuzi wa moja kwa moja. Uwasilishaji wa kimaelezo ulifanywa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule.

### 1.9.5 Maadili ya Utafiti

Kabla ya kuanza utafiti, mtafiti aliomba idhini kutoka chuo Kikuu cha Kenyatta na shirika la NACOSTI. Kwa mujibu wa Kimalu na Marimba(2014), wizi wa maandishi ni kosa ambalo huhusisha matumizi ya kazi ya kiakademia ya mtu mwingine bila kumrejelea. Utafiti huu ulizingatia maadili kwa kuhakikisha kuwa kazi ambayo imeandikwa na kuchapishwa ni kazi asili ya mtafiti bali si wizi wa maarifa.

### 1.9.6 Hitimisho

Katika sura hii, msingi wa jumla wa utafiti umewekwa kwa kuelezea vipengele muhimu. Vipengele hivi ni pamoja na; usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka. Aidha, sura hii imeeleza kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi na mihimili ya nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa na ile ya Udenguzi. Vilevile, mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti zimeelezwa. Sura ifuatayo imeshughulikia sura za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012).

# SURA YA PILI
# SURA ZA UFISADI KATIKA RIWAYA *ZA MAFAMBA NA WATU WA GEHENNA*

## 2.1 Utangulizi

Sura ya kwanza imeshughulikia vipengele vya kimsingi katika utafiti. Sura hii inahusu muhtasari wa riwaya ya *Watu wa Gehenna* na *Mafamba* na sura mbalimbali za ufisadi. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya Udenguzi ya Jacques Derrida (1962). Baadhi ya sura zilizoangaziwa kwa kutumia mihimili ya nadharia ya Udenguzi ni kama vile; Ubadhirifu, Matumizi mabaya ya Mali ya Umma, Hongo, Ulaghai na kadhalika.

## 2.2 Muhtasari wa Riwaya ya Mafamba

Mwandishi ameanza hadithi kwa kutuchorea picha ya mtaa wa Bikerani-Msiige ambapo umaskini umekita mizizi. Kuna matabaka mawili ambayo yahahuzunisha Arijojo mkaazi wa Bikerani-Msiige. Wakazi wa Bikireni-Msiige wamejaa uchungu kwa sababu ya uongozi mbaya. Wamenyimwa haki zao.

Kiongozi wa Bikireni-Msiige ni Maotad.Wakazi wamembandika jina *Aende*.Jina hili lionatokana na kuwa alikuwa ameamrishwa aende lakini alikuwa amekatalia mamlakani.Alikuwa kiongozi wa sayari ya NUKA katika nchi ya Kiafra.Alipendwa na watu aliotimiza haja zao na kuchukiwa na watu kama Arijojo ambao haja zao hazikutimizwa.

Katika hatua ya kwanza ya kuleta mabadiliko, Arijojo anaungwa mkono na Amrao mwanasayari wa DiPieLi, ambaye alitaka Maotad aende ili aongoze. LiMioe ni mwanasayari wa PiDi ambaye pia anataka kuleta sayari zote pamoja ili azitawale. Maotad anakatalia mamlakani na yeyote aliyejaribu kumbandua anadhulumiwa.

Maotad alipendwa na wale waliomchukia Amrao.Nia ya Amrao kutaka kukitia kitumbua mchanga inamsababishia kutiwa kizuizini na Maotad kwa miaka 30.

Malengo ya Amrao yalibainika katika wimbo aliotunga akiwa jela wa kutimiza haki za wakazi wa sayari zote.Maotad pia alikuwa na wimbo uliosifu mafamba.Sayari zote zilikuwa na muundo wa lugha iliyohusisha vokali na Konsonanti. Katika sayari ya NUKA, herufi M, A, F na B zilipendwa sababu hazikusababisha ufukara. Ziliwakilisha mafamba.Maradhi ya NUKA yalienea katika sayari nyinginezo kama kanisani, baina ya madaktari na wagonjwa,hospitali vilevile makasisi na waumini.

Maotad anataka kuokoa sayari ya NUKA dhidi ya mahasidi wa sayari nyinginezo kama LiMioe, Boyi, Fadhila, Mastanji na Sinya.Anataka kujihusisha na Amrao ili awakabili.Anaamrisha wapelekwe Mkanyageni.Hili lilikuwa jumba la orofa 77 lililotengenezwa kwa waliojaribu kumpinga Maotad.Waliopitia chumba hiki ni Mastanji,Charo na wengine.Maotad alitaka kuungana na Amrao ili kukabiliana na Fadhila,Boyi na LiMioe.Maotad alikuwa na tamaa ya uongozi alitaka kutawala milele.

Maotad anaita Kamu, Avad, Kanga na U na kuwaibia siri kuwa alitaka kuchagua kiongozi wa NUKA baada ya kujiuzulu.Anawadanganya vikaragosi hawa kisha baadaye kumchagua U. Amrao anajiondoa kwa kundi la U na kujiunga na kundi la BORA la Boyi, LiMioe na Fadhili. Wanasayari wengi waliunga mkono kundi hili. Boyi na wenzake wanakubaliana kuwa wakishinda wangemchagua LiMioe awe kinara, Boyi naibu wake, Amrao msaidizi mkuu wa kinara, Fadhila naibu wa msaidizi mkuu wa kinara naye Kamu awe naibu wa pili wa Kinara.

Katiba ya sheria za NUKA haikukubaliana na mamlaka ya Amrao, Fadhila, na Kamu. LiMioe anawahakikishia kuidhinisha katika mda wa miezi mitatu na siku kumi. Kundi

la BORA lina lengo la kuzika mafamba na kuweka hadharani watu walionyakua makaburi, mashamba, mito, maziwa, nyumba, barabara na misitu.

Tarehe 12/27/2200, ilikuwa siku muhimu ya kuamua nani kati ya U na LiMioe. LiMioe alichaguliwa kisha Boyi kuwa msaidizi wake. LiMioe anahakikisha kupambana na suala la mafamba. Baadaye Boyi anafariki na Damisi kuteuliwa mahali pake.Baada ya LiMioe kuchaguliwa, hakufaulu kutimiza maagano ya kundi la BORA kwa kuwapa wanasayari wote katibu kwa  siku alizoahidi. Wakazi wa Bikerani-Msiige walikuwa wametoa mapendekezo yao kuhusiana na azimio walilotaka.Mambo haya yalihusu dini, ardhi, uhuru wa wanawake, mamlaka ya kinara wa BORA na wasaidizi wake, uenezaji wa utawala wa mashinani na kadhalika. Mawazo ya wakazi wa Bikerani-Msiige yalikusanywa pamoja kama stakabadhi iliyojulikana kama *Azimio la Nyumba*. Kundi lililopinga azimio hili  halikutosheka na maamuzi yaliyoafikiwa hivyo kusababisha uhasama kati ya makundi haya mawili. Walidai mamlaka ya kinara wa BORA yalikuwa mengi na yapewe msaidizi mkuu. Kundi lililounga lilitaka kuanzisha utawala wa kiimla na kuchukua madaraka kwa njia isiyo halali.

Umoja wa sayari ya BORA ulivunjika.Kamati zilivunjwa. Marekebisho yalifanyiwa *Azimio la Nyumba* na kuibua stakabadhi mpya ya *Siri ya Mbuyu* iliyompa kinara wa BORA mamlaka mapya.Maasi yalianza na viongozi wakaanza kumpinga LiMioe. Wakati wa kupigia debe azimio la *Siri ya Mbuyu*, kundi la LiMioe lilitumia ishara ya *Mumbi*. Lilishindwa na kundi la Amrao lililokuwa na ishara ya *Njiwa*. Hali hii ilisababisha uhasama baina ya viongozi wa BORA huku baadhi ya viongozi wakipigwa kalamu. Uharibifu wa mali na ufisadi ulizidi. Kutoelewana kati ya viongozi wa BORA kuliendelea hadi mwisho wa kipindi cha  uongozi cha LiMioe ambapo wananchi walipiga kura. Upigaji kura huu ulikuwa na athari nzuri na mbaya. Vigogo wengi walitolewa mamlakani.Kulizuka vurugu katika baadhi ya sehemu nchini kwa sababu

haikujulikana kama aliyeshinda alikuwa Amrao au LiMioe.Vita vilizuka vilivyosababisha maafa, kuchomwa kwa nyumba, uharibifu wa mali, damu kumwagika na kueneza uhasama kati ya makabila.

Vita viliisha pindi tu Amrao na LiMioe walipokubali kugawana madaraka.Mkataba ulitiwa sahii na kushuhudiwa na sayari zote. Sayari ya BORA ilizaliwa upya na viongozi wapya na ukombozi ukafanyika Haponasaremwige. Baada ya mapatanisho, wanasayari waliomba mungu ili maafikiano yadumu milele.

### 2.3 Muhtasari wa Riwaya ya Watu wa Gehenna

Riwaya ya *Watu wa Gehenna* imetungwa katika mandhari ya njozi. Riwaya hii ina wahusika wawili tu na hadithi inafanyika katika akili ya mhusika mmoja Eks. Wahusika wanatoka katika ulimwengu halisi hadi ulimwengu wa kijonzi na kurejea tena katika ulimwengu wa uhalisia.Riwaya hii inasimulia chimbuko la ufisadi na kupanga msasa masuala ibuka kama vile biashara ya kuuza nyeti za zeruzeru,kuteswa kwa wafanyikazi wa nyumbani katika mataifa ya ng'ambo na vilevile athari za teknohama katika mitandao ya kijamii hususan *facebook* na *twitter*.Watu ambao wanatenda maovu kama haya ndio urejelewa kama *Watu wa Gehenna* na mwandishi.

Mwanzoni mwa riwaya mwandishi anaanza kwa kutujengea mandhari ya Gehenna sehemu ambayo watenda maovu wanavuviwa moto mwisho wa hadithi. Gehenna lina matanuu manne yenye moto na volkano nne juu ya milima minne inayogawanywa na bonde katikati. Huko kuna mziki unaoitwa *Watajuta*. Mandhari haya ni ya kijonzi yamo akilini mwa Eks

Eks ni mhusika anayejumlisha wahusika wengi. Eks alimwoa Takosani binti Abdalla na hawakubarikiwa na mtoto kwa sababu ya kiafya. Alikuwa na kasoro katika shahawa zake.Hatimaye mkewe alifariki. Baada ya kifo cha mkewe alioa mke wa pili Lakeisha

ambaye alikuwa na watoto wawili Baingana na Siyawezi.Waliishi kwa miaka kumi na mitatu.Lakeisha baadaye anapapia maendeleo ya kitarakilishi na kumpata mme tajiri katika mtandao wa *facebook* na kuomba talaka kwa Eks. Watoto wanabaki  naye Eks. Baadaye anaoa mke mwingine  ambaye anakataa kuishi na watoto wa Lakeisha na kuwaacha peke yao.

Eks alifanya kazi katika kampuni moja ya kutengeneza saruji iliyoitwa *The World Cementers Inc*.Aliathirika kiafya akawa anasahau mambo na kuugua ugonjwa wa mapafu na matatizo ya figo. Eks anazungumza na nafsi yake na Mzee Afisul kuhusu binadamu ni nani? Na suala la *Superior Intelligence* ambapo anatumia kielelezo cha *Sataranji* kumfafanulia. Kulingana na Eks binadamu ni familia ya *Hominadae* na wa spishi ya *Homosapiens*. Mwandishi anasema kuwa Eks alikufa na kufufuka baada ya miaka saba katika nafsi yake.

Takosani ni totoshoo maridadi ambaye anafanya usuhuba na Sikujua katika *Reficul Meadows.* Aliwahi kuolewa na mwarabu na ndoa ikavunjika baada ya siku saba.Anasema wanaume wamemtenda na anataka abaki peke bila kuolewa.Anapatana na Sikujua ambaye anamuekea masharti ya kuombea kaburi la mama yake kwa kulipigia magoti na kuwekeza sarafu juu yake. Takosani anaonekana kuwa na sifa za kishetani. Sikujua anampenda Takosani na masharti yake na kufanya usuhuba naye. Wanapokuwa pamoja,anaondoka kupitia ukutani na kumpeleka Sikujua kimiujiza hadi Mapangoni. Takosani anashirikiana na Sikujua baadaye na kumuua kasisi Yunasi, mkewe Saida na watoto wawili. Sikujua alikamatwa na kuwekwa rumande. Takosani naye anakiri kuwa ana mpango ulioratibiwa na shetani wa kuwaadaa vijana wote duniani ili waasi. Kupitia mbinu rejeshi, Sikujua aliwahi kuwa mbunge na kushiriki maovu kama vile ukabila, mauaji, kukata maelfu ya miti na kunyakua ardhi.Anatumiwa kuonyesha uongozi mbaya.

Wafanyikazi wa nyumbani wanatumikishwa ughaibuni kutoka nchi yao ya Kenya. Bi. Saeeda Khan na Bi.Rabecca Balira ni baadhi ya wakaazi wa Gehenna wanaohukumiwa kwa kuwatesa wafanyikazi wa nyumbani. Bi. Saeeda Khan pia anashiriki biashara ya kuuza zeruzeru na viwiliwili vyao.Bi Rabecca na Bi. Saeeda wanaangamia kwenye ajali ya barabara Nahegen.Wauwaji wengine ni wakili Angamizamtuwewe II anayepanga njama za mauaji ya kimbari nchini NdaRwa mnamo 2064 .

Mwalimu Baya anafanya usuhuba na Mishi akilini mwake.Mishi anabadilika na kuwa jini.Baya anajikuta kwenye ghorofa akikumbatiana na mpenzi wake.Anazinduka usingizini na kujipata juu ya mbuyu huku nguo zake zikining'inia kwenye matawi. Anasaidiwa na wasamaria kwa kumpa shuka kujisitiri. Wanamweleza kuwa alipatana na shetani wa mahaba kutoka Gehenna. Anaelekezwa kwenda Mabokweni kwa Sheikh Hamza Hamdeni ampe dawa ya kumuagua.Anapewa masharti yanayomchukua miaka saba kutimiza mwishowe laana inavunjwa baada ya kupata mtu wa kutupia laana hiyo.

Katika Chuo Kikuu cha Kuhisika,wanafunzi wanagoma wakiungwa mkono na wazazi na baadhi ya walimu kwa sababu ya utawala wa kidhuluma. Wanabeba mabango yaliyoandikwa THE CORRUPT POLITICIANS CREED.Mwanafunzi aliyebeba ni Hikmat.Anapigwa risasi na kuumizwa.Maandamano yanafanywa katika nchi nyingi za Kiafra.Hikmat baada ya chuo kikuu anazindua kampeni za ubunge ndotoni.Hikmat ni mhusika mwenye nafsi ya Ikmat, Kmat na Mat wanaoendeleza kipindi cha *The night of the living dead* katika runinga.Wanazungumzia changamoto katika nchi za Kiafra.Anatetea wanyonge na kukashifu wabunge kwa kudai nyongeza badala ya mishahara yao kukatwa ili operesheni za kaunti ziboreshwe.

Baadayadhiki ni mhusika wa ajabu anayeishi makaburini.Ni rafiki ya Takosani.Ni msimulizi anayesimulia kisa cha mwanasiasa Faki aliyepewa wadhifa wa waziri wa

afya na kutawala vibaya.Anabainisha maovu kama ufisadi,ukabila na jinsi maendeleo yalivyorudi nyuma Kiafra.Anaeleza jinsi Faki alivyopata arafa kuhusu kasisi Taabu.Kasisi alishtakiwa kwa kumnajisi msichana wa miaka 13 kwenye madhabahu ya kanisa.Taabu alikuwa amefumaniwa tena na kibiriti ngoma mwingine katika mahaba kwenye madhabahu. Matendo haya yanatokea kwenye fikra ili kuonyesha uovu ulivyokithiri kanisani.

Mchezo wa *The Matrix of the corruption* in Kiafra unaofanyika akilini mwa Bi. saeeda Khan unaibua maovu ya Kiafra.Anahukumiwa kuwa mmoja wa watu wa Gehenna. Mtunzi anatumia mhusika wa kiajabu Nyamaume anayehukumia wahalifu wote wa Kiafra.Munkari anahutubia wafisadi wote na kuamuru Nyamaume kuvuvia moto.Wahusika wote wabaya ndio wanaorejelewa kama watu wa Gehenna.Munkari anasema kuwa hasa wanaoshiriki ufisadi ndio aliohutubia na Nyamaume alipaswa kuvuvia moto.

## 2.4 Sura za Ufisadi Katika Riwaya ya *Mafamba* (2012) na *Watu wa Gehenna* (2012)

Wamitila (2003) anaeleza sura kama sehemu ndani ya kazi ya kifasihi ambapo mawazo au matukio tofauti uwakilishwa. Kamusi kuu ya Kiswahili (2015) inaeleza mafamba kama mambo yasiyokuwa ya uadilifu, hila au udanganyifu. Mayieka (2015) anaeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mali au raslimali za chama, shirika, watu au nchi kupitia rushwa. Muthui (2019) anaeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mamlaka kwa kujifaidi na kufaidi wengine. Kulingana na Ndung'u (2022) ufisadi ni maovu yanayotendwa na mtu ili kujifaidi na kufaidi wengine. Kwa mujibu wa Lomatoro (2014) ufisadi ni matumizi mabaya ya pesa za umma. Wahakiki hawa na wengineo wanaeleza ufisadi kwa namna tofauti na wengi wameelezea ufisadi kama matumizi

mabaya ya pesa za umma. Katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) kuna aina tofauti za ufisadi ambazo zimeelezewa katika sura hii.

Baadhi ya sura za ufisadi ambazo zinadhihirika katika riwaya hizi ni; Ubadhirifu, unyanyasaji, hongo, ulaghai, kuwekeza nchi za nje, ukwepaji kodi na wizi wa kimabavu.

### 2.4.1 Ubadhirifu

Ubadhirifu ni matumizi mabaya ya mali ya umma. Wamitila (2003) anaeleza ubadhirifu kama tabia ya kutenda mambo kwa kusudi la kuharibu mali ya mtu mwingine au kudharau mali ya wengine.Anasema kuwa ubadhirifu ni kikwazo cha maendeleo.Watafiti wengi uelezea ufisadi kama matumizi mabaya ya pesa za umma tu.Utafiti wetu umevuka mpaka na kuelezea raslimali tofauti ambazo hutumiwa vibaya zaidi ya pesa kama vile ofisi za viongozi na mamlaka.Hili linaafikiana na mhimili wa nadharia ya udenguzi kuwa maana ni telezi.

Viongozi wengi hutumia vyeo vyao kuwanyanyasa wengine. Baadhi ya viongozi huwa hawafanikishi malengo waliyohaidi kwa wananchi. Baadhi yao huwakandamiza wananchi hasa wa tabaka la chini na wale ambao hawafuati amri na kanuni zao ziwe nzuri au mbaya. Lomatoro (2014), anasema kuwa, watu wengi barani waliona kuwa wakiwa uongozini ilikuwa nafasi yao kujilimbikizia mali ya umma. Njenga (2021) anaelezea suala hili la matumizi mabaya ya mali ya umma kama wizi. Anasema kuwa, wenye mamlaka huiba mali ya umma na kuendeleza maslahi yao ya kisiasa.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) kiongozi wa sayari ya NUKA anatumia mamlaka vibaya kwa kuwaua wote ambao walikuwa wanampinga. Baadhi ya watu ambao wanauliwa na Maotad ni Rojoo. Fununu zinaenea kote kuwa Rojoo alikufa kwa sababu alikua amekula chapati moja na vipande saba vya nyama. Baadaye, kulitokea

vifo vingine ambavyo Maotad alihusika (Uk. 7). Suala hili la kuuliwa na kupotea kwa watu limekuwa sugu sana katika nchi nyingi. Mara nyingi, ukienda kinyume na mipango ya viongozi au kufichua siri zao uuliwa na kupotea usijulikane ulioko.

Vilevile, viongozi wengi ulimwenguni huwa na tabia ya kukatalia mamlakani pindi muda wao wa uongozi unapoisha. Wenye hutumia vifua vyao hutawala kinyume na matakwa ya wananchi. Hili ni suala ambalo husababisha wizi wa kura ndiposa waweze kubaki pale pale. Jambo hili husababisha uongozi mbaya. Mwandishi amedhihirisha kuwa Maotad anakatalia mamlakani. Anasema;

> Siendi! Siendi! Siendi! Miaka 720 tu! (Uk. 10)

Kulingana naye miaka 720 ni kidogo na anataka kuendelea kutawala watu wa sayari ya NUKA. Watu wa sayari hiyo wamechoka na wanaungana ili kumtoa Maotad kwenye kiti ikiwemo baadhi ya viongozi wa sayari zingine kama Fadhila. Hata hivyo, mwandishi anadhihirisha kuwa si Maotad tu ila viongozi wengi wa sayari ya NUKA walikatalia mamlakani. Mwandishi anasema;

> Kila mara waliposema wanatoka, hakika walitoka lakini hawakwenda (Uk. 14).

Maotad alitumia ofisi yake vibaya. Mwandishi anajenga mandhari ya ofisi yake kama ya kuogofya. Katika ofisi yake kuna kiti maalum ambacho kilikuwa na swichi nyuma yake. Kilikua kiti maalum cha mgeni aliyemtembelea Maotad. Baadhi ya wageni waliokaribishwa walijua kunguni wake. Kiti hiki kilitumiwa na Maotad kudhulumu wote ambao walimpinga. Mwandishi anaeleza mandhari tofauti ya Mkanyageni orofa takribani 77 ambapo pia watu walifanyiwa ukatili na viongozi. Mwandishi anasema;

> Vyumba hivyo vya juu vilitumika na utawala wa Maotad kwa shughuli zao rasmi. (Uk. 47).

Vilevile, mwandishi anasema kuwa Mkanyagenii ndio sehemu haswa ambayo ilikuwa imeteuliwa kufanyia ukatili wote walikwenda kinyume naye.

> ……Ungelifanya hivyo ungelikwenda moja kwa moja Mkanyageni. Kule Mkanyageni ukiwa salama ulikuwa ni mchezo wa karata tatu. (Uk130)

Maotad anatumia mamlaka yake vibaya kwa kuteua kiongozi aliyemtaka. Anamteua U ambaye hakuwa na sifa za uongozi ila kwa sababu alitaka kujinufaisha kutoka kwake (Uk94). Maotad hakutilia mkazo viongozi ambao walikuwa na sifa nzuri za uongozi kama Amrao. Baada ya kiongozi wa sayari ya BORA LiMioe kuwa mgonjwa, Amrao alichukua jukumu hilo. Kundi la Amrao liligawanyika katika makundi tofauti. Kila kundi lilipaswa kueneza ile sumu ya sayari ya NUKA. Kundi la U walitumia vyombo vya habari kueneza uvumi na kufuja hela nyingi. Katika hotuba ya LiMioe, anasema kuwa magari yote rasmi yalikua yao na kuwaambia wasaidizi wake wayatumie watakavyo. Mwandishi anasema kuwa viongozi wa mtaa wa Bikerani-Msiige yalijaa maovu na baadhi ya maovu hayo ni ubadhirifu. Anasema kuwa, viongozi walibinafsisha raslimali za nchi kwa kupitia mlango wa nyuma. Ugavi wa mali ulikuwa kwa msingi wa kigogo gani unayemfahamu kule juu (Uk. 243). Hii inasababisha utabaka hivyo wananchi kuungana na kutaka kutafuta viongozi watakaofaa sayari hiyo.

LiMioe pia anatumia mamlaka vibaya baada ya kuteuliwa kuwa kiongozi wa sayari ya BORA. Anawaachisha kazi wasaidizi wake wa upande wa upinzani bila kosa lolote. Mwandishi anadhihirisha ubadhirifu kupitia mhusika Avad na Bwana Paka. Wote walihusika katika kampuni ya mfuko wa vito. Ilisemekana kuwa Bwana Paka alipenda kunywa maziwa-maziwa ambayo si yake. Maziwa ya wakazi wa Bikerani-Msiige. Maziwa ni neno ambalo mwandishi amelitumia kijazanda kumaanisha Raslimali.

Alikuwa anauza raslimali za wakazi wa Bikerani- Msiige. Jambo hili lilisababababisha uzorotefu wa uchumi huku maskini wakiathirika zaidi.

Ubinafsishaji wa raslimali za nchi pia ulifanywa kwa mlango wa nyuma. Umiliki wa mali ulitegemea kiongozi gani uliyemfahamu. Viongozi ndio waliofaidika. Waliota vitambi ila wananchi walizidi kuwa hohehahe. Walishiriki maovu yote ya dunia. Waliokuwa na majina walikuwa mwafulani. Uchumi ulizorota kwa sababu ya ubinafsishaji huu wa viongozi. Wananchi walizidi kulalamika na kuungana ili kubadilisha uongozi mbaya wa Maotad. Hata baada ya kumtoa Maotad na kupata uongozi mpya wa BORA, mambo hayakubadilika. Viongozi walizidi kutumia mamlaka yao vibaya kwa kudhulumu wengine. Maskini walikuwa hawana neno. Waliishi maisha ya kuogopa kwa kuwa ungethubutu ungeuliwa namna ambavyo haingeweza kujulikana.

Katika riwaya ya *Watu Wa Gehenna (*Olali, *2012)* mwandishi amedhihirisha sura ya ubadhirifu kwa namna tofauti. Muziki wa Gehenna ulioitwa *walijuta* unadhihirisha ubadhirifu. Mwandishi katika wimbo huo anasema kuwa watajuta kujilimbikizia ekari nyingi za mashamba. Anasema pia, Watajuta kujiongezea mishahara yao kiholela (Uk. 9). Muthui (2019) anaeleza maudhui ya ubadhirifu kama maudhui tofauti na ufisadi. Anaeleza ubadhirifu kama matumizi ya mali kwa fujo. Anaongeza kuwa, serikali hukopa pesa nyingi na kuziwekeza katika miradi isiyofaa wananchi. Anasema pesa hukopeshwa kutoka mataifa ya kigeni na kutumiwa katika miradi isiyofaa. Anasema kuwa, viongozi ujilimbikizia mali huku wananchi wakididimia katika umaskini. Jambo hili husababisha kuzaliwa kwa matabaka. Kulingana na mhimili wa nadharia ya udeguzi kuwa kazi ya mhakiki ni kuibua kile kilichonyamaziwa na kupuuzwa na wahakiki wengine, ubadhirifu si maudhui tofauti na ufisadi ila ubadhirifu ni aina ya

ufisadi kulingana na utafiti wetu.Vile vile,ufisadi si matumizi mabaya ya pesa za umma tu kama inavyodaiwa na watafiti wengine

Katika ndoto ya Hikmat, inadhihirika kuwa serikali ilikuwa inakarabati ikulu kila mwaka. Wanasiasa pia walikuwa na safari ya mara kwa mara nje ya nchi. Hikmat anasema kuwa, safari hizo za wabunge sharti zipunguzwe ili kuleta ufanisi katika nchi. Wamitila (2003) anasema ubadhirifu unaweza kusababisha kupoteza mali na kushuka kwa maendeleo ya kiuchumi. Fikra hii ya Hikmat inadhihirisha suala la ubadhirifu kwa wabunge. Tazama mfano ufuatao:

> Ili kuleta ufanisi, tutaunda serikali ndogo isiyozidi wizara kumi na tatu, tutapunguza matumizi yasiyo lazima safari za mara kwa mara nje ya nchi na kuondoa kabisa ukarabati wa kila mwaka wa Ikulu (Uk. 157).

Hikmat pia anadai kuwa wawakilishi wa watu wa Kiafra wakishaachaguliwa husimama bungeni na kuomba nyongeza yao posho zao za mishahara au ofisi. Anasema kuwa, wawakilishi hawa wanapaswa kusema mishahara yao ikatwe ili kugharamia operesheni kwenye kaunti. Suala hili linadhihirisha matumizi mabaya ya mali ya umma kupitia wabunge (Uk. 176). Anadhihirisha pia matumizi mabaya ya mali ya umma kupitia madaktari. Anasema kuwa, raslimali za Kiafra hazijatumiwa vizuri. Dawa za kutosha kila pembe ya Kiafra hazijakuweko kiini na maana kuwa, madaktari huuza madawa ya hospitali za umma katika hospitali zao za kibinafsi. Hikmat anasema kuwa dawa hizo zinageuka kuwa sumu na mauti kwa binadamu kwa sababu ya kuuza dawa bandia (Uk. 177).

Katika Fikra za Hikmat, ukosefu wa vifaa muhimu Kiafra ulitokana na uongozi mbaya. Anasema kuwa, watu hasa kiongozi wa pili walinajisi raslimali za nchi. Vilevile, anakiri kuwa walinyakua mashamba na kutumia hazina ya uzeeni kujinufaisha. Hela

zilizokusanywa kama ushuru hazikufikia malengo yake ambapo suala la ubadhirifu linaibuka (Uk. 265).

Katika hukumu ya Munkari Gehenna, viongozi wengi hupata pesa za kujiandaa katika mikakati ya siasa kwa njia ya ubadhirifu. Ili kupata fedha zaidi viongozi wanaonuia kupata uongozi ushirikiana na baadhi ya viongozi walioko madarakani. Wanapata pesa hizo kwa kuiba kutoka taasisi za serikali au miradi mikubwa ya umma. Munkari anasema;

> Wanaweza kupata fedha wanazozihitaji kwa ajili ya kupata ushindi kwa kuiba au kukwapua kutoka taasisi za serikali kama vile mabenki au miradi mikubwa ya umma yenye fedha nyingi (Uk. 231).

Mwandishi anasema kuwa viongozi hao wakati mwingine hupewa zabuni bandia za serikali ambazo watalipwa pesa nyingi. Isitoshe, chama tawala pia huweza kutengewa fedha nyingi katika bajeti ya serikali kwa kuingiza miradi hewa au mikataba mibovu (Uk. 231). Huu ni ubadhirifu. Munkari anasema kuwa, suala hili la ukwapuaji wa mali ya umma ni suala chafu. Wanaoumizwa ni wananchi maskini mijini na vijijini. Anasema kuwa, suluhisho la hili ni kupaza sauti (Whistle blowers) kuhusu suala lolote la ufisadi kwa namna hili na kudai uwajibikaji.

### 2.4.2 Unyanyasaji

Mugwika (2012) akichunguza uchimuzi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) anasema kuwa Mzee Twajua aliwakilisha walionyanyaswa kupitia mawazo yake. Anawafungua macho wakazi wa Bikerani-Msiige dhidi ya unyanyasaji wa viongozi kupitia sera ya Nopro na kuwaambia washikilie silaha ya ukombozi. Anawaambia kuwa kwenda kwa debe ndiko kulikuwa Alpha na Omega ya mateso yao. Akieleza suala hili la unyanyasaji hajaliweka wazi kama aina ya ufisadi.Ufisadi uelezwa kama matumizi

mabaya ya mali ya umma ingawa kuna aina tofauti za ufisadi.Unyanyasaji pia si kwa sababu ya pesa tu bali kuna unyanyasaji tofauti zaidi ya pesa kama vile kubakwa,kutumikishwa kazini na kadhalika. Mhimili wa nadharia ya udeguzi kuwa hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi basi umetufaa kuelezea unyanyasaji huu kama aina ya ufisadi.

Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba (*Olali,*2012)* amedhihirisha unyanyasaji kama suala ambalo limejitokeza sana kutoka kwa viongozi. Mwandishi anasema kuwa viongozi walijaa unyanyasaji (Uk. 243). Kiongozi wa sayari ya NUKA Bwana Maotad anadhihirisha unyanyasaji kwa njia nyingi. Shanata anapomtembelea Maotad ofisini mwake anashindwa kuketi chini. Maotad ndiye angetoa ruhusa ya kuketi chini. Inasemekana kuwa yeyote ambaye alikwenda sebuleni mwake na kufululiza moja kwa moja hadi kitini na kukaa kabla ya kuambiwa kufanyaa hivyo, alisubiri siku chache tu na matokeo yake kufa na kufufuka. Mle ofisini mlikuwa na kiti kilichokuwa na swichi nyuma yake. Ambrose (2014) watu wa kawaida katika jamii unyanyaswa kila siku kwa sababu huogopa kwenda kinyume na fikra za watawala na kutopewa nafasi ya kujitetea na kupata hukumu za vifungo magerezani. Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* anasema kuwa kiti hiki kilikua cha kudhulumu wale wote walioenda kinyume na ushauri wa Maotad.

Tazama mfano ufuatao,

> Hiki ndicho kiti kilikuwa kiti rasmi cha mgeni aliyemtembelea Maotad. Baadhi ya wageni waliomtembelea. Waliokaribishwa wakikalie walijua kunguni wake (Uk. 17).

Maotad pia anamtia jela bwana Amrao kwa miaka 30 kwa kuwa alikataa kujihusisha na mafamba na kutaka kumwaga mchanga ndani ya kitumbua (Uk. 25). Babake Amrao Bwana Mastaji pia alitiwa Jela. Huyu ndiye aliyekuwa wa kwanza kufungiwa chumba

kilichofanana na Mkanyageni. Alitiwa ndani kwa sababu alikuwa anapinga uongozi dhalimu. Mwandishi anasema kuwa yeye ndiye alikuwa simba wa kukabiliana na viongozi kama Maotad (Uk. 49). Mastaji pia alifanyiwa ukatili na Maotad. Anaamrisha Mastaji alishwe siafu, pilipili, shubiri, sumu ya *anaconda* kama kifungua kinywa. Mlo wa mchana analishwa maji ya batari, vipande vya chupa, gundi ya viatu, samadi na moshi wa tairi ya magari. Chumba alimokuwa hamkua na kitanda bali ndoo aliyotumia kutema mate. Mwandishi anasema kuwa alilalia maji. Licha ya kuwa marafiki, Mastaji na Maotad hawakuonana kwa muda mrefu. Alifanyiwa ukatili huu baada ya kukosana na Maotad na kumzaba kofi na kuhamia sayari ya ASIFO. Wengine walionyanyaswa ni wale waliotoa hotuba zao katika hoteli ya Come-K. Punde walipomaliza walipelekwa Mkanyageni walikochomoka si maiti si mamati. Mfano ni Jokaga, Tojombo, kuka, Pange, Freku, Onachi, Bika na wengineo. Wangekabiliana na hatari nyingi kama mbwa koko, gesi ya sumu na risasi.

Avad pia ananyanyaswa na Maotad. Avad alikuwa amekataa kabisa kujiunga na Maotad. Anamlazimisha kutoka kundi la BORA na kujiunga na NUKA. Avad anaalikwa na Maotad katika ofisi yake ambapo anafanyiwa ukatili. Anapigwa teke na kumpiga kidevu kwa goti lake hadi damu likamchiririka (Uk. 154-155).

Wanasiasa pia wanafanyiana unyanyasaji. Siku moja walikuja wafuasi wa U na kumkata vipandevipande mzee mmoja na wanawe wanne kwa sababu ya kutoungana na upande wao na badala yake, kumfuata Amrao. Ndimi za wafuasi wa Amrao zilikatwa na sehemu zao za siri kuchopolewa na kukandwa na wafuasi wa U. Viongozi wengine wanaofanyia watu ukatili ni U. Mwandishi anasema;

> Wafuasi wake walimkatakata vipande mzee mmoja na wanawe wanne kwa sababu ya kutoungana na upande wao. Ndimi za wafuasi zilikatwa na sehemu zao za siri kuchopolewa na kukaangwa na wafuasi wa U (Uk. 99).

Unyanyasaji unajitokeza pale ambapo watu hawakuruhusiwa kujitetea katika sayari yoyote ile ila Sayari ya DUNIA. Sheria katika sayari zote zilikiukwa. Watawala walidhulumu watawaliwa kisha watawaliwa kufungwa. Viongozi wanashiriki katika biashara haramu ya mbao. Ekari nyingi za misitu zilinyakuliwa na kasri za ajabu kujengwa humo. Wenye kuuza mbao walizipeleka hela hizo katika sayari mbalimbali bila kulipa ushuru. Aliyekamatwa baada ya kupatikana na hatia ya kukata miti ni Sikujua. Mwandishi anasema kuwa Sikujua hakuelewa sababu ya kufungwa na wengine alioshiriki nao katika shughuli hiyo hawakukamatwa (Uk. 173).

Mwandishi wa riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) amekoleza unyanyasaji katika kazi yake. Katika mandhari ya Gehenna, waliokuwa na uwezo wa kuona ndani ya giza totoro ya Gehenna ni wale ambao hawakudhulumu wafanyikazi wa nyumbani (Uk. 3).

Mhusika mashuhuri anayetuhumiwa na kosa hili la unyanyasaji wa wafanyikazi wa nyumbani ni Bi. Saeda Khan. Alikuwa anakabiliwa na shtaka la kumtesa mwajiriwa wake Bi. Mwanahamisi Mruke. Bi. Saeda Khan alishtakiwa kwa kosa la kuingiza mwanamke nchini Uingereza kwa minajili ya kumpunja baada ya kuwasili kwake. Ilisemekana kuwa Mruke alifanya kazi kuanzia saa kumi na moja alfajiri hadi asubuhi iliyofuta. Alifanya kazi zote za nyumbani pamoja na kuwaangalia watoto wa Bi. Saeda Khan ambao walikuwa na ulemavu. Hakuruhusiwa ale na familia na mara nyingine alipewa mkate kama chakula na wakati mwingine hakupewa chochote. Hakuwa na chumba cha kulala, alipewa kigondoro chembamba na bedishiti na kulala kwenye sakafu. Hakupata mapumziko wala kuruhusiwa kutoka nje bila kuwepo Bi. Saeda khan. Wazazi wake wanapougua, hakupewa hela na ruhusa ya kwenda kuwaona hadi wakafariki. Mruke anamwona Dkt. Musa katika kituo cha matibabu na kumueleza alivyoteswa na Bi. Saeda Khan. Bi. Mruke baadaye anatolewa na polisi na kupangiwa

makazi. Mnamo Jumatatu tarehe 22 Machi 2050, Bi. Saeda Khan alitiwa nguvuni kwa shtaka la kuwasafirisha watu na kuwapunja (Uk. 88).

Bi. Rabecca Balira alikuwa mshukiwa wa pili aliyehusika na upunjaji wa wafanyikazi wa nyumbani. Mfanyikazi wake alikuwa Methodia ambaye alikuwa amesafirishwa kutoka Kenya kumfanyia kazi. Mhasiriwa alidai kuwa alishawishiwa na kudanganywa kuwa mtumwa nyumbani. Alisema kuwa stakabadhi zake za usafiri zilikuwa zimetwaliwa na mwajiri wake. Alikuwa ametiliwa vikwazo kama vile; kutembea, kudhulumiwa kimwili na kutukanwa na mwajiri wake. Vilevile, alifanya kazi kwa masaa mengi, alipewa makazi mabaya na alizuiliwa kuwasiliana na jamii yake na wengine. Methodia alitoroka baada ya kupewa ushauri na mama mmoja (Uk. 96).

Suala la unyanyasaji limekuwa sugu miongoni mwa nchi nyingi za Afrika. Wafanyikazi husafirishwa kwenda huko ughaibuni na wakifika wanaanza kukandamizwa na kudhulumiwa. Kumekuwa na visa vingi vya wasichana ambao hata wamepunjwa hadi wakafa. Wengine hupata usaidizi kutoka kwa serikali husika na kurudi makwao. Wakifika wengi huwa wamedhoofika kimwili. Kinaya ni kuwa, hata baada ya suala hili kuwa sugu na kutangazwa katika vyombo vya habari bado wasichana wanasafiri nchi hizo kufanya kazi. Wengine wakiwa kwa uwanja wa ndege wakirudishwa makwao wengine wanasubiri kwa uwanja wa ndege kusafiri kwenda huko. Umaskini ndio chanzo kikuu cha wasichana kutaka kwenda kufanya kazi za nyumbani nchi za nje.

### 2.4.3 Hongo

Hongo ni hali ya kutoa pesa au chochote kile ili kupata huduma hasa kutoka kwa mtu ambaye huwa na madaraka. Mugwika (2012) anasema kuwa, ufisadi hutekelezwa na vigogo serikalini. Wanahusishwa na kupokea na kutoa mlungula kwa waliopewa

kandarasi ya uuzaji mashamba yaliyotengewa miradi ya kunufaisha umma. Vilevile, anaeleza kuwa Avad alikuwa amekubali hongo na kujilimbikizia mali kwa njia isiyofaa. Muthui (2019) anasema kuwa kupata kandarasi ilitagemea ulimjua nani serikalini.

Ufisadi katika riwaya ya *Mafamba (*Olali,*2012)* umeota mizizi na taasisi zinakubali ulaji wa mlungula. Mwandishi anasema kuwa, ufisadi umekithiri hadi kuchapishwa kwenye vyombo vya magazeti. Kunaibuka kichwa katika gazeti moja la BORA kuhusu ufisadi kutoka sayari moja ya nje. Gazeti linasema hivi;

> OVER 2,000 FIRMS IN BRIBES SCAM
>
> ZAIDI YA KAMPUNI 2,000 KUHUSISHWA NA KASHFA YA RUSHWA (Uk211)
> (Tafsiri yangu)

Makundi mawili yaliibuka baada ya azimio la siri ya mbuyu kuibuliwa. Kundi moja likiongozwa na Amrao likiwa na ishara ya ndege Njiwa na Kundi la pili liliongozwa naye LiMioe likichukua ishara ya mnyama Mumbi. Aliyetaka azimio la siri ya mbuyu alihitajika kuimba Mumbi. Aliyepinga Azimio la siri ya mbuyu alihitajika kuimba njiwa. Kundi la Mumbi liligawanyika katika maeneo sita ya kijiografia. Kieneo lilikuwa na kiongozi wake. Watu wa maeneo haya walianza kuzawadiwa vyakula mbalimbali ili waunge mkono Azimio la siri ya Mbuyu. Watu waliokuwa maskini walizidi kutajirika baada ya muda mfupi. Mwandishi anasema;

> Watu wa maeneo haya walianza kuzawadiwa vitafunaji mbalimbali. Wale ambao zamani walikuwa maskini, walianza kuwa matajiri. Wale ambao walikuwa wanamwimba ndege mumbi walikuwa matajiri mara moja au kuahidiwa vitafunaji (Uk. 228).

Maeneo mbalimbali ya sayari ya BORA yalizawadiwa pia. Eneo la Ma lilipewa ardhi, Ai kiwanda cha nyama, Fa hifadhi kubwa ya wanyama, Ao madeni yake yalifutwa. Isitoshe, Watu wa Me waliahidiwa uwanja wa F-16, nao wa Ba nasari kubwa kuliko nasari zote za wilaya mbili. Wakereketwa sugu wa Njiwa walihamia Mumbi kwa

sababu ya zawadi hizi (Uk. 229). Vilevile, viongozi ambao walimsaidia LiMioe katika utawala wa mashinani, watu wa chini kabisa katika utawala wa LiMioe waliongezewa mapato maradufu. Katika sayari ya NUKA ufisadi ulikuwa umehalalishwa. Mwandishi anatumia neno *Mfuko wa vito* na *Nopro* kudhihirisha hongo. Anasema kuwa, wahusika walitiwa muhuri wa nopro ili kupewa kibali cha kuendeleza ufisadi. Wanyonge hawakuwa na haki katika sayari ya NUKA. Viongozi wangefanya maovu kama vile mauaji na kukamatwa. Waliowakamata walihongwa na hivyo kuachiliwa (Uk. 88).

Mwandishi anadhihirisha hongo kupitia mhusika Maotad. Maotad anamwita Avad ofisini mwake kumshawishi ajiunge na kikundi cha NUKA. Anamtishia kukamatwa kwa kuwa alikuwa ameshiriki katika maovu ya ufisadi. Anamwambia kuwa chochote ambacho alikuwa nacho alipata kwa njia ya ufisadi kwa kutoa hongo (Uk. 154). Avad analazimishwa kuligura kundi la BORA ingawa alijua lilikuwa kundi lenye uwezo mkubwa. Hakuweza kumpinga Maotad. Alifahamu walungula na kukubali wadhifa huo shingo upande (Uk. 157).

Katika mtaa wa Bikerani-Msiige, viongozi wanashiriki katika biashara haramu ya ukataji miti. Yupo mtu mmoja tu aliyekamatwa na kufungwiwa miaka saba gerezani. Mtu huyo alijulikana kama Sikujua. Hakuelewa sababu yake kukamatwa na wengine walioshiriki katika shughuli hiyo hawakukamatwa. Mwandishi anasema kuwa wenye kukamatwa walisubiri hadi usiku wa manane. Shanata zilibebwa nzito sana. Kilichokuwa ndani hakikujulikana. Kesi ilitupiliwa mbali zamani za kale. Mayieka (2015) anasema kuwa kamati ya uhasibu hupokea hongo na kuandaa ripoti za kupotosha kisha majina ya watu wenye ushawishi wanaohusika na kashfa hii yanaondolewa. Baadaye, Sikujua alifahamu kuwa walioachiliwa walikuwa wametoa kitu kidogo (Uk. 174).

Akiwahutubia wananchi na kuwaomba kura, LiMioe anadhihirisha kuwa utawala wa NUKA kwa uongozi wake Maotad ulikuwa umekoleza utoaji wa hongo. Anasema kuwa, ameunda tume za kuchunguza ulanguzi na kashfa ya mfuko wa vito (hongo). Vilevile, anasema kuwa yeyote atakayepatikana akiendeleza umangimeza katika afisi za serikali kwa sababu anataka mlungula, atakuwa anashiriki ufisadi. Hiki ni kinaya kwa sababu hata baada ya kuchaguliwa, LiMioe anajihusisha kwa nyendo hii chafu ya ulaji mlungula.

Biashara nyingi haramu zimekolea katika jamii kwa sababu ya utoaji hongo. Wanaohusika hutoa kitu kodogo kisha kuachiliwa. Vileo hatari pia huuzwa vijijini ambavyo vimeathiri watu wengi sana. Wenye kuuza vileo kawaida watalipa kitu kidogo na kuendeleza biashara yao bila hatia yoyote. Biashara haramu zinaendelezwa katika utawala wa BORA. Biashara hizi ni kama kuuza vileo hatari. Wanaohusika wanaishi kukamatwa kila mara na kuachiliwa kwa sababu walikuwa wanatoa hongo. Tazama mfano ufuatao;

> Mwenye kuuza kileo kile hatari alijulikana na wakazi wa Tuga Amor. Serikali ya BORA ilimfahamu vema. Alichukuliwa hatua na kukamatwa mara saba. Na kila mara hizo saba, aliachiliwa huru mara saba kwa sababu ya sera ya Nopro (Uk. 191).

Mzee Twajua wa kijiji cha Tuga Amor katika hotuba anadhihirisha sura hii ya ufisadi. Anawaelezea watu kuwa NUKA ilipokuwa madarakani ilishiriki mafamba kwa njia ya hongo na vilevile BORA.Mzee Twajua anasema kuwa, utoaji hongo umesababisha ufisadi katika sayari hiyo. Anasema kuwa hakuna ufisadi mbaya zaidi ya kutoa hongo. Anaongeza kuwa, watu wanakamatwa kuhusiana na kashfa ya hongo na kuachiliwa. Aidha, anaeleza vile watu walikuwa wamejenga majengo maovu katika mji wa Kar Pi Mangich. Majengo hayo yanaporomoka na wenye majengo kutoweka baada ya kufanya

kazi mbovu.  Kwa sababu ya hongo, tume ya Kar Pi Mangich iliidhinisha majengo hayo yaendelee. Baada ya miezi chache majengo hayo yaliporomoka na kuwaua watu wengi (Uk. 209).

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), hongo imedhihirika kwa namna mbalimbali. Wakati mwingi, hongo hutolewa kwa ajili ya kupata upendeleo kutoka kwa watu wenye mamlaka. Hongo ni adui ya haki na huathiri maendeleo katika jamii. Ndung'u (2022) anasema kuwa, ufisadi ni maovu yanayotendwa na mtu ili kujinufaisha au kunufaisha makundi ikiwepo kupeana rushwa na matumizi mabaya ya mali ya umma. Anaeleza jinsi ufisadi ulivyokolea katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) ingawa hajadhihirisha sura mbalimbali za ufisadi ambazo zinapatikana pale. Anaelezea ufisadi kwa ujumla kama matumizi mabaya ya pesa za umma.Ufisadi si matumizi mabaya ya mali ya umma tu ila kuna sura tofauti za ufisadi kama ilivyo katika muhimili wa nadharia ya udenguzi kuwa maneno ya matini hujenguana na kupingana zenyewe na hivyo matini kuibua fasili nyingi.

Munkari anasema kuwa viongozi hutisha wanahabari ili waogope kufanya kazi kikamilifu na kuficha maovu ya ufisadi. Wamiliki wa vyombo vya habari vilevile ununuliwa mradi wasiweze kutumia fursa zao kukomesha ufisadi (Uk. 234). Muziki *Watajuta* uimbwao Gehenna unadhihirisha suala hili. Mwandishi anasema;

> "Watajuta kupokea rushwa kazini (Uk. 8)

Hongo pia hutolewa na wanabiashara. Wakati mwingine huuza bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Wakijulikana huwa wanahonga bodi inayohusika na kuachiliwa huru. Baadhi ya bidhaa ambazo watu utoa hongo ili waruhusiwe kuuza ni kama vile dawa za kulevya na vipodozi. Mwandishi anatumia wahusika Faki Nahodha na Baadayadhiki kuelezea suala hili. Wakibadilishana hadithi zao, Faki Nahodha

anasema kuwa kwao Al Jazeera bidhaa bandia ambazo hazifai matumizi ya binadamu huuzwa kote. Wanaohusika hushikwa kisha kutoa hongo kwa Afisa mwezeshaji wa Bodi ya chakula, dawa na vipodozi (Uk. 78).

Cheche za kutafuta uhuru hutokana na wananchi maskini. Mhusika Hikmat anawania kiti cha ubunge kwa Chama cha Mwananchi ndotoni. Wanajamii wanamwombea ili awe na ujasiri katika kuwakomboa wananchi kutokana na umaskini. Akiwahutubia wafuasi wake, anasema kuwa kura za maoni hutawaliwa na chirimiri (hongo). Chama tawala hujengwa kwa vitisho na matumizi ya nguvu za hela. Hikmat anasema hongo ni adui wa haki na imeathiri sekta zote. Tazama mfano ufuatao:

> Chirimiri sio tu adui wa haki bali pia ni kikwazo cha maendeleo. Chirimiri imeiathiri sekta zote za nchi yetu kiasi kuwa ili mtu apate haki yake hana budi kujipapasa (Uk. 156).

Hongo ndio chanzo cha umaskini katika nchi nyingi. Kuna hongo ya kiwango cha chini na kiwango cha juu. Hikmat anasema hongo ikitokea kwa nchi maskini inaitwa rushwa ilhali ikitokea katika nchi tajiri inaitwa kashfa. Hikmat anasema kuwa, pesa ambazo hupatikana kwa njia ya rushwa huhifadhiwa katika nchi tajiri. Tazama mfano ufutao:

> Tatizo kubwa kwa nchi za Kiafra ni kuwa fedha zinazopatikana kwa rushwa, Kiafra hupewa sehemu ya kuhifadhiwa katika nchi Tajiri. Dunia inapoteza kiasi cha dola zisizopungua trilioni moja kwa mwaka kutokana na rushwa (Uk. 179).

Munkari akielezea madhara ya ufisadi kwa watu wa Gehenna anasema kuwa rushwa ndio adui namba moja ya haki. Anasema rushwa uharibu dhana nzima ya uadilifu na kuhatarisha maendeleo ya uchumi, amani, mashikamano na umoja wa Kiafra (Uk. 223). Nyamaume akizungumza na Munkari anataka kujua maana ya *Matrix of Corruption*. Munkari anamjibu Nyamaume kuwa ufisadi ni wasilisho la wananchi katika Kiafra kuhusu vitendo vya rushwa, wizi, ukwapuaji au udanganyifu wa kupindukia wa fedha

na mali za umma unaofanywa na kikundi kidogo cha watu kinachohusisha baadhi ya viongozi wa serikali na wafanyabiashara wakubwa (Uk. 225). Munkari anasema kuwa ufisadi ukiwa sehemu ya utamaduni wa Kiafra, rushwa na wizi haviishi kufanywa na watu wenye mamlaka peke yao bali vitendo hivyo husambaa na kujengeka kwa watawaliwa. Munkari anazidisha kwa kusema kuwa, viongozi wengi hutoa hongo kwa wapiga kura ili wapigiwe kura. Tazama mfano ufuatao;

> Hii imewezekana kwa kuweka mikakati mahususi ikiwa ni pamoja na kuhonga wananchi kwa fedha, mavazi, chakula na vitu vingine vidogo vidogo kukidhi mahitaji ya fukara, kunua shahada za wapiga kura ili wasiweze kupiga kura, kuwatishia wananchi kwa kutumia vyombo vya dola, kuunda vikundi vya kihalifu kuwashambulia, kuwafilisi na kuwatisha watu watakaonekana kuunga mkono vyama vingine (Uk. 234).

Munkari anaendelea na mhadhara wa *The matrix of Corruption* Kiafra na kusema kuwa, viongozi hununua baadhi ya maafisa wa tume ya uchaguzi ili majina ya wapiga kura yavurugwe hasa kwenye maeneo ya upinzani wasiweze kupiga kura kabisa au wakati uliopangwa (Uk. 235). Hili ni jambo ambalo limekuwa likitendeka katika nchi nyingi duniani. Kiongozi aliyetakikana na kuchaguliwa na wengi ashinde. Matangazo hutokea vinginevyo. Hii ni kwa sababu viongozi hao hutoa hongo kwa tume husika ili kuwaibia kura kwa njia yoyote ile. Kesi dhidi ya uchaguzi zimeishi kubatilishwa pia. Walioibiwa kura hata wakipeleka kesi kortini hushindwa kwa sababu viongozi hao uhonga hadi mahakama ya juu.

### 2.4.4 Ulaghai

Ulaghai ni udanganyifu au matumizi ya uwongo ili kupata faida kwa njia ya kudhulumu mtu. Wamitila (2003) Ulaghai ni hali ya kudanganya au kudharau wengine kwa lengo la kupata faida au kuathiri matokeo kwa njia isiyo halali. Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), mwandishi amedhihirisha aina mbalimbali za ulaghai. Okemwa (2017),

anaeleza ulaghai kama maudhui tofauti na ufisadi. Nadharia ya Udenguzi inaeleza kuwa kazi ya mhakiki ni kuibua na kujumuisha kile kilichonyamaziwa na kupuuzwa na wahakiki wengine. Katika utafiti wetu, tumeeleza ulaghai kama sehemu ya ufisadi ila si maudhui kivyake. Okemwa (2017) anaeleza pia namna wahusika walivyosaidia wengine kwa ajili ya kuwalaghai. Pia, anaeleza namna Wachuna walivyotumia woga na hofu kujilimbikizia mali. Wanatunga sheria zinazowalinda. Anasema kuwa wachache hutumia ulaghai kujinufaisha huku wengine wakiteseka. Ni bayana kuwa, watu wanapaswa kuelimishwa ili waweze kutoa minyororo ya ulaghai.

Kuna watu wengi ambao hawalipi kodi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012). Ajuza mmoja aliwaona watuza ushuru kupe. Kila walipomwambia alipe ushuru alirusha matusi mazito zaidi na wao wakasalimu amri na kwenda zao (Uk. 198). Pili, mwandishi anasema utawala wa BORA ulikusanya kodi ingawa kuna baadhi ya watu ambao walikataa kulipa ushuru. Tatu, mabwenyenye wa mtaa wa Bikereni-Msiige walikata miti kuuza na kuzipeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru wowote (Uk. 173). Matajiri wengi katika sayari ya NUKA walitoa hongo baada ya kutenda maovu kama mauaji, ukataji wa miti, kujenga majengo maovu na kuuza vileo hatari. Huu ni ulaghai wa kifedha. Matajiri hao pia wanadhihirisha ulaghai huu kwa njia ya ubadhirifu. Mwandishi anasema kuwa viongozi walibinafsisha raslimali za nchi kwa mlango wa nyuma (Uk. 243). Katika hotuba ya LiMioe, anasema kuwa magari yote rasmi ni yao, ngilishi zote ni zao watumie watakavyo kwa kuwa alikuwa ametoa amri. Tazama mfano ufuatao,

> Magari yote rasmi ni yetu sasa, ngilishi zote ni zetu sasa. Mtumieni mtakavyo. Mimi nimetoa amri. Mimi LiMioe (Uk. 216).

Miradi hewa pia ni mfano wa ulaghai wa kifedha. Mzee Twajua anasema kuwa utawala wa BORA uliunda bajeti hewa. Anaongeza kwamba, uhalifu ulikuwa umeongezeka kwa sababu vyombo vya ulinzi vilisemekana kununuliwa lakini havikuonekana. Anasema;

> Ile bajeti haikunununa hata bastola moja ile bajeti ya ngilishi bilioni 666! (Uk. 210).

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), suala hili la ulaghai linadhihirika kupitia sakata mbalimbali ikiwemo sakata ya *Mfuko wa vito* na *Anglolasting*. Sakata hizi zilinufaisha viongozi kama vile Engineer wa utawala wa BORA. Kupitia hadithi ya Mzee Twajua, Engineer alikuwa mfisadi ambaye anahusishwa na miradi hewa. Mwandishi anasema;

> Unamaanisha kuwa bidhaa hutanunua lakini utazilipia. Mimi nitakupa chako na wewe unipe changu (Uk. 207).

Vilevile, mwandishi anasema kuwa watu walioanika watu mafisadi kama Jogi walikosa amani na kuguria sehemu zingine ili kuokoa maisha yao. Watu walijiuliza bajeti ya vyombo vya ulinzi ilinunua nini kwa sababu yale yaliyosemekana kununuliwa hayakuonekana. Bajeti haikunua hata bastola moja. Mwandishi anasema kuwa, kampuni haikujulikana ni ya nani na pia, jina la kampuni haikujulikana. Sayari inayohusika na na sakata hiyo pia haikujulikana. Engineer anatakikana kueleza kwa nini alifanya kazi na mapepo, ni vipi alitumia akaunti hewa. Mwandishi anasema kuwa, Engineer alikuwa ndiye kiwakilishi cha Mafamba na Nopro katika utawala huu mpya. Walitaka ajiuzulu kwa sababu ya miradi hewa.

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), kuna wimbo ambao unadhihirisha ulaghai unaoendelezwa na watu wa Gehenna. Munkari anasema kuwa watajuta kwa

kuuza bidhaa bandia, watajuta kwa kuuza viwiliwili vya albino, kuongeza bei za bidhaa kiholela (Uk. 9). Huu ni ulaghai. Mwandishi anamtumia mhusika Faki Nahodha kutoka Al Jazeera Al Khadra adhihirisha ulaghai. Faki anahadithiana na Baadayadhiki kuhusu maisha ya Al Jazeera. Faki anasema kuwa wafanyi biashara wa Al Jazeera ni wafisadi. Huwalaghai watu kwa kuwauzia bidhaa ambazo hazifai kutumika. Badala ya watu hawa kukamatwa, wenye maduka hutoa hongo kwa Afisa Mwezeshaji wa Bodi ya chakula, dawa na vipodozi (Uk. 78).

Mwandishi anadhihirisha ulaghai ambao wafanyikazi wa nyumbani hufanyiwa. Bi. Mruke alimfanyia kazi Bi. Saeeda Khan na kulipwa mshahara wa laki moja za Kenya kama walivyokubaliana. Baadaye, hela za pauni kumi za mwezi ambazo alikuwa anapewa zilisimamishwa. Aipotaja suala la pesa alinyimwa. Wazazi wake walipougua, aliitisha hela kwenda kuwajulia hali bali hakupewa ruhusa ya kufanya hivyo. Hivyo basi, wazazi wake walifariki akiwa huko Uingereza kwa kukosa pesa za kuwapeleka hospitali ilhali alikuwa ameajiriwa.

> Katika mwaka wa kwanza, Bi. Mruke alimfanyia kazi Bi. Saeeda Khan, alipata mshahara ambao walikuwa wamekubaliana wa shilingi laki moja za Kenya na pauni 10 za Uingereza, lakini baadaye nyuma, hela za pauni kumi kwa mwezi ambazo alikuwa anapewa na Bi. Saeeda Khan zilisimamishwa (Uk. 87).

Mwandishi anatumia ndoto kudhihirisha ulaghai. Katika ndoto ya Hikmat, Madaktari huwalaghai watu kwa kuwauzia dawa bandia. Mwandishi anadhihirisha kuwa, maduka binafsi yamegeuka kuwa karakana ya sumu. Madawa hukosekana katika hospitali za umma hivyo kuuzwa katika hospitali za kibinafsi. Anaongeza kuwa, dawa zenyewe hazina sifa za dawa.

> Maduka binafsi yamegeuka kuwa karakana za sumu na hatimaye mauti ya wagonjwa, kwa sababu ya wingi wa fake drugs. Hospitali zinajali zaidi biashara kwa maana ya kuingiza fedha. Ndiyo maana hata anayefanya kazi kwenye hospitali ya serikali anamwagiza mgonjwa aende kununua dawa au vifaa mtaa wa tatu (Uk. 177).

Baingana anasimulia kuhusu wizi wa viwiliwili katika hospitali ya Asomtakatifu Reficul. Hii ilikuwa baada ya kugongwa na gari la mchungaji wake Taabu. Ilisemekana kuwa Taabu na Bi. Saeeda Khan ndio waliokuwa maarufu katika biashara hii ya kuuza sehemu za mwili. Wawili hawa walilipa watu kuwatafutia sehemu hizo katika makafani ili kwenda kuuza. Baingana anasimulia mazungumzo ya baadhi ya waliokuwa wanafanya kazi hiyo ya kukata sehemu za siri. Anasema kuwa, nyeti ilikuwa ghali iligharimu laki moja. Baingana anasema;

> Mara simu ililia ". Heloo afande!"
> "Asifiwe Afisul yaani unatuletea miili minne?"
> "Utapata sehemu yako. Ile hundi ya juzi pia imeiva. Kesho saa tatu tukutane nje ya benki."
> "Asante afande!"
> "Ndiyo daktari mtajuta anatekeleza lile jukumu tulilompa"
> "Ndiyo, atakuwepo nje ya benki kesho" (Uk. 198).

Munkari anasema kuwa kumekua na mitandao mingi ya kujipatia fedha haramu. Viongozi wanapora wanyonge mali yao kwa kisingizio cha uwekezaji. Raslimali za nchi kama vile madini, samaki na pembe za ndovu huporwa kiholela na wanyonge kukosa haki mbele ya vyombo vya sheria. Hii huzuka kwa sababu ya tamaa ya utajiri suala analoliita umimi. Umimi ni aina ya ulaghai ambapo, wahusika ni matajiri wanaowakandamiza wanyonge kupitia uporaji. (Uk. 227).

Katika Riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), mwandishi anadhihirisha ulaghai wakati Munkari anahukumia watu wa Gehenna kwa kosa la kuwa na miradi hewa. Anasema kuwa viongozi wengi wa Kiafra ung`ang`ania madaraka kwa ajili ya maslahi yao kibinafsi. Chama tawala huweza kufanya lolote lile ili kishinde uchaguzi. Ondoro

(2021) anasema kuwa viongozi wengi utoa ahadi za miradi ambayo wanatekeleza endapo watachaguliwa. Mwandishi anaendelea kusema kuwa viongozi wanapochaguliwa husaliti wananchi kwa kuvunja ahadi zao. Fedha za kutengeneza ushindi huwekwa kwenye bajeti ya serikali kwa kuingiza miradi hewa au pesa kutokana na mikataba mibovu. Vilivile, viongozi hutafuta watu na kuwapa zabuni bandia za serikali ambazo hulipwa pesa nyingi kwa makubaliano kuwa watamega pesa nyingi zitakazopatikana kwa njia ya ufisadi ili kusaidia chama tawala kushinda uchaguzi. Munkari anasema;

> Isitoshe, inapokuwa ni utamaduni wa chama tawala kushinda uchaguzi kwa gharama yoyote ile, fedha za kutengeneza ushindi zinaweza zikawekwa kimkakati katika bajeti ya serikali kwa kuingiza shughuli au miradi hewa au zikapatikana kutokana na mikataba mibovu na dalili ya uwekezaji (Uk. 231).

### 2.4.5 Kuwekeza Akiba Nchi Za Nje

Kulingana na Lomatoro (2014), ufisadi ni wizi wa pesa. Anaongeza kuwa, viongozi waliiba pesa ingawa zilikuwa za kukopa. Isitoshe, viongozi huiba kisha mzigo wa kulipa huenda kwa wananchi. Bali na kuiba, viongozi huvuruga sheria. Anasema kuwa wananchi hawajawajibika kwa kuwa, huwachagua viongozi walewale. Anasema kuwa, suala la wizi wa pesa limekuwa la kawaida. Ameonyesha sura hii ya ufisadi ingawa amesisitiza ufisadi kama matumizi mabaya ya mali ya umma. Kulingana naye, viongozi huwekeza pesa nchi za nje mipango yao ikifeli hulalamikia mashirika. Ukweli ni kuwa, viongozi huwekeza akiba nchi za nje ili kuepuka ulipaji kodi. Hivyo basi, ni jukumu la wananchi kuungana, kupiga kura kwa wingi na kuteua viongozi bora bila ufisadi wowote.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) mwandishi ametumia wahusika tofauti kudhihirisha sura hii ya ufisadi. Maotad anadhihirisha Avad kama mfisadi. Baada ya

Maotad kumualika Avad sebuleni ili kumshawishi kukwepa sayari ya BORA anamwambia;

> Huna chochote ulichonacho bila Mafamba.Chichiri si dhambi?" Si magari, si mashamba, si nyumba, si makaburi, si mito, si makahaba, si akiba katika sayari nyingine. Zote hizi zinatokana na mafamba. Leo mafamba ni shetani (Uk. 154).

Maotad anamwambia kuwa alikuwa ameshiriki katika ufisadi kwa kuwekeza akiba nchi za nje na hivyo hakuwa tofauti naye. Matajiri wengi hujihusisha katika biashara haramu kisha kuwekeza pesa zao katika nchi za nje ili wasijulikane. Viongozi wa mtaa wa Bikerani-Msiige walikata miti, kuiuza na kupeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru wowote. Mwandishi anasema;

> Ekari nyingi za misitu zilinyakuliwa na kasri za ajabu kujengwa humo na mbao za bei hali kutoka aina nyingi za miti katika misitu hiyo kama vile mingambu, mikurungu, mikwaju, mipingo, migombakofi ziliuzwa na wenye kuziuza walizipeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru (Uk. 173).

Wengi wa waliokamatwa dhidi ya maovu haya ni maskini kama vile Siyawezi. Mhusika huyu hakuwa na uwezo wa kutoa hongo kama walivyofanya matajiri waliopatikana katika hatia hii. Matajiri walizidi kusaka mali kwa njia isiyo halali huku maskini wakitaabika.

Mhusika Mzee Twajua katika hadithi yake anadhihirisha uwekezaji wa akiba katika nchi za nje. Anasema kuwa, utawala wa BORA ulikuwa umeandika hundi ya ngilishi bilioni 666 kwa muuzaji wa sayari moja ya nje. Mzee Twajua anasema kuwa viongozi waliona ustaarabu kuwekeza ngilishi nje ya sayari ya BORA.

> Utawala wa BORA ukaandika hundi ya ngilishi bilioni 666 kwa muuzaji yule. Akaunti ya kupelekwa hundi hiyo ilikuwa ni ya Engineer nayo ilikuwa iko sayari moja ya nje. Ilikuwa ni ustaarabu kuzihifadhi ngilishi nje ya sayari ya BORA (Uk. 170).

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), viongozi wanawekeza nchi za nje. Suala la kuwekeza akiba nchi za nje huhusishwa na matajiri. Wengi huwekeza nje kwa sababu ya kukwepa ushuru au kwa kuwa ni mali ya wizi na hawataki kujulikana. Mwandishi amedhihirisha suala hili ambalo linatokea Kiafra. Anasema kuwa watu waliopokea rushwa walikuwa wanawekeza nchi za nje. Ambrose (2014) anasema kuwa viongozi kazi yao ni kujilimbikizia mali na kuhifadhi katika nchi za nje ili wasijulikane kuwa wana mali nyingi. Mwandishi wa riwaya ya *Watu wa Gehenna* anasisitiza kuwa mafisadi hao pia walijihusisha na wizi na kuhamisha utajiri wao kutoka Kiafra kwenda kujitajirisha zaidi nchi nyingine. Mwandishi anatumia mhusika Hikmat kudhihirisha hili katika ndoto. Anasema;

> Tatizo kubwa kwa nchi za Kiafra ni kuwa fedha zinazopatikana kwa rushwa, Kiafra hupewa sehemu ya kuhifadhiwa katika nchi tajiri. Dunia inapoteza kiasi cha dola zisizopungua trilioni moja kwa mwaka kutokana na rushwa (Uk. 179).

Hikmat anasema kuwa dunia upoteza kiasi cha dola trilioni moja kwa mwaka kutokana na rushwa. Fedha zinazopatikana kwa rushwa ndio huwekezwa nchi tajiri. Anasema kuwa, jambo hili husababisha umaskini katika jamii mbalimbali katika Kiafra. Rushwa ikitokea nchi tajiri huitwa Kashfa ilhali ikitokea nchi maskini inaitwa rushwa.

Munkari katika hukumu yake Gehenna anasema kuwa, ufisadi ni ugonjwa. Suala hili limesababisha umaskini Kiafra. Ufisadi hutokana na uongozi wa nchi na uongozi wa nchi hutokana na siasa za chama. Anasema kuwa, kukomesha ufisadi ni wanasiasa kuweka pembeni maslahi yao kibinafsi pamoja na ya vyama vyao na kujali zaidi

maslahi ya taifa. Anaongeza kuwa, siku hizi utandawazi hutumiwa kuteka vyama vya kisiasa na mafisadi na hivyo chama kujikuta kinakuwa mawakala wa mafisadi ambao lengo lao ni kuiba na kuwekeza nchi nyingine.

> Ni viongozi, makada na wananchi wangapi wa vyama vya siasa ambao wanafahamu kuwa katika enzi hizi za utandawazi vyama vyao vinaweza kutekwa kwa urahisi na mafisadi na hivyo chama kujikuta kinakuwa wakala wa mafisadi wenye lengo la kuiba na kuhamisha utajiri wa Kiafra kwenda kujitajirisha nchi nyingine (Uk. 223-224)

Nadharia ya Udenguzi inasisitiza katika mhimili wa pili kuwa kazi ya fasihi ina maana ya ndani inayopatikana ikifasiriwa kwa undani. Katika utafiti wetu, tumebaini kuwa uwekezaji wa hela katika nchi za nje ni aina ya ufisadi. Watafiti wengi wameeleza tu istilahi hii kivyake ila hawajaiweka kama sura ya ufisadi na vile vile wanaeleza ufisadi kama matumizi mabaya ya mali ya umma tu.

### 2.4.6 Ukwepaji Kodi

Hili ni jaribio lisilo halali na la kimakusudi la kulipa kodi kidogo au kutolipa kodi. Suala hili la ukwepaji kodi hudhihirishwa sana na matajiri. Wengi wao hupata mali kwa njia isiyo halali kisha kukwepa kodi. Mutuku (2016) anasema kuwa, kodi ilitumika na wakoloni kama njia ya kunyanyasa wananchi. Wanaume walilazimika kuacha mashamba na kutafuta kazi. Yeyote aliyeshindwa kulipa kodi alifikishwa mahakamani. Ni dhahiri kuwa, ukoloni mambo leo ni tofauti. Watu wa tabaka la chini ndio hulipa kodi ilhali wengi wa viongozi na matajiri wa nchi wakikwepa kulipa kodi. Ni jukumu la serikali hasa kupitia sheria ya kodi na mapato (KRA) kuhakikisha kila mtu amelipa kodi na wale ambao hawajalipa wakamatwe. Ufisadi si matumizi mabaya ya pesa za umma tu.Hali ya kutolipa kodi pia ni aina ya ufisadi.Hii inaafikiana na mhimili wa nadharia ya udenguzi kuwa hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi na maana kulingana na matini tofauti ya fasihi ni telezi.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), mwandishi amedhihirisha ukwepaji kodi katika mtaa wa Bikerani-Msiige. Anasema kuwa, ekari nyingi za misitu zilinyakuliwa na mbao za bei ghali kuuzwa na wenye kuuza walizipeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru wowote.

> Ekari nyingi za misitu zilinyakuliwa na kasri za ajabu kujengwa humo na mbao za bei ghali kutoka aina nyingi za miti katika misitu hiyo kama vile mingambu, mikurungu, mikwaju, mipingo, migombakofi ziliuzwa na wenye kuziuza walizipeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru (Uk. 173).

Mzee Twajua wa kijiji cha Tugor Amor anasimulia kisa cha ajuza mmoja ambaye hakulipa kodi. Anawaona watoza ushuru kama kupe. Badala ya kulipa ushuru aliwarushia matusi mazito.

> Mama yule aliwaona watoza ushuru kama kupe. Kila walipomwambia hivyo, alirusha matusi mazito zaidi na wao wakasalimu amri na kwenda zao (Uk. 198). Mwandishi pia anadhihirisha suala hili katika muktadha tofauti. Anasema kuwa baadhi ya watu wa Sayari ya BORA walikwepa ushuru kama yule ajuza wa Tuga Amor (Uk. 229).

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) mwandishi anadhihirisha sura hii ya ukwepaji kodi. Miaka ishirini baada ya Hikmat kumaliza masomo yake, anaota ndoto halaiki kubwa ikimwombea dua wakati wa kuzindua kampeni za ubunge kwa chama cha Mwananchi.Katika kampeni zake, anasema kuwa serikali inakusanya kodi ambayo haisaidii wananchi bali inawanyanyasa wananchi wa tabaka la chini. Chama tawala huwatoza kodi watu wa tabaka la chini na kuwasamehe watu wa tabaka la juu. Baada ya kusema hili, umati unamshangilia Hikmat. Anasema;

> Kodi inayokusanywa sasa na serikali haichangii maendeleo ya nchi tu bali inawanyanyasa wananchi wa chini. Tukiingia madarakani, kodi zinazoitwa za maendeleo tutazifuta. Hizi ni kodi za manyanyaso. Chama kinachotawala kinawatoza watu wa chini kodi na kuwasamehe watu wa juu. Kodi za manyanyaso zinaingiza fedha chache mno ikilinganishwa na kodi zinazosamehewaa watu wa daraja la juu (Uk. 159).

Watu ambao hukwepa ulipaji kodi ni watu wa tabaka juu. Maskini hutozwa kodi za manyanyaso ambazo huingiza fedha chache mno ikilinganishwa na kodi zinazosamehewa watu wa daraja la juu. Ondoro (2021) anasema kuwa wanaotozwa kodi ya juu hufanywa vibarua vya kutumikishwa katika mashamba ya mabwenyenye. Jambo hili huzidisha utabaka. Matajiri huzidi kutajirika na maskini uzidi kuwa maskini.

### 2.4.7 Wizi wa kimabavu

Njenga (2021) anasema kuwa, ufisadi ni matumizi ya ofisi za umma kwa lengo la kujinufaisha kibinafsi. Akielezea suala la wizi katika ufisadi, wenye mamlaka huiba mali ya umma kuendeleza maslahi yao ya kisiasa. Wizi husababisha uzorotefu wa uchumi. Wenye hutaabika katika hali hii ni maskini. Wizi ni tendo la kuchukua mali au milki ya mtu mwingine na kutaka kuimiliki bila idhini yake. Kuna aina mbalimbali za wizi. Wizi wa mali, wizi wa mitihani na wizi wa kura.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) kuna aina mbalimbali za wizi. Kwanza kuna wizi wa kura. Mwandishi anaelezea kwa kusema kuwa;

> Uliposhindwa ulishinda. Uliposhindwa ulishinda (Uk. 181).

Wakati LiMioe alipochaguliwa ilisemekana kuwa alikuwa ameiba kura. Tetesi baina yake na Amrao zilizuka. Maovu mengi ya viongozi huibuliwa katika hotuba za wanasiasa wenzao wanapofanya kampeni zao. Viongozi hutengeneza majina yao kupitia maovu ya wapinzani wao. Katika hotuba ya LiMioe, inadhihirika kuwa ardhi zilikuwa zimechukuliwa kutoka umma na viongozi. Anasema kuwa, zitatwaliwa na kutaifishwa. Vilevile, anaongeza kuwa, wafanyikazi hao walihitajika kusema jinsi walivyoipata mali waliyonayo la sivyo mali hiyo itaifishwe. Hii ina maana kuwa, wafanyikazi hao walikuwa wamejihusisha na wizi. Ondoro (2021) anasema kuwa wapiga kura wanajuta wanapogundua kuwa walichagua mwizi. Anasema kuwa

wanaoibia nchi yao hukimbilia maabadini na kutoa sadaka kwa lengo la kuficha uovu. Katika maelezo yake, anainisha wizi kivyake. Kulingana na utafiti wetu, wizi ni aina ya ufisadi jambo ambalo linaafiki mhimili wa nadharia ya Udenguzi kuwa hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi.

Katika riwaya ya *watu wa Gehenna* (Olali, 2012) mwandishi ameibua wizi wa aina tofauti. Watu wa Gehenna wanahusishwa na wizi wa magari, kura, dawa hospitalini, kuibia wasanii riziki, wizi wa mitihani, nyumba, bunduki na hata wizi wa pesa. Mwandishi anasema kuwa watu walioweza kuona giza totoro ya Gehenna ni wale ambao hawakuiba kura za wengine (Uk. 3). Muziki walijuta ulioimbwa Gehenna unadhihirisha aina mbalimbali za wizi:

> Wanajuta kuiba dawa za hospitali
> Wanajuta kuwaibia wasanii riziki zao
> Wanajuta kuuza bidhaa bandia
> Wanajuta kuteka nyara watu kwa minajili ya kutaka fidia
> Wanajuta kuiba mitihani
> Wanajuta kuvunja nyumba za watu usiku na kuwaibia pamoja
> na kuwabaka wengine (Uk 8-9).

Muziki huu unadhihirisha kuwa watu wa Kiafra waliiba dawa za hospitali, wakaibia wasanii riziki zao, waliuza bidhaa bandia, waliiba mitihani, walivunja nyumba za watu usiku na kuwaibia. Wanasemekana kufanya mapenzi nje ya ndoa hivyo basi kushiriki katika wizi wa mapenzi. Wizi huhusisha matabaka mawili. Matajiri huiba kwa sababu ya tamaa ilhali maskini huiba ili waweze kumiliki. Pengo kubwa baina ya maskini na matajiri ndilo husukuma maskini kujihusisha katika na wizi. Maskini hufanya hivi ili kupambana na hali yao ya maisha.

Nafsi ya Hikmat inasema kuwa hakuna mtu wa Kiafra ambaye ana uwezo wa kusimama kidete na kutetea wananchi dhidi ya uongozi mbaya. Kulingana na Hikmat,

viongozi ambao wapo ni wale ambao hupora na kusema kuwa wanaiba kwa ari, nguvu na kasi mpya (Uk. 174). Vilevile, anaongeza kuwa, mapenzi yanaelekea kupotea Kiafra. Wasiokuwa nacho pamoja na wengine wenye tamaa wanatumia muda mrefu kuiba, kuumiza na hata kuua watu. Kulingana naye, ni vizuri watu wa Kiafra wazinduke, waendelee na udungu, amani na utulivu ili wasitumbukie kwenye shimo la Gehenna.

Suala la wizi huibuka sababu ya umaskini na watoto kutengwa na familia. Baada ya Baingana na Siyawezi kuachwa na wazazi, waliamua kuacha shule. Baigana alijiunga na kikundi cha watoto wezi, wakamfunza na akawa anaiba na kuleta chakula na mahitaji ya nyumbani. Baingana alimchukua Siyawezi ili awe pamoja nao na baada ya muda, Siyawezi alikuwa bingwa na stadi wa kuiba. Walikuwa wanaleta vitu vya kiajabu wasivyokuwa navyo (Uk. 194). Baadaye, Tokosani na Siyawezi wanatuhumiwa na suala la wizi. Aliazima gari ya mama yake hadi kwa afisa mmoja wa kitengo cha udhibiti wa silaha na kuvunja kisha wakaiba bunduki na makasha mawili ya polisi. Baadaye, anaiba gari ya Yunasi kumuua akiwa na mkewe.

Nchi nyingi hufilisika kwa sababu ya wizi. Viongozi wengi huiba raslimali za nchi na kuifilisisha. Katika Riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), mwandishi anaelezea suala hili kupitia mhusika Munkari. Anasema kuwa, ufisadi ulianza Kiafra baada ya mkutano uliofanyika Mtajuta. Viongozi walitajwa hadharani kuwa wamehusika na vitendo vya ufisadi vilivyochangia Kiafra kufilisika. Anasema kuwa, walikuwa wameiba shilingi bilioni 666 kutoka akaunti ya madeni ya nje katika benki kuu (Uk. 226). Munkari anaendelea kueleza maovu ya Kiafra. Anasema kuwa, maovu ambayo yameshamiri ni matumizi mabaya na wizi wa fedha za serikali na wizi wa mitihani.

Ufisadi unapokuwa sehemu kubwa ya utamaduni kwa jamii, maovu huwa hayaishii kufanywa na watawaliwa bali vitendo hivyo husambaa kwa watawaliwa. Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), Munkari anasema kuwa, watawaliwa walikuwa wameanza kujihusisha na mambo kama wizi na udanganyifu ambayo yalifanywa na watu wenye mamlaka (Uk. 228).

Wizi ukithiri sana nyakati za uchaguzi. Viongozi wengi hujihusisha na suala hili ili kutafuta pesa za uchaguzi. Wanasiasa hutumia vijana kufanya maovu haya. Munkari anasema kuwa viongozi wa Kiafra walitafuta pesa za uchaguzi kwa njia ya wizi. Wizi ulikithiri katika maduka makubwa ya bidhaa, maduka yanayoendesha biashara ya fedha, vituo vya mafuta na mikahawa na baa. (Uk232).

### 2.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza muhtasari na sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012*)* na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Mtafiti ameongozwa na nadharia ya Udenguzi kuchambua sura hizo. Mtafiti amebainisha kuwa kuna aina mbalimbali za ufisadi kama vile ubadhirifu, hongo, ulaghai na kadhalika. Akielezea ubadhirifu,amebainisha jinsi viongozi hutumia raslimali za nchi kama vile ofisi na mamlaka.Viongozi wengine pia ukatalia mamlakani na kujenga mandhari ya ofisi zao kama za kuogofya kama vile Maotad kiongozi wa sayari ya NUKA.Vile vile anateua viongozi wasiokuwa na sifa za uongozi ili kujinufaisha.Unyanyasaji umebainika pia ambapo wasiomuunga mkono Maotad wanapigwa na kudhulumiwa.Wengine wanakamatwa kwa makosa wasiyofanya.Wengine pia wananyanyaswa kwa kunyimwa haki ya kijitetea kama vile Sikujua.Watu wanalipwa hili kupiga kura.Wanapewa zawadi ndogo ndogo kama hongo ya kuwapigia viongozi kura.Wanaohusika katika kashfa mbalimbali wanaachiliwa kwa sababu ya hongo na kesi kuwaendea maskini.Viongozi tofauti wamewalaghai wananchi kwa kutolipa kodi.Viongozi wa sayari ya NUKA

wanatoa bajeti hewa.Viongozi waliuza bidhaa bandia,kuuza viwiliwili vya albino na kuongeza bei ya bidhaa.Baadhi ya viongozi kama Avad mfuasi wa LiMioe anawekeza pesa nchi za nje bila kulipa ushuru.Wengine waliwekeza pesa walizopata kwa njia ya hongo.Wengine wanakwepa ulipaji kodi.Waliotozwa kodi ni watu wa tabaka la chini.Mtafiti ameeleza sura tofauti za ufisadi zaidi ya matumizi mabaya ya pesa za umma hivyo kufanikisha nadharia ya uhalisia wa kijamaa kuwa hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi. Sura inayofuata inahusu vyanzo mbalimbali vya ufisadi.

# SURA YA TATU

# VYANZO VYA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA *MAFAMBA* NA *WATU WA GEHENNA*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura iliyopita mtafiti amejadili muhtasari pamoja na sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012). Mtafiti ameeleza jinsi ufisadi unavyojitokeza kwa njia tofauti zaidi ya matumizi mabaya ya pesa za umma. Baadhi ya sura ambazo zimebainishwa ni kama vile; ubadhirifu, wizi, hongo, kutolipa kodi, na kadhalika. Mtafiti aliongozwa na nadharia ya Udenguzi kubainisha sura za ufisadi. Katika sura inayofuata mtafiti ameeleza vyanzo tofauti vya ufisadi katika riwaya teule kwa kuongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

## 3.2 Vyanzo vya Ufisadi Katika Riwaya za *Mafamba* na W*atu wa Gehenna*

Njoroge (2014) anasema kuwa, umaskini ndicho chanzo kikuu cha ufisadi. Vilevile, kulingana naye ukosefu wa desturi ni chanzo kingine cha ufisadi miongoni mwa viongozi. Wanasema kuwa, viongozi huozeshwa kwa urahisi kwa sababu wao sio warithi wa desturi za hifadhi za majukumu ya umma. Mbali na umaskini na ukosefu wa viongozi wa sifa nzuri, wanaamini kuwa ufisadi husababishwa na ukarimu wa kupeana zawadi, uzembe, uchangukaji wa thamani za desturi na kiwango cha maadili ambao kwa bahati mbaya haujafidiwa kwa njia mwafaka.

Ufisadi umekuwa kama saratani ulimwenguni na hata nchini Kenya.Shida kubwa iko kwetu wananchi. Wananchi wengi huchagua viongozi kwa misingi ya pesa.Kura zimegeuzwa kama biashara.Ili kufunika uovu huu tume za mara kwa mara zimeanzishwa na viongozi  kupigana na ufisadi huku tume hizi zikitumiwa kama hifadhi za wafisadi.Haiwezekani kabisa viongozi wafisadi kupigana na ufisadi. Wananchi hivyo basi wanapaswa kujukumika kuteua viongozi bora bila hongo.

Kuna vyanzo tofauti vya ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Baadhi ya vyanzo hivyo ni kama vile, umimi, utovu wa maadili, ushindani wa kupata madaraka, migogoro, mapendeleo, tamaa na udhaifu wa sheria. Viongozi wengi huendeleza ufisadi kwa sababu ya ubinafsi. Wao hutaka kujilimbikizia vitu bila kujali wengine. Suala hili la umimi ndio chanzo kikuu cha umaskini na utabaka. Wenye mali huzidi kuwa na mali ila maskini huendelea kukosa. Wao hutafuta raslimali kwa njia zozote zile bora wamiliki bila kujali wengine. Baadhi ya watu wa tabaka la chini ambao huendeleza ufisadi hufanya hivyo kwa sababu ya umaskini. Maskini hulazimika kufanya chochote kile ili kupata alichotaka. Jambo hili wakati mwingi husababisha maskini kukandamizwa na kudhalilishwa hasa na walio nacho hivyo kufanikisha nadharia ya uhalisia wa kijamaa inayohusu wahusika kitabaka. Kulingana na nadharia hii wahusika hujigawa katika makundi mawili ambayo ni tabaka la juu na la chini jambo ambalo usababisha ufisadi. Tabaka la juu unyanyasa tabaka la chini. Vyanzo vya ufisadi ni kama vile;

### 3.2.1 Umimi Katika Jamii

Kwa mujibu wa Ochenja (2008) ubinafsi ni jambo la kawaida katika ofisi nyingi za umma. Anatoa mfano wa askari ambao wana ubinafsi wa kutumia lugha isiyofaa. Wanahitaji kulinda sheria lakini wanazivunja. Anaongeza kuwa, wahusika wengi hujifikiria tu bila kujali shida za wengine. Wao huthamini mali kuliko uhai na utu.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), ufisadi umesababishwa na umimi hasa wa viongozi. Kwanza kabisa, mwandishi anasema kuwa raslimali za nchi zilibinafsishwa kwa mlango wa nyuma. Pia, anasema ugavi wa mali ulikuwa kwa msingi wa kigogo gani uliyefahamu. Viongozi walifaidika na hivyo kusababisha matabaka. Vilevile, walisababisha umaskini ambapo wanasayari waliamua kuamka na kutafuta ukombozi kwa njia ya upigaji kura (Uk. 243). Ukombozi huu unaafikiana na mhimili wa nadharia

ya uhalisia wa kijamaa kuwa wahusika wake hudhihirishwa kama wahusika wanaonuia kubadilisha hali yao ya maisha na kunuia kumiliki njia kuu za uzalishaji mali.

Kuna wahusika ambao ni wabinafsi hadi kwa watoto wao ili watajirike hasa katika utoaji kafara. Shanata anataka kujitajirisha kupitia mtoto wake. Mwandishi anaeleza namna uvumi ulivyovuma kuwa Shanata aliweka mkataba na fundi mmoja kila mwaka na kuwatoa kafara watoto wake. Shanata alifanya jambo hili ili ajitajirishe ghafla (Uk. 13). Viongozi wengi hufanya uovu huu hasa wakati wa siasa unapowadia. Kwa sababu ya umimi, viongozi hutoa watu tofauti kafara kwa mfano, watoto na walemavu kama vile albino ili wapate ushindi. Hili ni jambo ambalo husababisha uongozi mbaya.

Vyombo vya habari vimeishi kutangaza visa vingi vya viongozi wafisadi. Uvumi ulienea katika vyombo vya habari kuhusu unyakuzi wa mashamba, mito, maziwa, nyumba na barabara. Walinda usalama walisemekana kunajisi wanawake na wasichana wadogo hata wakati wa mchana. Ekari nyingi za misitu zilinyakuliwa na kasri za ajabu kujengwa humo na mbao kuuzwa na hela hizo kupelekwa katika sayari ya mbali bila kulipa ushuru wowote. Viongozi walioshiriki ukataji miti hawakukamatwa ila maskini kama Sikujua kutoka mtaa wa Bikereni- Msiige ndio walikamatwa. Viongozi walitoa hongo ili kesi zao kusitishwa (uk. 173-174). Viongozi hunyakua raslimali za nchi kwa sababu ya ubinafsi. Huwa wana nia ya kumiliki mali zaidi ya waliyonayo bila kujali watu wa tabaka la chini. Matajiri hawa hukosa utu hata kuishia kupokonya maskini ardhi zao. Huwa hawatosheki. Wanataka kumiliki zaidi na zaidi.

Maotad ni mbinafsi. Maotad alikuwa kiongozi wa Sayari ya NUKA. Mwandishi anasema kuwa wakati LiMioe alipopata ajali, gari lake lilisemekana kuruka juu na kufululiza hadi gofu lililoachwa na mwenyewe baada ya kupokonywa shamba na utawala wa Maotad (Uk. 170). Kumekuwa na visa vingi katika tume ya kupambana na

ufisadi dhidi ya upokonyaji. Viongozi wengi wametuhumiwa na makosa haya ya upokonyaji hasa dhidi ya maskini. Ardhi za umma zimenyakuliwa. Watu wameuliwa ili kuficha ukweli wa maovu haya. Wengi wao hukamatwa na kuachiliwa. Kesi huisha vivyo hivyo. Hongo hutembea na kunyamazisha malalamishi hayo. Vilevile, Maotad anamteua U atawale baada ya kuondoka mamlakani ili ajifaidi kupitia kwake. Anampendelea U si kuwa alikuwa kiongozi bora ila alitaka ajinufaishe kutokana na uongozi wake.

> "Vipi U anataka Maotad ambaye hana haja kwenda choo kwa niaba yake? Vipi? Labda Maotad ana haja. Pengine hana." (Uk.167).

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), umimi umejitokeza kwa njia tofauti. Mwandishi anaibua suala hili kupitia fikra za Bi. Saeeda Khan. Mandhari katika akili ya Bi. Saeeda Khan ni Gehenna. Kuna wahusika wawili katika mchezo huo. Kuna Munkari ambaye ndiye hakimu wa Gehenna na Nyamaume. Wanazungumza na kutoa hukumu kuhusu ufisadi wa Watu wa Gehenna. Mhadhara wa mchezo unaitwa *The Matrix of Corruption.* Munkari katika mchezo huo anadhihirisha ubinafsi wa viongozi ambao usababisha ufisadi. Sereti (2016) anasema kuwa ubinafsi husababisha viongozi kuanguka. Anaeleza jinsi viongozi hujilimbikizia mali sababu ya ubinafsi. Kulingana naye, viongozi wengi hunyakua ardhi ya umma kwa sababu ya ubinafsi. Kitendo hiki husababisha hali ya kutoaminika na tuhuma zinazowaondoa mamlakani hivyo kusababisha uongozi mbaya. Anasema kuwa, mwamko wa kisiasa miongoni mwa vijana husababishwa na ubinafsi wa viongozi. Katika mchezo wa *The matrix of Coruption,* Munkari anasema kuwa ufisadi ni tatizo linalohusishwa na uongozi wa nchi. Anasema kuwa, dawa ya ufisadi itapatikana endapo wanasiasa wataweka pembeni maslahi yao binafsi na ya vyama vyao na kujali zaidi maslahi ya taifa (Uk. 223). Hii inadhihirisha ubinafsi wa viongozi ambao unaelezewa na nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa wahusika huendeleza utabaka kimaksudi licha ya kuwa wanasawiri

matukio ya kihistoria. Vilevile, Munkari anasema kuwa, hamna viongozi wa kisiasa ambao wanaweza kujitoa mhanga kuona kuwa demokrasia ya vyama vingi vya vya kisiasa inaimarika na kustawi vizuri katika Kiafra kwa sababu watu wa Kiafra hasa wanasiasa ni wabinafsi. Nafasi wanazopata ujifikiria wao kwanza (Uk. 224).

Katika mchezo huo wa *The Matrix of corruption*, Nyamaume alimudadisi Munkari na kutaka kujua kwa nini watu wa Kiafra walishiriki ufisadi. Munkari alimjibu kuwa ufisadi hufanywa kwa ajili ya wahusika kujinufaisha binafsi kiuchumi na kuwawezesha kubaki madarakani kwa gharama yoyote ile hata kama kwa kufanya hivyo kutaathiri mfumo wa Demonkrasia (Uk. 225). Munkari pia anaeleza kuwa kuna aina mbalimbali za ufisadi na hutokana na tabia ya viongozi wa ngazi za juu kutojali maadili ya kazi. Anasema kuwa, viongozi hao hujali urafiki na undugu kuliko maadili na yote hutokana na umimi au ubinafsi.

> …. Wanajali zaidi urafiki na ungugu kuliko maadili yote haya ni matokeo ya ule ubinafsi. Ule umimi (Uk. 225).

Vilivile, Munkari anasema kuwa wenye uchu wa madaraka hutengeneza jambo ambalo litazusha mjadala unaoleta mgawanyiko na pengine chuki kati ya makundi ya jamii husika kutokana na imani za dini, mila na desturi, jinsia, rangi au ukabila. Jambo hili husababishwa na wanasiasa wenye ubinafsi (Uk. 238). Munkari anasema kuwa, ufisadi ungekumba Kiafra endapo chama tawala kwa wakati husika hasa viongozi walijali Zaidi maslahi yao binafsi na ya chama chao kuliko maslahi ya Kiafra (Uk. 229). Nyamaume anamjibu kwa kusema kuwa jambo hilo lilitendeka kwa sababu ya kukosa utaifa, elimu na uraia na kuwaandaa vijana kuwa viongozi wa kesho.

Nasimiyu (2016) anaeleza ubinafsi kama ulivyojitokeza katika Uchumi wa kikoloni. Anaongeza kuwa, mambo muhimu yaliyotakiwa yatekelezwe hayakutekelezwa

kutokana na kujisahau, ubinafsi na mfumo wa kibepari usiojali utu. Anaelezea kuwa ubepari uliandamana na ulimbikizaji wa mali kwa kuwanyonya waliozalisha mali hiyo. Anasema mtu akiongozwa na ubinafsi hajali hata haki za wanyonge.

Katika mjadala wa Akilimali na Krockoff kuhusu siasa za katiba pendekezo unadhihirisha ubinafsi. Krockoff anasema kuwa, kilichotakiwa ni kujenga taasisi badala ya kujenga watu wachache wanaoanzisha vyama kwa ajili ya shida zao badala ya shida za wananchi. Anamuambia Akilimali kuwa watu walipaswa kuacha ukale wa kuwaamini na kuwaabudia wanasiasa, kwa kuwa wangewahangaisha bure. Anasema kuwa, viongozi hutumia uongozi wao vibaya na kukatalia mamlakani kwa sababu ya ubinafsi. Akilimali anamwambia kuwa suluhisho la viongozi wabinafsi ilikuwa kujenga na kuanzisha vyama (Uk. 53-55) na kufanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa binadamu huwa na matumaini juu ya maisha ya binadamu na kuelezea jinsi atakuwa mshindi dhidi ya unyanyasaji wa aina yoyote.

Hikmat katika nafsi ya Baingana anaeleza namna viongozi hujipendelea kwa sababu ya ubinafsi. Anasema kuwa, wao huunga mkono kitu fulani leo na kukipinga kesho ikiwa kitaonekana hakiwapi unafuu au maslahi fulani japo ni maumivu kwa wengine. Anasema kuwa, wanakuwa hawana msimamo jambo ambalo anasema wazungu huita *double standards* (Uk. 207).

### 3.2.2 Tamaa

Sereti (2016) anaeleza tamaa kama hamu ya kupata kitu. Anaeleza namna tamaa husababisha viongozi kunyakua ardhi ya umma. Kulingana na Omoga (2018), tamaa husababisha viongozi wenye dhuluma. Wanadamu hukandamizwa na wenzao kwa kuzingatia maslahi yao binafsi kwa sababu ya tamaa.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali 2012) Maotad kiongozi wa utawala wa NUKA ameongozwa na tamaa. Mwandishi anasema kuwa, alikuwa maarufu wa kupendwa na wale haja zao zilikidhiwa na kutimizwa. Kuna wale ambao haja zao zilinyimwa kama Arijojo. Haja zao zilikuwa maji matamu (uongozi). Maotad na wapinzani wake walikuwa na tamaa ya uongozi (Uk. 3-4). Maotad na viongozi wengine wanatumia mamlaka yao vibaya kukatalia mamlakani. Mwandishi anasema kuwa, kila mara waliposema wanatoka hakika walitoka lakini hawakuenda walienda lakini ungeliwaona tena. Hii ina maana kuwa, tamaa ya uongozi ilikuwa imewakwamilia na kushindwa kugura uongozini (Uk. 14).

Suala la hongo hujitokeza kwa sababu ya tamaa. Magazeti yalichapisha habari kuhusu hongo katika utawala wa NUKA. Mwandishi anasema;

> Over 2000 firms in bribe scam companies paid $ 1.8 bn to SAHU regime
> Under the oil-for food deal (Uk. 112).

Vilevile, kuliibuka sakata ya *Mfuko wa vito* na sakata ya *Anglo lasting.* Hizi ni sakata ambazo zilihusisha hongo. Madhara ya Sakata hizi ilikuwa ni umaskini. Sakata ya Anglolasting ilihusishwa na Engineer ambaye aliifadhi pesa katika sayari moja ya nje. Kampuni iliyohusishwa na sakata hiyo haikujulikana. Engineer anajihusisha na sakata hii kwa sababu ya tamaa ya pesa.

Maotad alimuita Avad ofisini mwake ili kumlazimisha kugura BORA. Anamfanyia dhuluma pale ofisini mwake. Anachapwa na kushauriwa ahame BORA. Avad anatuhumiwa kwa kosa la matumizi mabaya ya pesa za umma kwa sababu ya tamaa. Maotad anamwambia Avad kuwa kile alichokuwa nacho ni sababu ya ufisadi. Anamhusisha na kosa la kutoa hongo. Anamueleza jinsi alivyokuwa na tamaa na kujilimbikizia magari, mashamba, nyumba na kuwekeza sayari nyingine. Hii ilitokana

na tamaa (Uk. 153-154). Mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa wahusika huendeleza utabaka kimaksudi licha ya kuwa wanasawiri matukio ya kihistoria ulifaa utafiti kwa kuwa Avad anampinga Maotad.Avad anajifungata kimasombo kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi kama Maotad.

Tamaa ya mali husababisha watu kupata mali isiyo halali. Katika hotuba ya LiMioe kwa wakazi wa Bikerani- Msiige, wafanyikazi wote akiwa mmoja wao, watahitajika kuelezea walivyopata mali waliyo nayo la sivyo mali hiyo itaifishwe. Anasema kuwa, umangimeza katika ofisi za serikali ni haramu na yeyote angepatikana akiendeleza umangimeza kwa sababu ya mlungula, angekuwa anaendeleza ufisadi ambao ulikuwa haramu kuanzia wakati huo (Uk. 183-184).

Tamaa ya viongozi inadhihirishwa na vyombo vya habari. Walinda usalama wanadhihirishwa kuwa wenye tamaa ambapo ilitangazwa kuwa waliua watu usiku, kuvunja mabenki na kuiba magari. Wanaonekena kuwa na tamaa ya mapenzi ambapo waliwanajisi wanawake na wasichana wadogo hasa wakati wa mchana. Viongozi wananyakua misitu kujenga kasri za ajabu. Mbao za bei ghali zinatoka huko na zinapouzwa pesa zilipelekwa katika sayari za mbali bila kulipa ushuru wowote. Kinyume ni kuwa, matajiri wanaoshiriki katika kosa hilo la jinai hawakamatwi. Maskini kama vile Sikujua ndio waliokamatwa. Sikujua haelewi mbona amekamatwa ilhali waliojihusisha na kosa hilo walikuwa huru. Ni wazi kuwa, walikuwa wamehongana ili kesi zitupiliwe mbali. Uhalifu huu wa ukataji miti, ubakaji, wizi, hongo na kuwekeza nchi za nje unajitokeza kwa sababu ya tamaa.

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) ufisadi unaibuka kwa sababu ya tamaa. Munkari katika fikra za Bi. Saeeda Khan anaeleza jinsi viongozi walivyokosa maadili kwa sababu ya tamaa. Anasema kuwa kulikuwa kumezuka mitindo mingi ya

watu ya kujipatia fedha haramu. Wanyonge waliporwa mali yao hasa ardhi kwa kisingizio cha uwekezaji. Magogo na pembe za ndovu ziliporwa kiholelaholela na wanyonge kukosa haki mbele ya vyombo vya sheria. Nyamaume anamkata kauli Munkari na kusema kuwa walifanya hivyo kwa sababu ya tamaa ya mali au utajiri wa haraka (Uk. 227).

Mwandishi anadhihirisha tamaa ya mawaziri katika serikali za Kaunti. Anasema kuwa, bajeti na miundo misingi hugawanywa kwa upendeleo. Wachache wanaofaidika katika serikali hizo ni mawaziri au wale ambao wana ushawishi. Mawazo haya yanajitokeza katika fikra za Hikmat. Anasema kuwa, viongozi wanapaswa kuacha tamaa na kuelekeza nguvu kwa watu. Katika fikra za Hikmat, anasema kuwa viongozi wanapaswa kuacha tamaa na kuelekeza nguvu kwa watu katika maeneo yote. Hikmat anaelezea suala la rushwa ambalo ndilo chanzo kikubwa cha umaskini. Waliopata pesa kwa njia ya rushwa huziifadhi pesa hizo katika nchi tajiri. Hikmat anasema kuwa dunia inapoteza kiasi cha dola zisizopungua trilioni moja kwa mwaka kutokana na rushwa. Suala hili la rushwa na matumizi mabaya ya pesa husababishwa na tamaa ya viongozi (Uk.179) ambapo kulingana na nadharia ya uhalisia wa kijamaa viongozi hutekeleza matendo yao kitabaka kimaksudi au bila kufahamu.

Katika nafsi ya Hikmat, mapenzi yanaelekea kupotea. Anasema kuwa wasiokuwa nacho pamoja na wenye tamaa na roho ya kikatili wanatumia muda mrefu kuiba, kuumiza na hata kuua watu. Anataka watu wa Kiafra waendelee na udungu na upendo katika amani na utulivu kwa kuunganishwa na umoja. Hii ina maana kuwa watu wamekosa utu na kudhulumu wengine kwa sababu ya tamaa. Hikmat anasema;

> Wasiokuwa nacho, pamoja na wengine wenye tamaa na roho za kikatili. Wanatumia muda mrefu kuiba, kuumiza na hata kuua watu (Uk. 178).

Tamaa ya viongozi husukuma viongozi wengi kufanya lolote lile bora wapate cheo wanachohitaji. Munkari katika fikra za Bi. Saeeda-Khan anadhihirisha suala hili. Anasema kuwa, pesa za kutafuta ushindi hutafutwa kwa njia chafu. Ikiwa ni pamoja na kuunda mitandao ya ujambazi ambayo huendesha wizi kokote kule kunakoweza kupatikana fedha. Anasema kuwa, maovu haya yatakoma ikiwa watu wa Kiafra watakuwa jasiri na kusimama imara bila kugawanyika na kuhakikisha waliohusika au chama kilichohusika kimejibishwa kabla ya maovu hayo kusambaa na kuigwa na vyama vingine vikubwa (Uk. 230-233) hivyo basi, mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa kuwa wahusika hunuia kubadilisha hali yao ya maisha unafanikisha utafiti huu

Tamaa inasababisha viongozi wa dini kupatikana kwenye patashika za *sex scandal* kama inavyojitokeza katika fikra za Hikmat. Gazeti la *Itaenea Times* linatoa habari kuwa kasisi Taabu ambaye alihamishwa hadi parokia ya St. Reficul (Uk. 226). Kwingineko, Kasisi Taabu anashtumiwa vikali kwa tuhuma za kumdhalilisha kijinsia binti mmoja katika madhabahu ya kanisa.

> Twende chumba cha kubadilisha Joho. Let’s have sex in the pulpit (Uk. 253).

Faki Nahodha alieleza kuwa Kasisi Taabu alikubali kuwa uhusiano wa kimapenzi na Kinaya. Anasema kuwa, Kinaya alikua uchi wa mnyama akipiga kelele huku akidai kuwa kasisi alimyanyasa kijinsia alipokuwa padre huko chuo kikuu cha Kuhisika (Uk2. 54).

Tokosani anadhihirisha suala hili la tamaa ya mapenzi. Anapokutana na Sikujua, Tokosani anadhihirisha tamaa ya wanaume kwa wanawake. Anasema kuwa, wanaume hudanganya wanawake kila siku na kuishia kuwatusi na kuwaita malaya. Anasema kuwa, alijua alimpenda kwa kuwa hakumjua na endapo angemjua, angemuacha.

Sikujua alimpasha Tokosani kuwa alimpenda. Tokosani alicheka sana na kumwambia kuwa alimlaghai kwa mapenzi. Ulaghai wa kimapenzi husababishwa na tamaa (Uk. 45-46). Vilevile, wenye tamaa ya mapenzi wanatumia dawa za kuongeza nguvu za kiume zinazotokana na wachawi ili kuwawezesha kufanya mapenzi kwa muda mrefu na mtu asiye mume au mke wake. Pia, wanawake wanatengeneza ubikira bandia kwa kutumia dawa zinazotokana na wachawi ili kumfurahisha anayefanya naye uzinzi au mume wake. Huu ni ulaghai, unaosababishwa na tamaa.

Katika nafsi ya Hikmat, wafanyabiashara huwa na tamaa ya pesa. Ngiti (2019) anasema kuwa wahusika wenye tamaa huteseka kwa kuwa wana hamu kubwa ya kupata. Anasema kuwa, tamaa husababisha hasara. Hikmat anadhihirisha jambo hili anaposema kuwa maduka ya kibinafsi ya dawa yamegeuka kuwa karakana ya sumu na hatimaye mauti ya wagonjwa kwa sababu ya wingi wa *fake drugs.* Anasema kuwa, hospitali zinajali zaidi biashara kwa maana ya kuingiza fedha, wenye wanafanya kazi katika hospitali za umma huagiza wagonjwa kununa dawa katika hospitali za kibinafsi (Uk. 177). Daktari hao huelekeza wagonjwa katika hospitali zao. Hikmat anasema kuwa, afya inatisha kwa sababu ya wanataaluma wanaojiingiza kwenye biashara zaidi badala ya kutazama afya za watu. Ulaghai wa aina hii husababishwa na tamaa ya wanabiashara na daktari.

### 3.2.3 Utovu wa Maadili

Maadili ni jumla ya matendo mema au ubinadamu. Musya (2017) Utovu wa maadili ni mienendo isiyoendana na matakwa na matarajio ya wanajamii. Ametoa mifano ya utovu wa maadili kama vile unyanyasaji na ufisadi. Kerre (2020) anasema kuwa, ukuaji wa maadili ni uwezo wa kujenga tabia kutokana na mfumo wa kuamini ili kujua lisilo sahihi na lililo sahihi. Anadhihirisha kuwa, watu hubadilika wakipata pesa ila kilicho

muhimu duniani ni utu. Anasema kuwa, dini na elimu ndizo nguzo kuu za kukomaza maadili ya vijana.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), wakaazi wa mtaa wa Bikerani-Msiige wadhihirisha aina tofauti za utovu wa maadili. Viongozi walihusishwa na masuala ya unyakuzi wa mashamba, nyumba, barabara na misitu. Walinda usalama walisemekana kuwanajisi wanawake na wasichana wadogo, ubakaji ulifanyika hadi mchana. Biashara haramu ya mbao iliendelea. Ekari nyika za misitu zilinyakuliwa na kasri za ajabu kujengwa. Walizoziuza walipeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru wowote (Uk. 173).

Kuna ukosefu wa maadili ya kitaaluma. Viongozi wengi wanaonekana kutumia mamlaka yao vibaya. Wengi wanaenda kinyume na sheria za kitaaluma. Viongozi wanajihusisha na suala la hongo baada ya kufanya uhalifu. Katika hotuba ya LiMioe ni wazi kuwa, majaji walipitisha baadhi ya kesi kwa sababu ya hongo. Ardhi zilikuwa zimenyakuliwa kutoka kwa umma na kutaifishwa. Wengi walikuwa wamepata mali kwa njia isiyo halali. LiMioe anasema kuwa, akiwa kiongozi wafanyakazi watahitajika kusema jinsi walivyoipata mali waliyonayo, la sivyo mali hiyo itaifishwe. Hotuba hii ya LiMioe inafanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa binadamu huwa na matumaini juu ya maisha yake na kuelezea jinsi atakua mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote. Aidha, kuna biashara haramu pia ambazo zinaendelezwa na wenyeji wa Bikerani-Msiige Wanauza vileo hatari. Hii inadhihirika kupitia kwa mzee Tuga Amor. Aliyehusika na uuzaji wa pombe alikamatwa kisha kutoa kitu kidogo na kuachiliwa (Uk. 191).

Vilevile, kuna ukosefu wa maadili kwa viongozi wakati wa kupiga kura. Viongozi wengi hujihusisha katika sakata hii ili kupata ushindi. Ni jambo ambalo husababisha

wageni kutoka sayari nyingine kuingia nchini ili kushuhudia watu wamepiga kura kwa njia ya usalama. Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), viongozi waliiba kura. Mwandishi anasema kuwa waliopata kura kidogo walisemekana kupata kingi na walioshinda walishindwa. Anasema kuwa, mafamba ilibatilisha "ndiyo" kuwa "hapana" na hapana kuwa ndiyo. Tazama mfano ufuatao:

> "Katika miaka ya Anedi, waliopata chakula kidogo walisemekana kupata kingi na wenye kukipata chakula kingi walisemekana kukipata kidogo kwa sababu ya mafamba. Liliposhindwa lilishinda, liliposhinda lilishindwa" (Uk. 181).

Kuna utovu wa maadili ya kitaaluma unaojitokeza katika vyombo vya habari. Taarifa ya habari katika idhaa ya Redio ya Nuka ilisema kuwa Avad alikuwa amegura kundi la Bora na kuhamia NUKA. Zinasema pia, kuwa wakazi wa Bikerani-Msiige waliapa kumuunga mkono U dhidi ya upinzani wa BORA. Habari hizi zilishangaza watu sana. Aliyeshangaa zaidi alikuwa Avad. Alishangaa kuwa hakufanya mahojiano na mtu yeyote. Hakutaka kuiacha BORA. Alilazimishwa na Maotad. Vyombo vya habari hivyo basi vilieneza uvumi tu (Uk. 157). Vilevile, gazeti moja lilieneza uvumi kuwa kura ya maoni ilionyesha U atashinda. Gazeti jingine lilikuwa na kichwa tofauti. Amrao asogea kumpa LiMioe ushindi (Uk. 172-173). Mwandishi anasema kuwa vyombo vya habari vilieneza uvumi tu. Hii inaleta dhana ya utovu wa maadili ya kitaaluma.

Katika riwaya ya *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012), kuna wimbo ulioitwa Walijuta ambao unadhihirisha ukosefu wa maadili kwa njia tofauti. Kuna kunajisi wasichana, kuiba dawa hosipitali, kupokea rushwa, kwenda kwa wapiga ramli, kubeba vibiritingoma barabarani, kuua, kusambaza ukimwi kimaksudi, kuuza viwiliwili vya albino, kulawiti watoto kwenye mtandao, kuavya mimba, walimu kulala na wanafunzi, kufanya uzinzi, bidhaa bandia, utekaji nyara, kuabudu shetani na pesa, kuiba mitihani,

ndoa ya jinsia moja, ubakaji, mapenzi nje ya ndoa na kupunja wafanyikazi (Uk. 8-9). Masuala haya yanaibua utovu wa maadili kama chanzo cha ufisadi.

Wanabiashara wanauza bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Mazungumzo baina ya Nahodha na Baadayadhiki yanadhihirisha hili. Faki anasema kuwa huko Al Jazeera bidhaa ambazo hazifai ziliuzwa. Alisema kuwa wenye maduka walitoa hongo kwa Afisa mwezeshaji wa Bodi ya chakula, dawa na vipodozi. Anasema kuwa huko kulikuwa kukiuka masharti ya leseni na haki za binadamu (Uk. 78-79).

Wizi ni utovu wa maadili ambao unadhihirika katika riwaya wa *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Kuna wizi wa dawa hosipitalini, wizi wa mitihani, wizi wa gari, bunduki, maduka na wizi wa riziki za wasanii (Uk. 8-9). Baada ya Baingana kuachwa na wazazi wake, alianza wizi ili kuleta chakula nyumbani. Baadaye alimuingiza siyawezi katika wizi. Siyawezi anatiwa jela na baadaye alitoka akiwa msichana aliyebadilika. Hii ina maana kuwa, sheria ni muhimu kwani inasaidia kubadilisha tabia (Uk. 194). Wahusika tofauti ambao wanajihusisha na wizi ni Tokosani. Gari ya Yunasi ilikuwa imeibiwa kisha yeye na mkewe kuuliwa. Tokosani pia alikuwa ameiba bunduki katika kitengo cha udhibiti wa silaha kwa kukivunja na kisha kuiba bunduki. Watu hawa wote Tokosani na Sikijua waliwekwa rumande. Tokosani alikiri kuwa walikuwa watumishi wa shetani (Uk. 214-216).

Munkari katika fikra za Bi. Saeeda Khan anadhihirisha aina tofauti za wizi. Anasema kuwa, neno ufisadi lilianza Kiafra baada ya mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Mtajuta ambapo viongozi kadhaa walitajwa hadharani kwamba wamehusika na vitendo vya ufisadi vilivyohusiana na wizi wa shilingi bilioni 666 kutoka akaunti ya madeni ya nje katika benki kuu. Vilevile, Munkari anasema kuwa wizi wa mitihani ni miongoni mwa maovu yaliyoshamiri Kiafra (Uk. 226-227). Katika nafsi ya Hikmat

watu huiba kwa sababu ya ukosefu wa maadili ya utu. Anasema kuwa, vyama vya siasa huongozwa na binadamu ambao hawakuwa wakiiba eti kwa kuwa wao ni wanachama wa umma. Waliiba kwa kuwa wao ni wanadamu ambao hawana maadili na utu (Uk. 266).

### 3.2.4.Ushindani wa Kupata Madaraka.

Kwa mujibu wa katiba ya Kenya (2010) ni haki ya kila mwananchi kuteua viongozi wanaostahili bila kushurutishwa. Uchaguzi unapaswa kuwa wa haki na huru. Ongarora (2020) anaeleza kuwa marais wengi katika nchi za Afrika uongoza kwa kutumia nguvu na mamlaka kupita kiasi. Huwa wanakataa kung'atuka mamlakani zamu zao zinapokwisha hata kama wananchi wanataka mabadiliko. Anasema kuwa madhara ya kukatalia mamlakani ni mauaji na mapinduzi ya serikali.

katika riwaya ya *Mafamba (*Olali, 2012) kuna wahusika tofauti wanaonyanyaswa na viongozi. Viongozi wanawanyanyasa ili kuwanyamazisha na kutaka kuendelea kutawala kwa vyovyote vile. Kuna wahusika ambao walinyanyaswa na Maotad kama vile Amrao, Mastaji, kojo, waliotoa hotuba huko Come -K na Avad. Amrao alitiwa jela kwa miaka 30 kwa kuwa alitaka kumwaga mchanga kwa kitumbua. Haja ya Amrao ni kuondoa Maotad katika utawala wa NUKA jambo ambalo linaafikiana na mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa haja ya mafukara wa ulimwengu ni kuimarisha udikteta wa makabwela. Amrao anatendewa ukahini huu na Maoted alifikiria kuwa Amrao angemnyang'anya mamlaka (Uk. 24-25). Kundi la U linamkatakata vipande mzee mmoja na wanawe kwa sababu ya kutounga mkono upande wa U. Unyanyasaji huu unaibuka kwa sababu ya kutaka kupata mamlaka.

> …Siku moja walikuja wafuasi wa U na kumkata vipande vipande mzee mmoja na wanawe kwa sababu ya kutoungana na upande wao na badala yake kumfuata Amrao. Ndimi za wafuasi wa Amrao zilikatwa na sehemu zao za siri kuchopolewa na kukaangwa na wafuasi wa U (Uk. 99).

Viongozi wanaushindani wa kupata madaraka hadi wanaiba kura. Mwandishi anasema kuwa, waliosemekana kupata chakula kingi walisemekana kupata kidogo kwa sababu ya mafamba. Liliposhindwa lilishinda liliposhinda lilishindwa. Ufisadi ulibatilisha ndiyo kuwa hapana na hapana kuwa ndiyo (Uk. 181). Viongozi pia waliwazawadi wapiga kura ili wawapigie kura. Tunapata kuwa kundi na Mumbi lilianza na kuzawadi watu wa maeneo mbalimbali. Wale ambao zamani walikuwa masikini walianza kuwa matajiri. Wote ambao walimwimbia ndege Mumbi walikuwa matajiri mara moja na kuahidiwa vitafunaji katika kipindi cha majuma mawili tu, maeneo mabilimbali ya sayari ya Bora yalizawadiwa (Uk. 228). Zawadi hizi zilitolewa ili viongozi wapigiwe kura.

Viongozi wana ushindani wa kupata madaraka hadi wanakatalia katika uongozi. Viongozi pia wanawanyanyasa wote waliowapinga. Wakaazi wa Bikerani-Msiige wanampa Maotad jina aende kwa kuwa hawakutaka uongozi wake. Maotad aliwajibu kuwa haendi. `Siendi! Siendi! Ziliwahamasisha baadhi ya wenyeji wa sayari ya Waka. Maotad alijiona kuwa ni kijana sana. Mwandishi anasema kuwa, alijihisi kama shababi na alizidi kusema haendi haendi. Ansema alitawala miaka 720 tu ilhali wengine walitawala miaka 1440. Anasema kuwa ni nusu tu ya 1440. Mwandishi anasema kuwa Maotad hakujua ni kwa nini Arijojo alimtaka aende (Uk. 10).

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) katika fikra za Bi. Saeeda Khan Munkari anaeleza chanzo cha ufisadi kama ushindani wa kupata madaraka. Anasema kuwa kumekuwa na ushindani mkubwa katika suala nzima la kupata madaraka ya kuongoza nchi. Anasema kuwa ushindani si wa vyama bali pia ndani ya vyama

kunakuwa na ushindani unaohusisha makundi na mitandao inayotafuta kwa udi na uvumba kushika madaraka ya Kiafra. Anasema kuwa katika ile hali ya kupata madaraka inawezekana raia au wageni wakawa wenye malengo ya kutumia fedha safi na chafu kufikia malengo yao (Uk. 229).

Munkari anasema kuwa ushindani wa kupata madaraka husababisha chama tawala kung'ang'ania uongozi wa Kiafra kwa ajili ya maslahi binafsi zaidi. Chama hicho kinaweza kuamua kufanya linalowezekana liwe njema au baya, ilimradi kishinde uchaguzi. Anasema kuwa, wakiona wana ushindani mkubwa ambao unahatarisha ushindi wao na wenyewe hawana fedha za kutosha kupata ushindi wanaweza kufanya mbinu za kupata fedha zaidi kwa kushirikiana na baadhi ya viongozi kutenda maovu ili kushinda kwa vyovyote vile (Uk. 230).

Munkari anasema kuwa pesa za kupata ushindi kwa viongozi zilipatikana kwa kuibia taasisi za serikali kama vile mabenki au miradi mikubwa ya umma yenye fedha nyingi. Anasema kuwa pia viongozi hao hutafuta watu ambao watapewa zabuni bandia za serikali ambazo hulipwa fedha mingi kwa kukubaliwa kuwa watamega fungu kubwa la fedha zitakazo rudishwa kifisadi kusaidia chama kupata uchaguzi. Ikiwa ni utamaduni wa chama tawala kushinda, fedha za kutangazwa ushindi huwekwa katika bajeti ya serikali kwa kuingiza miradi hewa au miktaba mibovu. Anasema kuwa, pesa za kutafuta ushindi huwezwa kutafuta kwa kuunda mitandao ya usambazaji ambao huendesha wizi wa kutisha katika shughuli za wananchi kama vile wizi kwenye maduka makubwa ya bidhaa, maduka yanayoendesha biashara ya fedha, vituo vya mafuta, mikahawa na baa, kuvamia ofisi siku za kulipa mishahara na mahali popote ambapo wanaweza kupata fedha (Uk. 231-232).

Akizungumza na Munkari, Nyamaume anasema kuwa viongozi wanaokosa sera zinazohusika huweza kufanya lolote liwezekanalo ili washinde kura na kuendelea kutawala. Nyamaume anasema kuwa ukosefu wa elimu ya uraia kwa wananchi huchangia uchaguzi wa viongozi wabaya. Anasema kuwa viongozi hao huweka mikakati mahususi ikiwa ni pamoja na kuhonga wananchi wa fedha, mavazi, chakula au vitu vidogo kukidhi mahitaji ya fukara, kununua shahada za wapiga kura ili wasiweze kupiga kura, kuwatisha wananchi kupitia vyombo vya dola kuunda vikundi vya kihalifu kuwashambulia na kuwatisha watu. Anasema kuwa, viongozi wanaweza kununua baadhi ya maafisa wa tume ya uchaguzi ili majina ya wapiga kura yavurugwe hasa katika maeneo yenye upinzani mkubwa yasiweze kupiga kura kabisa.

Matumizi mabaya ya mali ya umma husababishwa na ushindani wa kupata madaraka. Munkari katika fikra za Bi Saeeda Khan anasema kuwa ukwapiaji wa mali ya umma kwa malengo ya kiuchumi na kupata madaraka ni kitu ambacho ni chafu kwa jamii na wanaumizwa na ufisadi wa aina hii. Kila mhusika anapaswa kuhakikisha kuwa kila sauti ambayo inaweza kuinuka na kudai uwajibikaji dhidi ya uovu huo watu ambao anaita “whistle blowers” (Uk. 236). Uwajibikaji huo unabainisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa haja ya mafukara kwenye ulimwengu huwa ni kuimarisha udikteta wa makabwela.

Ushindani wa kupata madaraka unasababisha viongozi kunyanyasa albino na unyofoaji wa sehemu za siri za maiti kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti. Hikmat akizungumza na nafsi ya Baingana anasema kuwa taifa lipo vitani dhidi ya mauaji ya albino na ukataji wa sehemu za siri za maiti kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti. Anasema kuwa, viungo vya albino ni njia ya kujipatia utajiri na kupata kura. Anaongeza kuwa, wamewamaliza albino sasa walikuwa wamevamia vyumba vya kuhifadhi maiti kutafuta nyeti za watu.

Anasema kuwa wauaji hao huua albino kupitia maagizo wanayopata kutoka kwa waganga washirikwa. Waganga wa kienyeji huwaambia wateja wao kuwa wakiua albino watatajirika na kufanikiwa katika mambo yao hasa wanaogombea ugavana, ubunge, useneta, udiwani na pia kwenye uchaguzi wa viti hivyo. Jambo analoliita *blackmagic*. Anasema kuwa waganga wa kienyeji wanawapa masharti ya kuua albino ili waweze kusafisha nyota zao. Anasema kuwa ushindi wa viongozi hao huchangiwa na vitisho, nguvu za giza na vitisho vya kishirikina (Uk. 208-209). Njia hii ya kishirikina ya kupata uongozi husababisha dhuluma zao za siri. Uovu huu hufanywa kwa sababu ya ushindani wa kupata madaraka.

### 3.2.5 Migogoro

Wamitila (2003) anasema kuwa migogoro ni mivutano inayokuwa kati ya mhusika mmoja na mwingine katika kazi ya fasihi. Migogoro ni hali ya kukosa kuelewana kwa sababu ya ugomvi. Ufisadi ni janga ambalo husababisha migogoro katika jamii. Dhuluma za kitabaka husababisha migogoro baina ya matabaka. Kulingana na Kausi (2021) migogoro huibuka kwa sababu ya ubaguzi wa rangi. Akielezea ubaguzi wa wakoloni Wazungu kwa Waafrika anasema kuwa, Waafrika waliozalisha mali walipewa mshahara duni. Jambo hili lilisababisha matabaka. Hivyo basi, uongozi mbaya husababisha migogoro baina ya matajiri na maskini.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) kuna migogoro dhidi ya viongozi kwa viongozi na viongozi wa serikali na watu wa tabaka la chini. Sayari ya NUKA inaongozwa na Maotad ambaye anataka kufurushwa kwa sababu ya mafamba. Baadaye anatimuliwa na kundi la BORA ambalo liliongozwa na LiMioe. Migogoro inaibuka baina ya kundi la NUKA na BORA. Baadaye watu wanaerevuka na kuwatia viongozi wao mashakani hivyo kufanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa haja ya mafukara huwa ni kuimarisha udikteta wa makabwela. Scott (2020) anasema

kuwa migogoro usababisha umwagikaji wa damu unaohusisha mauaji na migogoro vilevile uibua maudhui kama dhuluma, tamaa na ukiukaji wa haki.

Kuna mgogoro wa mwana na baba dhidi ya uongozi. Maotad kiongozi wa Sayari ya NUKA anakosana na mwanaye kwa sababu ya urithi. Mwana alitaka kutawala ila baba alitaka kumpa kiti kingine (Uk. 104). Jambo hili linadhihirishwa naye Boyi akizungumza na LiMioe na Fadhila. Anasema kuwa ajabu mwana alikuwa na wafuasi wengi kuliko baba. LiMioe amuunga mkono Boyi na kusema kuwa alichotaka ndicho walichotaka. Anauliza kuwa angekubali wakichukue kiti cha babake ikiwa alijiona kama ndiye mrithi wa kiti kile? LiMioe aliuliza (Uk. 106). Huu ni mgogoro baina ya wanasiasa kwa sababu ya upendeleo wa kinasaba.

Kuna mgogoro wa kundi la NUKA na BORA. Nuka ilitawaliwa na Maotad na hivyo alimteua U aendeleze utawala. U alipigana na LiMioe wa kundi la BORA. Katika hotuba LiMioe anasema kuwa ushindi wa BORA ulikuwa ushindi dhidi ya Mafamba. Anasema kuwa wanyonge walikosa haki. Anasema kuwa NUKA ilinuka sana na kutoa harufu mbaya. Anasema kuwa, hana lengo ya kulipiza kisasi bali kubuni tume za maridhiano na kupata ukweli wa mambo. Anasema kuwa wangeteua viongozi ambao wangesaidia kuitawala sayari ya BORA. Anaeleza kuwa usalama ulikuwa haupo na kuahidi kurudisha usalama. Anadhihirisha jinsi viongozi wa BORA walivyojihusisha na mauti na kusema kuwa angeunda tume za kuchunguza vifo vya watu mbalimbali. Anasema pia, tume ingeundwa kuchunguza ulanguzi na kashfa ya *Mfuko wa vito.* Anahahidi kuchukua ardhi zote zilizokuwa zimenyakuliwa na kuzitaifisha (Uk. 182-183). Mwandishi anasema kuwa, viongozi walifanya mikutano mingi kusuluhisha tofauti zao ila hawakuwa na suluhisho. Kundi moja liliponyamaza lilituhumiwa kula njama (Uk. 186).

Kuna migogoro ya kikabila. Migogoro hii ilisababishwa na upendeleo wa kikabila. Watu wa jamii ya Bikerani-Msiige walikuwa wameapa kuwa kamwe watu wa jamii ya QiQu haingeweza kuitawala sayari ya NUKA mara nyingine. Boyi anasema maneno haya akiwaambia LiMioe na Fadhila ambao pia walitaka kuongoza sayari ya NUKA. Taarifa ya habari katika idhaa ya redio NUKA ilisemekana kuwa Avad alikuwa ameteuliwa kuwa makamu wa Maotad. Alisema kuwa Avad alikuwa amegura BORA na kujiunga na kundi la NUKA kwa sababu viongozi kama Amrao walikuwa wakabila (Uk. 157). Habari hizi zilikuwa za uwongo kwa kuwa, ingawa Avad alikuwa ametishiwa na Maotad hakuwa amekubali kama ilivyotangazwa katika idhaa ya redio ya NUKA.

Kuna migogoro kati ya Maotad na wakazi wengine wa Bikareni-Msiige. Wakaazi wa Bikerani-Msiige walilalamikia viongozi wao hasa kwa sababu ya mafamba. Walisema kuwa mali waliokuwa nayo ilikuwa imetokana na mafamba. Wakereketwa wa Maotad walitunga wimbo kuwa mafamba maendeleo ya sayari, ya NUKA, barabara za sayari ya NUKA zilitokana na mafamba (Uk. 9). Amrao akiwa jela alitunga wimbo wa kukashifu utawala wa Maotad. Alisema alikuwa na wajibu wa kuzitetea haki za wakazi wa sayari zote. Anasema kuwa wajibu wake ulikuwa kukomesha mafamba (Uk. 281). Wimbo huu wa Amrao wa kutetea haki za wakazi unabainisha wahusika wanaonuia kubadilisha hali yao ya maisha basi kufanikisha mhimili wa kwanza wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.Kuna mgogoro ambao unadhihirika katika wimbo wa Maotad ambao ulipendekeza mafamba ila Amrao anaimba wimbo wa kukomesha mafamba hasa hongo na matumizi mabaya ya mali ya umma. Mwandishi anasema kuwa mgogoro kati ya Maotad na Amrao ulisababishwa na falsafa zao kuhusu mafamba. Kwa sababu ya tofauti hizo, Amrao alisukumwa ndani. Maotad alisifia mafamba naye Amrao alikashifu mafamba (Uk. 30).

Katika riwaya ya *watu wa Gehenna* (Olali, 2012) kuna migogoro tofauti kama vile migogoro ya matajiri na wafanyikazi nyumbani, migogoro ya kasisi na washirika, migogoro ya majini na binadamu, Munkari na binadamu, migogoro ya kibinafsi, wanafunzi na wasimamizi wa chuo kikuu na Albino na viongozi. Macharia (2021) anainisha kuwa kuna aina tofauti za migogoro kama vile; migogoro wa kisaikolojia, mapenzi, ndoa, tamaa, ulafi na malezi. Anaongeza kuwa, migogoro inapaswa kusuluhishwa vyema na kwa njia ya kueleweka hivyo kuzingatia nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambayo huzingatia maslahi ya makabwela wenye nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela.

Migogoro ya matajiri na wafanyikazi inaibuliwa naye Bi. Saeeda Khan na Bi. Rebecca Belira. Bi. Saeda anashtakiwa kwa kosa la kusafirisha na kuwaingiza watu nchini Uingereza kwa minajili ya kuwapunja. Mfanyikazi alilalamika kufanya kazi siku saba kwa juma; hakuruhusiwa ale na familia na alikuwa mara nyingi alipewa mkate ale na wakati mwingine, hakupewa chohote. Hakupewa chumba cha kulalia badala yake alipewa kigodoro chembamba na bedishiti na kuambiwa kulala jikoni kwenye sakafu. Hakupewa ruhusa kupata mapumziko wala kuruhusiwa kutoka nje. Katika mwaka wa kwanza alilipwa mshahara kama walivyokubaliana lakini baadaye hela alizopewa kila mwezi zilisimamishwa. Anapolalamika kwa wale waliomtafutia hiyo kazi anaambiwa akome kuitisha pesa na kufanya alivyoamrishwa na Bi. Saeeda Khan. Wazazi wake wanapougua anaitisha hela kwenda kuwajulia hali na kwa mara nyingine hakupewa ruhusa na hivyo wazazi wake walifariki bila kuwatembelea. Baadaye Bi. Mruke anaripoti hosipitalini alivyokuwa akiteswa na Bi. Saeda na madai kurekodiwa na daktari. Chama cha Operesheni puliza vuvuzela (OPV) kiliarifiwa na baadaye polisi kujulishwa. Bi. Mruke alitolewa na polisi pamoja na Operesheni puliza vuvuzela

kutoka nyumbani kwa Bi. Saeeda Khan na kumpangia makazi. Baadaye Bi. Saeeda Khan alitiwa nguvuni kwa shtaka la kuwasafirisha watu na kuwapunja (Uk. 86-88).

Bi. Rebecca Belira pia anapata shitaka kama la Bi. Saeeda Khan. Methodia alikuwa mfanyikazi wa nyumbani. Alifanya kazi kwake Bi. Rebecca huko ng`ambo. Aliletwa kutoka Kenya hadi London kufanya kazi kwa Rebecca ambaye alikuwa mwanafunzi wa shahada ya uzamifu katika utafiti wa matibabu. Mhasiriwa kwenye taarifa yake anadai kuwa, alishawishiwa na kukubali kuwa mtumwa wa nyumbani. Alilalamika kuwa stakabadhi zake za usafiri zilitawaliwa na mwajiri wake. Alikuwa ametiliwa mkwazo kutembea, kutwaliwa kwa mshahara, kudhulumiwa kimwili na kutukanwa na mwajiri wake saa nyingi na kufanya kazi na mwajiri wake, makazi mabaya yaliyotolewa na mwajiri wake na hata kuzuiliwa kuwasiliana na jamii yake na wengine. Methodia aliamua kutoroka baada ya kupewa ushauri na mama mmoja wa shule (Uk. 96-97).

Kuna migogoro baina ya walimu wa dini na washiriki. Kasisi Taabu anatumiwa kudhalilisha washiriki wao kijinsia. Katika mawazo ya Faki Nahodha, Kasisi Taabu anashtumiwa vikali kwa tuhuma za kumdhalilisha kijinsia binti mmoja katika madhabahu ya kanisa.  Anasikia sauti ya taabu;

> "Kinaya nakupenda!"
> "Taabu wewe ni kasisi!"
> "Usijali."
> "Ninajali."
> "Adamu alishindwa kujistahimili. Sembuse mie?"
> "Hapana kasisi Taabu"
> "Njoo hapa!"
> "Lakini…"
> "Lakini nini?"
> "Hapa ni katika madhabahu matakatifu!"
> "Usijali.Hakuna atakaye jua"
> "Twende chumba cha kudalisha joho!"
> "Let`s have sex in the pulpit!"
> "Ok!" (Uk. 253-254)

Faki Nahodha aliona kasisi akikubali kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kinaya alikuwa uchi wa mnyama akipiga kelele huku akidai kunyanyaswa kijinsia na kasisi na kusababisha ufisadi wa kimaadili. Taabu wakati alipokuwa padri huko Chuo kikuu cha Kuhisika. Faki Nahodha anazinduka baada ya tangazo hilo la Munkari. Anapata mlio wa arifa la ujumbe mfupi kutoka parokia alipokuwa anahudumu kasisi Taabu kuwa alikuwa amejitia kitanzi na kufariki katika madhabahu. Faki Nahodha alienda moja kwa moja hadi kwenye parokia. Alipigwa na butwaa baada ya kupata kasisi akinywa chai akisoma gazeti la *TLA tombstone Epitaph*. Gazeti ilisoma;

> Kiafra prosecutors said today
> They had charged a priest
> With raping an underage girl
> After a trip off from a special
> Body set up to combat abuse
> Sandala that have rocked
> The church. The priest so
> Allegedly abused the girl
> Aged 13 at the time
> Over three-year period from 2050
> Telling her she wouldn`t go to heaven if she did not comply (Uk. 256).

Faki Nahodha aliona kasisi akikumbwa na aibu baada ya kufumaniwa na msichana kwa jina Kinaya akiwa na kibiritingoma mwingine. Kasisi alikuwa amefumaniwa na Kinaya aliyekuwa mpenzi wake wakiwa katika mahaba mazito. Akiwa katika madhabahu kasisi Taabu na kibiriti ngoma huyo walikuwa wakinywa divai chapa *Blasted church*. Kasisi na yule kibiritingoma walianza kunywa lakini ghafla akaingia Kinaya. Kinaya alianzisha vurugu kibiritingoma alitoroka na kuacha kasisi akichapwa na Kinaya ambaye baadaye anakimbia na kuokoa maisha yake. Kadhia hii ilifanyika akilini mwa Faki Nahodha alipokuwa amemtembelea kasisi (Uk. 257). Suala hili la unyanyasaji kutoka kwa watumishi wa Mungu limekuwa sugu nchini Kenya na hata kote ulimwenguni. Jambo hili huibua migogoro ambao husababisha watumishi wengine

kufukuzwa kanisani na wengine kuachwa bila wafuasi. Ni jukumu la watu kuwajibika na kuripoti kasisi ambao watahusishwa na maovu haya.

Kuna mgogoro baina ya Munkari na watu wa Gehenna. Mgogoro unaibuka kwa sababu ya maovu wanayoyatenda. Kwanza, mgogoro unaibuka baina ya kasisi Taabu na Munkari. Mgogoro huu unaibuka kwa sababu ya kutokuwa mwaminifu katika kiapo chake cha useja. Kasisi alihusishwa na maovu ya kunyanyasa wasichana kijinsia kama vile Kinaya wakati Taabu alikuwa padre huko chuo kikuu cha Kuhisika (Uk. 254-255). Bi. Saeeda anaona mgogoro baina yake na Munkari katika mawazo yake. Bi. Saeda alijulishwa na Munkari kuwa alienda Gehenna kwa sababu ya maovu aliyotenda duniani (Uk. 222). Bi. Saeda alihusishwa na kosa la kunyanyasa mfanyikazi wake wa nyumbani. Munkari anaeleza chanzo cha ufisadi Kiafra. Hukumu yake kwa watu wa Gehenna ni juu ya ufisadi hasa viongozi. Anasema kuwa, umaskini umeibuka Kiafra kwa sababu ya sera za vyama vya kisiasa, uongozi mbaya na ugonjwa wa ufisadi ambao ulitikisa Kiafra. Anasema ufisadi ni lazima ung'olewe na kulinganisha ufisadi na ugonjwa (Uk. 222). Wahusika katika nadharia ya Uhalisia wa kijamaa huwa wahusika wa kimapinduzi wanaonuia kubadilisha hali ya maisha na wenye nia ya kumiliki njia za kuzalisha mali. Munkari ni mfano mwafaka wa wahusika wa kimapinduzi.

Kuna mgogoro baina ya wahusika wa kiuhalisia na wahusika majini. Sikujua alifanya urafiki na mhusika jinni. Sikujua anamudadisi Tokosani na kumwambia kuwa alihisi alikuwa jini lakini Tokosani hakukubali. Akilini mwa Sikujua, anapelekwa katika chumba kizuri na Tokosani. Anakumbushwa maovu aliyofanya duniani kama kukata miti, kunyakua ardhi, ukabila, kutumia nguvu za giza kupata cheo cha ubunge, kutumia dawa za kuongeza nguvu za kiume, kuhimiza wanawake kutumia dawa za kuongeza ubikira bandia na kadhalika. Anafungwa kitandani na kutandikwa bila huruma (Uk. 60-61).

Migogoro ya kijamii huibuliwa na matatizo mbalimbali ambayo wanajamii hukumbana nayo. Matatizo haya huibuliwa na viongozi wabaya ambao huendeleza maovu kama vile; utabaka, ufisadi, wizi, upokonyaji, hongo, mishahara duni, utozaji wa juu wa ushuru, uchumi kwenda juu miongoni mwa masuala mengine. Okwena (2013) anataja matatizo ya nchi za Kiafrika kama vile ufisadi ambao husababisha migogoro na kuibua kikundi cha upinzani miongoni mwa wakereketwa na wengine. Viongozi hao huibuka kupinga uongozi mbaya kwa njia ya migomo au maandamano. Wananchi hujipigania kupitia malalamishi dhidi ya matatizo hayo.

### 3.2.6 Mapendeleo

Katiba ya Kenya (2010) sura ya 4 inasema kuwa, kila mtu ana haki sawa na mwingine. Wamitila (2003 ) anaeleza upendeleo kama kumpa mtu manufaa zaidi sababu ya sifa zao maalum kama vile jinsia, kabila au hali ya kiuchumi.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) ufisadi umesababishwa na aina tofauti za upendeleo. Kuna aina tofauti za upendeleo kama vile; upendeleo wa kinasaba, kisiasa, kirafiki, kijinsia, kieneo na kadhalika. Yovo (2021) anasema kuwa upendeleo wa watu au makundi ya watu katika nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini Kenya ni mojawapo ya masuala ibuka. Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) upendeleo wa kinasaba unadhihirika katika sayari tofauti na kuzifanya zisambaratike. Mwandishi anasema kuwa sayari zilipogongana sayari moja ya EF ilivunjika jekejeke. Sayari hii iliaminika kuongozwa na aila moja ya Amrao na hii ndiyo ilikuwa sababu ya sayari hii kuvunjika (Uk. 44).

Vilevile, kuna upendeleo wa kisiasa ambapo Maotad alitaka kumpa Amrao kiti ila naye Amrao alitaka kiti tofauti kilicho gharimu pesa nyingi (Uk104). Jambo hili linasababisha matumizi mabaya ya mali ya umma. Vilevile, Amrao anasema kuwa,

Maotad alikuwa kiongozi mbaya ambaye hakujali maslahi ya wanasayari. Alipendwa na wale ambao haja zao zilikidhiwa na kutimizwa. Anasema kuwa wale ambao haja zao zilinyimwa walimwita Aende (Uk. 167). Anapozidi kukataliwa katika sayari ya NUKA, Maotad anamteua rafikiye U atawale ili ajinufaishe (Uk. 173). Anateua kiongozi ambaye hakuwa na sifa haswa za uongozi jambo ambalo wanasayari wa NUKA hawakuunga mkono ila wachache tu.

Korti pia zilipendekeza wengi waliopatikana kwenye uhalifu ila kwa njia ya hongo. Mwandishi anasema kuwa wengi walihusishwa na suala la ukataji miti ingawa wengi waliojihusisha na jambo hilo walikuwa viongozi. Waliotiwa ndani na kukamatwa walikuwa watu wa tabaka la chini kama vile Sikujua. Mwandishi anasema kuwa, Sikujua alishangaa kuona wenye maovu ya ukataji miti njiani wakiwa huru (Uk. 173). Hii ni dhahiri kuwa katika sayari ya NUKA ilitegemea ulijua nani na ulitoa pesa kiasi gani.

Wakaazi wa sayari ya NUKA walimuasi Maotad na kumchagua LiMioe wa kundi la BORA. LiMioe anapochaguliwa wanawapiga kalamu wasaidizi wake wote wa mpinzani wake Amrao (Uk. 238). Chama chake cha Mumbi hakuna aliyetupwa nje ila Engineer. Mwandishi anasema kuwa waliochaguliwa masomo yao hayakuzidi chekechea. Jambo hili lilisababisha uongozi mbaya ambapo walianza kujihusisha na maovu ya ufisadi kwa utawala wa kitambo wa NUKA.

Upendeleo wa aina mbalimbali ndio chanzo kikuu cha aina tofauti za ufisadi kama vile hongo, ukabila, matumizi mabaya ya mali ya umma na unyanyasaji. Katika riwaya ya *watu wa Gehenna* (Olali, 2012), hukumu ya Munkari Gehenna ambayo ni mchezo unaotokea katika mawazo ya Bi. Saeeda Khan, kuna upendeleo wa kidini ambao ulichochewa na wanasiasa (Uk. 227). Wanasiasa waliokuwa na malengo ya kibinafsi

hutengeneza jambo ambalo litazusha mjadala unaoleta mgawanyiko na chuki kati ya makundi ya jamii husika kutokana na imani za kidini, mila na desturi, jinsia, rangi au ukabila (Uk. 238). Katika wimbo watajuta unaoimbwa Gehenna, watajuta kupanda mbegu za ukabila (Uk. 8-9). Upendeleo unasababisha ukabila. Katika ulimwengu wa ndoto, Sikujua yuko naye Tokosani katika chumba kimoja ambapo anakumbushwa kuwa alipokuwa duniani alishiriki katika vita vya ukabila ambapo baadaye anafungwa kitandani na kuanza kutandikwa bila huruma (Uk. 60). Faki Nahodha akihadithiwa na Baadayadhiki hadithi ya kwao, anasema kuwa mahali alipopanga nyumba walikuwa wametishiwa kuhama pale na kurudi kwao. Upendeleo huu unasababisha unyanyasaji kwa wapangaji ambao hawakuwa wa kabila hilo.

Matumizi mabaya ya mali ya umma huibuka kwa sababu ya upendeleo. Katika fikra za Hikmat kwenye kipindi cha *The night of living dead*, katiba mpya ya Kiafra hususan ugatuzi imeruhusu bajeti kugawanywa kwa upendeleo. Anasema kuwa, inawafaidi wachache kwa sababu ni mawaziri au wanaushawishi (Uk. 179). Vilevile, Hikmat akizungumza na nafsi ya Baingana anadhihirisha wanasiasa kama ndumakuwili. Leo watasema hawataki hili kesho watasema wanataka lile. Wanapinga kitu fulani leo kesho wanakiunga mkono kitu hicho kinapoonekana kuwapa unafuu japo ni maumivu kwa wengine (Uk. 207). Ubinafsi huu wa wanasiasa unafanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa wahusika huendeleza utabaka kimaksudi licha ya kuwa wanasawiri matukio ya kihistoria. Katika mjadala baina ya Krockoff na Siyawezi katiba pendelezi lilitakiwa kujenga taasisi badala ya kujenga watu wachache walioanzisha vyama kwa ajili ya shida zao ila si kwa shida za wananchi (Uk. 53). Ubinafsi na tamaa hii ya viongozi ulisababisha ubadhirifu. Vilevile, anasema kwa siasa za Kiafra zinaendeshwa shaghalabaghala. Anasema kuwa, rais anaweza kuongeza muda au

kumrithisha mtoto. Krocoff anairejelea taifa ya Kiafra kama taifa ya kugawiana (Uk. 55).

Hikmat anadhihirisha upendeleo huu wa kinasaba akizungumza na nafsi ya Baingana. Anasema kuwa si vibaya watoto wa wakubwa kuongoza kwa sababu wana haki ya kukua viongozi. Anachopinga kuwa watoto wale hurithishwa kama hawana sifa au uwezo wa uongozi. Analipinga jambo hili kwa sababu linanyima watu fursa ya kupata viongozi bora na kunyima watoto maskini fursa ya uongozi ambao huwa na vipaji vya uongozi (Uk. 210).

Unyanyasaji uibuka mahala ambapo pana upendeleo wa rangi. Mwandishi anaeleza kuwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kuhisika waligoma ili kupinga mfumo wa elimu uliowatweza Waafrika wasomi na kuwakatisha tamaa kwamba wao ni watwana mbele ya mabwana weusi (Uk. 121). Wanafunzi waligoma kuingia darasani kwa majuma kadhaa baada ya kulazimishwa matumizi ya lugha ya Kigehenna katika baadhi ya masomo kwa wanafunzi wa viwango vya juu. Wanafunzi kugoma wanafanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa mafukara huwa na nia ya kuimarisha udikteta wa makabwela. Mwandishi anasema kuwa hiki kilionekana kama kilele cha ubaguzi hivyo hawangeweza kuvumilia. Wanafunzi walibeba mabango yaliyoandikwa:

THE CORRUPT POLITICIAN CREED (Uk. 122).

Badala ya kutafuta suluhisho mwafaka serikali ilitoa vyombo vya dola kutawanya wanafunzi. Walifyatuliwa risasi na kujeruhiwa mmoja akiwa Hikmat. Mali iliharibiwa, nyumba zikachomwa na baadhi ya polisi waliuliwa. Unyanyasaji huu unaibuka kwa sababu ya upendeleo wa kirangi ambao serikali ilipendelea wazungu na elimu yao.

### 3.2.7 Utovu wa Sheria

Mayieka (2015) anaeleza sheria kama kanuni zinazotungwa ili kuratibu shughuli za jumuiya inayohusika pamoja na adhabu pindi kanuni hizi zinapokiukwa. Anasema kuwa, kila nchi ina sheria zake ambazo kila mwananchi anapaswa kujiepusha na mkono mrefu wa sheria. Wenye vyeo hutumia sheria kujilinda na kuwanyanyasa wanyonge. Katiba ya Kenya (2010) Inaeleza kuwa haki za watoto, vijana, wazee, walemavu, wafungwa, wafanyikazi na wakimbizi ambazo zinapaswa kufuatwa na kila mwananchi. Haki hizi zimeweza kuvunjwa na kuibua sura tofauti za ufisadi.

Katika Riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) kuna sheria mbalimbali ambazo hazijafuatwa. Kulingana na tume ya EACC (2018) kila mwananchi anapaswa kulipa ushuru jambo ambalo limethibitishwa na katiba ya Kenya (2010) .Watu ambao hufanya kazi na kupata hela wana jukumu la kulipa kodi. Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) baadhi ya wananchi walidinda kulipa ushuru. Mwandishi anasema kuwa ekari nyingi za misitu zilinyakuliwa na mbao za bei ghali kuuzwa na wenye kuuza walipeleka hela hizo katika sayari ya mbali bila kulipa ushuru wowote (Uk. 173). Vilevile, mzee Twajua wa kijiji cha Tugor Amor katika hadithi yake anasimulia kisa cha ajuza mmoja ambaye hakulipa kodi. Anasema kuwa, aliwaona watoza ushuru kama kupe. Baada ya kulipa ushuru aliwarushia matusi mazito (Uk. 198).

Tume ya EACC (2016) inakashifu utoaji hongo katika sekta yoyote ile. Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), utoaji hongo ulikuwa umekithiri hadi uliibuka katika gazeti moja la BORA. Mwandishi anasema:

> OVER 2000 FIRMS IN BRIBES SCAM COMPANIES paid and 1.8bn to SAHU regime under the oil for food deal (Uk. 211).

Sheria inamkandamiza mwananchi maskini na kupendelea viongozi. Amrao anawekewa lawama ya kumwaga mtama dhidi ya kiongozi Maotad. Kumwaga mtama

ilikuwa kosa la urahisi na malipo ilikuwa kwenda jongomeo kupitia njia ya kitanzi. Kila mtu ana haki ya kuishi hata wafungwa kulingana na katiba ya Kenya (2010). Sheria haikufuatwa kwa sababu wote waliotiwa jela kwa kumwaga mtama waliuliwa kifo kisicho na huruma (Uk. 24-25). Mwandishi anasema kuwa sheria za sayari zote hazikuruhusu watu kujitetea ila katika sayari ya DUNIA. Katika sayari zile ziingine hakuna haki zozote za binadamu zilizoheshimiwa wala kuzingatiwa. Haki zote zilikiukwa. Ambrose(2014) anasema kuwa kila kundi katika jamii lazima lipate haki na ni lazima pawe na sheria na kila mmoja atii sheria. Mwandishi anasema katika sayari ya dunia hakuna aliyefungwa bila kujitetea. Haki ilidumishwa. Waliamini kuwa sayari ya DUNIA kuna siku ingefufuka ingawa hawakujua lini (Uk. 25-26).

Viongozi wengi huuliwa na wenzao wanapoonekana kuwa na wafuasi wengi. Kila kiongozi ana haki ya kutafuta kura na hakuna kiongozi ambaye anapaswa kuuliwa kwa sababu hiyo. Mwandishi anasema kuwa wote waliotoa hotuba zao katika hoteli ya Come- K ni kama vile Bwana $O_{2,}$ Jokanga, Tojombo, Kuka Pange, Freku, Onachi, na Bika. Mwandishi anasema kuwa wangekumbwa na hatari nyingi kama mbwa koko, gesi ya sumu, risasi na wimbo *zum zum zum nuclear wee!* Aina zote za bunduki zilitumiwa (Uk. 124). Vilevile, wote ambao hawakuunga mkono kiongozi wa NUKA Maotad walifanyiwa ukatili, mmoja wao ni Avad. Avad alichapwa na kulazimishwa kugura BORA na kujiunga na kundi la NUKA. Mwandishi anasema:

> "Utaasi BORA?"
> "Ndiyo. Ndiyo. Nimerudi NUKA.Nitashiriki katika mafamba.
> Tutanuka pamoja na kuicheza
> ngoma pamoja "alimaliza Avad.
> "Vema mrudisheni kwake."
> Avad alitoka pale akimangamanga (Uk. 156).

Avad alifahamu mwenye nguvu mpishe na hivyo ilimbidi asalimu amri. Hii ni tabia ya viongozi wengi Afrika. Hulazimisha viongozi walio chini ya uongozi wao kufanya

watakalo. Wasipofuata masharti yao huachishwa kazi na kuuliwa. Tume ya EACC (2016) inahitaji viongozi wafuate sheria katika ofisi za umma. Viongozi wanahitajika kuwa waaminifu katika ofisi za umma, matumizi mazuri ya mali ya umma na vilevile, kutojihusisha na mali inayohusiana na ufisadi.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) kuna matumizi mabaya ya mali ya umma. Maotad anatumia ofisi yake vibaya. Mwandishi anajenga mandhari ya ofisi yake kama ya kuogofya. Kuna kiti maalum ambacho kilikuwa na swichi nyuma yake. Kilitumiwa na Maotad kudhulumu wote ambao walimpinga Maotad. Mwandishi pia anaelezea mandhari ya mkanyageni orofa takriban 77 ambapo pia watu walifanyiwa ukatili na viongozi (Uk. 47). Vilevile, ubinafsishaji wa rasilimali za nchi pia ulifanywa kwa malango wa nyuma. Umiliki wa mali ulitegemea kiongozi gani uliyemfahamu. Viongozi walifaidika zaidi. Waliota vitambi ila wananchi walikuwa mwafulani. Uchumi ulizorota (Uk. 243).

Tume ya EACC (2016) imekashifu tendo la kumiliki mali inayohusishwa na ufisadi. Mwandishi wa riwaya ya *Mafamba* (Olali ,2012),anasema kuwa maendeleo ya sayari ya NUKA yalitokana na ufisadi (Uk. 9). Mandhari ya sebule ya Moatad yanadhihirishwa kuwa na vitu ambavyo vilihusishwa na ufisadi. Mwandishi anasema sebule ilizungukwa na mishumaa zulia, kalamu, mafaili, kiti, tarakilishi, chopasa ambazo zilitokana na sera ya mafamba. Sera ya mafamba ilikuwa imehalalishwa katika sayari hii (Uk. 12).

Katiba ya Kenya (2010) imetoa amri kuwa hakuna raia wa nchi ambaye anapaswa kuwekeza akiba katika nchi za nje. Wengi wa viongozi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), walienda kinyume na sheria hii. Mzee Twajua anadhihirisha suala hili katika hadithi yake. Anasema kuwa utawala wa BORA ulikuwa umeandika hundi ya

ngilishi bilioni 666 kwa muuzaji wa sayari mpya wa nje. Anasema kuwa viongozi waliona ustaarabu kuwekeza ngilishi nje ya sayari ya BORA (Uk. 170).

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), Munkari katika fikra za Bi. Saeeda anasema kuwa viongozi hutumia utandawazi kuteka vyama vya kisiasa na mafisadi hivyo chama kujikuta kinakuwa mawakala wa mafisadi ambao lengo lao ni kuiba na kuwekeza nchi nyingine (Uk. 224). Katika ndoto Hikmat anasema kuwa, watu waliopokea rushwa walikuwa wanawekeza nchi za nje. Mafisadi pia walijihusisha na wizi na kuhamisha utajiri wao kutoka Kiafra kwenda kujitajirisha zaidi nchi nyingine (Uk. 179). Anasema kuwa, dunia hupoteza kiasi cha dola trilioni moja kwa mwaka kutokana na rushwa. Fedha zinazopatikana kwa rushwa ndio huwekezwa nchi tajiri. Anasema kuwa, jambo hili husababisha umaskini katika jamii mbalimbali katika Kiafra. Rushwa ikitokea nchi tajiri huitwa kashfa ilhali ikitokea nchi maskini huitwa rushwa.

Katika Katiba ya Kenya (2010) hakuna yeyote ambaye anapaswa kufanya unyanyasaji wa aina yoyote. Katika riwaya ya *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012), sheria hii imevunjwa. Kuna unyanyasaji wa vilema, watoto, wafanyikazi na unyanyasaji wa jinsia. Mwandishi ametumia mhusika Kinaya kudhihirisha unyanyasaji wa jinsia. Tabu anahusishwa na kasisi Taabu ambaye anasemekana kumdhalilisha Kinaya katika madhabahu ya kanisa. Kasisi anakumbuka alivyofumaniwa na Kinaya na Kibiritingoma wakinywa divai. Kasisi vilevile, anakumbuka vile Kinaya alivyopiga kelele huku akidai kunyanyaswa kijinsia wakati alipokuwa padre Chuo Kikuu Cha Kuhisika (Uk 54). Vilema wananyanyaswa pia. Katika ndoto, Baingana ambaye alikuwa zeruzeru anaota wanaume wawili na mwanamke mmoja wakivamia pamoja na mamake Lakeisha. Wanampiga mamake kwa ubapa wa parange na kumtoa nje Baigana. Wanamkata Baingana na kumtishia Lakeisha kutopiga kelele (Uk. 183). Katika ndoto ya Sikujua,

miili ya albino ilisafirishwa kwa kutumia merikebu za kuelekea Tanga. Anasema kulikuwa na stoo kubwa ya kuhifadhi miili hii katika kisiwa cha Mtambwa kilicho karibu ambapo baadhi ya tambiko hizo zingalifanywa katika mahame ya Mtambwe mkuu (Uk. 64). Anaona jinsi madaktari walishiriki na serikali ili kuwaubua waganga wanaohusika na mauaji ya walemavu wa ngozi. Sikujua anazinduka usingizini anaposikia sauti ikiuliza;

Mbona mwawadhulumu Albino (Uk. 65).

Wafanyikazi wa nyumbani wananyanyaswa. Mwandishi akieleza mandhari ya Gehenna anasema waliokuwa na uwezo wa kuona ndani ya giza totoro ya Gehenna ni wale ambao hawakudhulumu wafanyikazi wa nyumbani (Uk. 3). Bi. Saeeda Khan anahukumiwa kwa kosa la kumtesa mfanyikazi wake wa nyumbani Mwanahamisi Mruke. Alifanya kazi kuanzia saa kumi na moja alfajiri hadi asubuhi iliyofuata. Hakuruhusiwa ale na familia, wakati mwingine alinyimwa chakula. Hakuwa na chumba cha kulala alipewa kigodoro na bedishiti na kulala kwenye sakafu. Hakupumzika wala hakuruhusiwa kutoka nje. Wazazi wake wanapougua hakupewa ruhusa ya kwenda kuwaona hadi wakafariki. Baadaye ananusurika kisha Bi. Saeeda Khan kutiwa ndani kwa shtaka la kuwasafirisha watu na kuwapunja (Uk. 88). Bi Saeeda Khan anamkoseshea Bi. Mruke haki ya ushirikiano, ya kutembea, haki ya kupata chakula, malezi na kadhalika. Huu ni uvunjaji wa sheria na upunjaji wa wafanyikazi wa nyumbani. Bi.Rabecca Belira ni mshukiwa wa pili aliyehusika na upunjaji wa wafanyikazi wa nyumbani. Mfanyikazi wake Methodia ambaye alikuwa amesafirishwa kutoka Kenya alifanywa mtumwa nyumbani. Alinyimwa haki ya usafiri, akadhulumiwa kimwili, kutukanwa, hakupumzika na kunyimwa haki ya kuwasiliana na familia yake. Methodia alitoroka baada ya kupewa ushauri na mama mmoja (Uk. 96). Watoto

wamenyanyaswa pia. Mwandishi anaeleza namna mtoto wa darasa la pili alikatwa miguu na kunyofolewa nywele utosini na kisogoni. Mwandishi anasema;

> Mwanafunzi huyo wa darasa la pili katika shule ya msingi ya Mbosisi alifariki dunia baada ya kukatwa miguu na kunyofolewa nywele utosini na kisogoni na watu wasiojulikana usiku wa kuamkia mwaka wa 2066 na kutoweka na viungo hivyo. Tukio hilo lilitokea siku iliyokuwa ya mkesha wa kuamkia maandamano ya kupinga mauaji ya watoto katika bara nzima ya Kiafra (Uk. 182-183).

Kulingana na tume ya Eacc (2016) hakuna mtu ambaye anapaswa kutoa hongo kwa sababu ya suala lolote lile. Sheria hii imekiukwa katika mtaa wa Bikerani-Msiige.Viongozi wanashiriki katika biashara haramu ya ukataji miti. Ni jukumu la kila mwananchi kuhifadhi mazingira kulingana na Katiba ya Kenya (2010). Viongozi wanakata miti na kuuza mbao katika nchi tofauti na kuweka akiba zao nchi za nje. Wanaolalamikiwa kuhusu suala hili ni wananchi. Munkari katika fikra za Bi. Saeeda Khan anaeleza madhara ya ufisadi. Anasema kuwa rushwa uharibu uadilifu na kuhatarisha maendeleo ya kiuchumi, amani na umoja wa Kiafra (Uk223). Anasema kuwa ufisadi ukiwa sehemu ya Kiafra, rushwa na wizi haviishi kufanywa na watu wenye mamlaka peke yao bali vitendo hivyo husambaa na kujengeka kwa watawaliwa. Anasema kuwa viongozi wengi hutoa hongo kwa wapiga kura ili wapigiwe kura. Hii inawezekana kwa kuweka mikakati mahususi ikiwa ni pamoja na kuhonga wananchi kwa fedha, mavazi, chakula, na vitu vingine vidogo vidogo kukidhi mahitaji ya fukara, kununua shahada za wapiga kura ili wasiweze kupiga kura kuwatishia wananchi kwa kutumia vyombo vya dola, kuunga mkono vyama vingine (Uk. 234).

Munkari anasema kuwa viongozi ununua baadhi ya maafisa wa tume ya uchunguzi ili majina ya wapiga kura yavurugwe hasa kwenye maeneo ya upinzani wasiweze kupiga kura kabisa au wakati waliopewa (Uk. 235). Kila mtu ana haki ya kupiga kura kulingana na katiba ya Kenya (2010). Kuhonga watu wakupigie kura ni kuenda kinyume na sheria.

Katika fikra za Hikmat anaonelea ni heri wawe na katiba upya. Vilevile, nchi ipigwe ukarabati na kuzaliwa upya. Anasema kuwa kuipitisha katiba sio mwisho wa safari ya kukabiliwa na ufisadi kazi ya kuitekeleza ipo. Anasema kuwa, pana uwezekano wa viongozi kukiuka sheria zilizowekwa na katiba na kuwateua wakuu wa sharia na Jaji Mkuu bila kuzingatia taratibu zilizowekwa. Mambo kama haya husababisha uongozi mbaya na uvunjaji wa sheria.

Kila mtu ana haki ya kufanya maandamano ili kupata haki. Kulingana na riwaya ya *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012) sheria hii haijazingatiwa. Wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Kuhisika wanafyatuliwa risasi na kufurushwa wakati walipokuwa wanafanya maandamano. Walikuwa wanapinga mfumo wa elimu uliowatweza Waafrika wasomi na kuwajenga hisia za kukata tamaa kwamba wao ni watwana mbele ya mabwana weupe. Walibeba mabago mbalimbali na moja ilikuwa imeandikwa;

THE CORRUPT POITITIAN CREED (Uk. 122).

Mwandishi anasema kuwa polisi mmoja alimlenga yule kijana na kufyatua risasi lakini haikumpata Hikmat alifyatuka kwa upande wake kama risasi. Baada ya kutawanywa na polisi wanafunzi walianza tena maandamano na kwa wakati huu wakibeba mawe. Wanafunzi hawa wanafanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa wahusika walionuia kubadilisha hali yao ya maisha. Hikmat na wenzake walipandwa na hasira na kuanza kuharibu magari, kuweka vizuizi barabarani na kuchoma moto majengo ya serikali, mabaa na stoo za pombe. Polisi waliuawa pia. Awali wanafunzi hawa walikuwa wamefanya maandamano kwa njia iliyokuwa na amani lakini baada ya kutawanywa na polisi vita vilizuka. Kila mtu ana haki ya kufanya maandamano yenye haki. Ilikuwa kinyume cha sheria kwa kujeruhi baadhi yao.

Kulingana na sheria za katiba ya Kenya (2010) kila mteja ana haki ya kuuziwa bidhaa halali. Katika mazungumzo ya Faki Nahodha na Baadayadhiki, Faki anasema kuwa wafanyabiashara wanauza bidhaa ambazo muda wake umepitwa na hazifai kwa matumizi ya binadamu. Baadhi ya bidhaa ni mchele, rangi za vyakula, nyanya za makopo, maji ya matunda, biskuti, maziwa ya vikopo na dawa za meno. Anasema wanaofanya hivyo hutoa hongo kwa Afisa mwezeshaji wa Bodi ya chakula, dawa na vipodozi (Uk. 78). Kwa upande mwingine, Hikmat anadhihirisha uvunjaji wa sheria hii katika fikra zake. Anasema kuwa maduka binafsi ya dawa yamegeuka kuwa karakana za sumu na hatimaye mauti ya wagonjwa kwa sababu ya wingi wa *fake drugs*, hospitali zinajali zaidi biashara kwa maana ya kuingiza fedha. Anasema kuwa hali ya afya inatisha kwa sababu wataalamu wanajiingiza kwenye biashara badala ya kutazama afya za watu (Uk. 177).

**3.3 Hitimisho**

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia vyanzo vya ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Baadhi ya vyanzo vya ufisadi ni kama vile umimi, tamaa, utovu wa maadili, ushindani wa kupata madaraka, migogoro, mapendeleo na utovu wa sheria. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa kuchambua vyanzo hivyo.Raslimali za nchi zilibinafsishwa kwa mlango wa nyuma.Vyombo vya habari vilitangaza kuhusu unyakuza wa ardhi,mito,maziwa na Barabara.Vile vile tamaa inaibuka kutoka kwa viongozi.Maotad wa sayari ya NUKA alipenda wale ambao haja zao zilitimizwa.Sakata zilizohusisha matumizi ya hongo kama *mfuko wa vito* na *Anglolasting* viliibuka.Mwandishi anadhihirisha tamaa ya viongozi katika serikali za kaunti.Bajeti na miundo misingi iligawanywa kwa upendeleo.Utovu wa maadili pia unabainika wakati wa kupiga kura.Viongozi waliiba kura.Kuna utovu wa maadili hospitalini ambapo madaktari wanauza *fake drugs*.Watu

wanaenda kwa wapiga ramli,kuua,kubeba vibiritingoma,kusambaza ukimwi kimaksudi,kuavya mimba na kadhalika.Migogoro inaibuka dhidi ya viongozi.Kuna migogoro baina ya viongozi wa sayari ya NUKA na BORA kwa sababu ya uongozi.Kuna migogoro ya matajiri na wafanyikazi.Matajiri wanadhulumu wafanyikazi wa nyumbani.Tumeeleza vyanzo hivi kwa kuzingatia mawazo ya Karl Marx. Matajiri ndio uzalisha mali.Kwa kufanya hivi huwatumikisha maskini hivyo kuleta pengo baina ya maskini na matajiri. Sura inayofuta itaangazia madhara ya ufisadi katika *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012).

# SURA YA NNE

# MADHARA YA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA *MAFAMBA NA WATU WA GEHENNA.*

## 4.1 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, mtafiti amejadili vyanzo vya ufisadi katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012). Katika sura hii, mtafiti ameshughulikia madhara ya ufisadi katika riwaya teule. Ameongozwa na nadharia ya uhalisia wa kijamaa kwa sababu huonyesha jinsi uhusiano kati ya tabaka la mabwenyenye na wachochole huleta mgongano unaosababisha kutokea kwa mapinduzi. Mivutano hii ndio usababisha madhara katika jamii hasa kwa watu wa tabaka la chini. Baadhi ya madhara ya ufisadi ambayo ameweza kufafanua ni kama vile, umaskini, kuzorota kwa uchumi, dhuluma dhidi ya wanajamii na uongozi mbaya

## 4.2 Madhara ya Ufisadi

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2012) inaeleza madhara kama uharibifu au athari mbaya. Ufisadi huibua madhara mengi katika jamii. Mengi ya madhara huathiri tabaka la chini. Baadhi ya madhara ya ufisadi ambayo mtafiti ameshughulikia ni kama vile umaskini, mauaji, kuzorota kwa uchumi, dhuluma na kudhoofisha utawala bora.

### 4.2.1 Umaskini

Kulingana na wamitila (2003), umaskini ni hali ya kukosa uwezo wa kufikia na kudumisha hali ya maisha inayohitajika. Anasema kuwa umaskini si hali ya kukosa pesa tu bali kukosa fursa ya elimu, afya na usalama. Kulingana naye, umaskini hujumuisha masuala ya kiuchumi, kijamii na kisaikolojia. Maithya (2022), maskini hupuuzwa na kuonekana watu wasio muhimu. Hakuna anayesikia kilio chake. Licha ya kuwa nchi ni tajiri, matajiri ndio hunufaika huku maskini wakila makombo. Umaskini umekuwa janga kubwa katika nchi nyingi.Umaskini huu usababishwa na ufisadi utokao

kwa viongozi na mwananchi wa kawaida katika jamii.Viongozi wengi wamekwamisha maendeleo ya nchi kwa sababu ya ufisadi.Wengi wakichaguliwa ujilimbikizia mali na kuiba mali ya umma na kuongezea utajiri wao.Matajiri uzidi kuwa matajiri na maskini uzidi kuwa maskini.Hii inaafikiana na nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambayo huagazia mfumo wa kiuchumi na kufanikisha mhimili kuwa wahusika huendeleza utabaka kimaksudi licha ya kuwa wanasawiri matukio ya kihistoria.

Katika riwaya ya *Mafamba,* ufisadi ni chanzo cha umaskini. Katika hotuba ya mzee Twajua, nchi ya Kiafra imekumbwa na janga la umaskini kwa sababu ya mafamba. Anasema;

> Tumekuwa katika umaskini mkubwa kutokana na mafamba ya mfuko wa vito.(Uk192)

Anasema watu wengi wamekuwa wakijihusisha na suala la ufisadi ila huwa hawakamatwi upelekwa mahakamani wanapewa hukumu kali, hukata rufani kisha kuachiliwa.Hurudia kile kile na kutenda zaidi ya awali.Mzee Twajua anasema kuwa hali hii ya kutoa hongo kwa wahalifu na kuachiliwa huru ndio usababisha umaskini.

Viongozi wa sayari mbalimbali walisababisha umaskini kwa wakazi wa Bikerani-Msiige.Mwandishi anasema kuwa matokeo ya maingililiano kati ya wakazi wa Bikerani-Msiige na viongozi wa sayari mbalimbali yalisababisha chuki,uhasama na umaskini mkubwa.(Uk132).Anasema pia wakazi wa Bikerani-Msiige hawakuwahi kuwa na taifa huru.Watu walijitambulisha kama watu wenye utamaduni uliojaa umaskini wa kupindukia.Hawakuwa na vyoo, barabara ,umeme, maji, shule ,chakula, nguo, hospitali wala usalama.Wengi walikuwa wafanyibiashara rejareja,wakulima wa kando ya mto na wengine walijiingiza katika biashara maarufu ya ubakaji.Waliishi kwa nyumba za madogo poromoka na mavazi yenye kupigwa viraka.Mwandishi anasema kuwa eneo la kijiografia walikoishi kulipitia pepo za kaskazini na kusi ambazo badala

ya kuleta mali zilileta umaskini.Pepo za kusi na kaskazini zilichangia kufanikisha juhudi za kiongozi Maotad wa sayari ya NUKA ambaye alisababisha umaskini katika sehemu hio.Anasema kuwa umaskini huo uliimarika sehemu hio kwa karne nyingi na kuathiri miundo ya makazi na utamaduni wa watu(Uk135).

Mazingira haya duni ya watu wa eneo la Bikerani-Msiige yanasababishwa na viongozi wenzake. Ni kinaya kwa kuwa wananchi waliowapigia kura wanaishi maisha ya umaskini ilhali wao wanaonekana kuishi mitaa ya kifahari, hoteli za kifahari na kuendesha magari ya kifahari. Katika SAUTI inayosika akilini mwa Avad,NUKA ilikuwa imeshiriki mafamba ambayo yalisababisha umaskini(Uk158)

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna*,unyanyasaji usababisha umaskini.Suala hili la unyanyasaji hufanya binadamu kuwa na woga,kunyenyekea na kuwa watiifu kwa watawala wao.Watu wengi usimama kidete na kupigana na suala hili kupitia maandamano na migomo.Katika chuo kikuu cha Kuhisika,wengi wa wanafunzi waliamini kwamba umaskini katika Kiafra ulikuwa zao la wanyanyasaji kama vile Bi.Saeeda Khan.Walitengeneza mazingira ambayo wengi waliokuwa wakikandamizwa hawangeendelea kuishi kwa amani na utulivu bali kukabiliwa na hali ngumu ya maisha(umaskini)(Uk121).Wanafunzi hawa wanakuwa wahusika wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa ambao hunuia kubadilisha hali ya maisha wakiwa na nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali katika jamii yao.

Katika fikra za mhusika huyu Bi.Saeeda Khan,mchezo wa *The matrix of corruption* unaendelea ambapo Munkari anatoa muhadhara wake.Anasema umaskini wa kupindukia unasumbua watu wengi Kiara .Jambo hili usababishwa na sera za vyama vya kisiasa,uongozi mbaya na ufisadi ambao unaitikisa Kiafra.(Uk222).Katika fikra hizo,naye Munkari anasema kuwa wanasiasa huwa na malengo binafsi wanaweza

kutengeneza jambo ambalo litazua mgawanyiko wa chuki kati ya makundi ya jamii husika,lengo lao likiwa kubaki madarakani jambo ambalo usababisha wananchi wengi kuwa maskini wa kutisha(Uk238)

Katika ndoto ya Hikmat ukoloni mambo leo ndilo zao la umaskini ambao umezidi kukithiri.Anasema viongozi wamejaa ukandamizaji na dhuluma,kwa kukosesha wananchi huduma muhimu na kunyimwa mafao yao.Viongozi walioko madarakani hawaelewi shida za wananchi na hawaonekani kuguswa na hali ya dhiki waliyonayo raia wa nchi(Uk156).Wananchi maskini ndio waliozidua cheche za kudai uhuru na kuunganisha watu wa taifa.Watu walichanga pesa kuimarisha chama kilichotawala lakini hawakushika tofauti ambao baada ya kuchaguliwa walibadilika na kunyanyasa wananchi maskini waliotawala.Mambo kama haya yameweza kushuhudiwa katika nchi nyingi za Kiafrika na usababisha pengo kubwa baina ya maskini na matajiri.

Hongo ni kikwazo cha maendeleo katika nchi nyingi. Utoaji hongo usababisha uvunjanji mwingi wa pesa za umma hivyo kurudisha nchi nyuma kimaendeleo. Jambo hili usababisha umaskini hasa kwa tabaka la chini. Tabaka la juu likizidi kujilimbikizia mali na wakipatana hutoa hongo na kesi zao kusitishwa ni suala ambalo usababisha nchi kuwa maskini na kuanza kutafta mikopo kutoka nchi za nje.Viongozi pia uelekea kupandisha kodi ili kujaribu kufidia suala hili la mikopo jambo ambalo uzidisha umaskini hasa kwa watu wa tabaka la chini.

Katika ndoto ya Hikmat,Chirimiri sio tu adui wa haki bali pia ni kikwazo cha maendeleo.Anasema kuwa chirimiri limeathiri sekta zote za nchi yetu kiasi kuwa ili mtu apate haki yake hana budi kujipapasa.Anasema suluhisho la hilo ni serikali kujenga viwanda vipya ili kutoa ajira, kuboresha sekta ya kilimo ,kufufua viwanda na kuongeza tija,kuunda serikali ndogo, kupunguza matumizi yasiyo lazima ya safari za mara kwa

mara nje ya nchi na kuondoa ukarabati wa kila mwaka wa ikulu(Uk156).Binadamu hivyo wanapaswa kujikomboa na janga la umaskini linalosababishwa na uongozi mbaya na kuchagua viongozi wazuri bila kushawishiwa kuchagua viongozi kwa misingi ya pesa na zawadi ndogo ndogo.Watafanikiwa wakipiga kura vyema bila kuhongwa na kubadilisha hali yao ya maisha wakiwa na nia ya kumiliki njia kuu za kuzalisha mali kama ilivyo katika nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.

### 4.2.2 Mauaji ya Watu

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), kuna mauaji mengi ambayo yalifanywa na viongozi. Anyango (2016) anasema kuwa mauaji ya kikatili ni mauaji ya kinyama. Anasema kuwa viongozi wenye nyadhifa hushiriki mauaji ili kuhifadhi nyadhifa zao na anayejaribu kupigania haki ukomeshwa kwa kifo.

Katika riwaya ya *Mafamba*, wengi wa wahusika waliouliwa ni wananchi waliopinga uongozi mbaya wa Maotad na viongozi wenzake. Wengi wa baadhi ya watu waliouliwa ni wananchi waliopinga uongozi wa Maotad na vitendo vyake vya kifisadi kama vile upendeleo na matumizi mabaya ya mali ya umma. Mwandishi anasema kuwa, kuna watu wengi na vifo vilivyosemekana kutokana na Maotad wa sayari ya NUKA. Mauaji hayo ni ya wahusika kama vile Rojoo. Maotad alipoulizwa kifo cha Rojoo alidai labda ni mahasidi wa NUKA kama vile Amrao (Uk. 7). Katika sehemu tofauti, mwandishi anasema kuwa Maotad alikiri kumuua Rojoo kwa kuwa alipinga mafamba. Anasema zipo njia za kuzima maadui wake na alifikiria kutumia njia aliyomsalimia Rojoo ingawa aliogopa kwa kuwa watu walijua na kuchukia sayari yake (Uk. 56). Mwandishi anasema kuwa ilikuwa kosa kubwa kumwagia kitumbua mchanga. Jibu la uhaini huu kama walivyoita ilikuwa kwenda jongomeo kupitia njia ya kitanzi (Uk. 25).

Come-K ilikuwa eneo la kihistoria ambapo viongozi wengi walitoa hotuba zao. Mwandishi anasema kuwa aliyetoa hotuba huko alipelekwa sehemu iliyoitwa Mkanyageni kwa nia moja ya kuozea huko. Baadhi ya watu waliofika Mkanyageni ni kama vile; Mastanji, Charu, Bwana $O_2$, Jokaga, Tojombo, Kuka, Pange, Freku, Onachi Bika na wengine. Wote waliuliwa na Maotad kwa sababu ya kupinga Mafamba (Uk. 124). Vilevile, Maotad anamtishia Avad. Alimtishia kumuua kwa vile alikuwa ameunga kundi la LiMioe lililokuwa likipinga uongozi mbaya wa Maotad. Anaitwa ofisini naye Maotad na anapokuwa mle ndani anakumbuka picha za wale ambao hawakutii wenye nguvu na hatimaye kubatilishwa *cadaver*!(maiti) Picha za watano wale zilimwogofya (Uk. 159).

Sauti kutoka popote inadhihirisha mauaji kama madhara ya ufisadi. Inasema matatizo yanayozikabili sayari yanatokana na uongozi mbaya. Kitovu cha uongozi mbaya ni mafamba. Inasema kuwa mafamba ni ibilisi ambaye ameangamiza mataifa mengi ya Kiafrika na sayari zote ulimwenguni. Sauti hiyo inasema kuwa mafamba imesababisha vifo vya watu wengi na maafa makubwa.

Mafamba imesababisha vifo vya wengi (Uk. 240).

Ufisadi pia umeenea katika sekta ya afya. Madaktari katika sekta za hospitali za umma huuza dawa za serikali na wengine kuziuza katika hospitali zao za kibinafsi. Usipokuwa na pesa huenda ukaangamia. Matibabu huwa ya wenye mali. Mwandishi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) anasema ili kufanikiwa kufanya jambo lolote katika sayari ya NUKA ilikulazimu kutoa hongo. Anasema kuwa katika mahospitali watu wengi walikufa. Ungepewa dawa iwapo ungeimbia daktari na wafanyikazi wa pale wimbo huu wa Mafamba. Ungekosa kufanya hivyo ungalikwenga jongomeo (Uk. 32).

Imekuwa jambo la kawaida kwa wafuasi wa vyama mbalimbali kuuliwa. Kumekuwa na visa vya vikaragosi wa viongozi wa vyama tofauti kupotea hasa wakati wa kampeni. Wafuasi hao huishi kuuliwa na kupotea kabisa. Katika sayari ya NUKA, kiongozi aliyeteuliwa na Maotad kutawala baada ya Maotad wanamkatakata mzee mmoja vipande pamoja na wanawe wanne kwa sababu ya kutoungana na upande wao na badala yake kumfuata Amrao, wafuasi wa Amrao walidhulumiwa pia kukatwa sehemu zao za siri, kuchopolewa na wafuasi wa U. Uhalifu huo ulihusishwa na majini na mapepo (Uk. 99). Mauaji mengi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) yanatokana na uongozi mbaya na yanatoka kwa viongozi hasa Maotad kiongozi wa sayari ya NUKA. Wote wa waliouliwa ni wale waliopinga uongozi wa Maotad dhidi ya mafamba.

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), kuna mauaji tofauti ambayo yanasababishwa na viongozi ili kupata mamlaka na kukwamilia mamlakani. Kumekuwa na visa vingi nchini dhidi ya mauaji kutoka kwa viongozi. Wengi huangamia kupitia ajali za barabarani na angani ilhali wengine hupatikana wameuliwa tu. Anyango (2016) amesema baadhi ya mauaji huwa ni ya kusetiri ushahidi. Uchunguzi umekuwa ukifanywa ila hakuna mtu ambaye hupatikana na hatia hio. Wanaohusika na matendo hayo ya kihayawani ni wanasiasa na uangamiza viongozi wenzao hasa waliopinga uongozi wao au kutambua njama zao. Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), Sikujua anaota ndoto akipelekwa katika chumba kimoja ambacho kilikuwa kizuri. Anampata Takosani na wapambe wake wawili. Licha ya kumkaribisha, walimkumbusha kuwa alipokuwa mamlakani alishiriki katika vita vya kikabila na kusababisha umwagikaji mwingi wa damu. Wakati na baada ya uchaguzi (Uk. 60). Anatuhumiwa tena kuua watu 666 alipokuwa mbunge (Uk. 63).

Katika ndoto, Angamizamtuwewe II anatuhumiwa na mauaji ya kimbari nchini NdaRwa mnamo mwaka wa 2060 ambapo baadhi ya watu wa kabila moja waliuliwa na serikali iliyosimamiwa na viongozi wa kabila jingine. Mauaji haya yanatokana na ukabila wa viongozi. Anatuhumiwa pia kuhusika na upangaji wa makundi yaliyohusika na mauaji ya kimbari (Uk. 250-251).

Mauaji pia yanadhihirishwa na madaktari hospitalini. Mauaji mengi hutokea kwenye hospitali kwa sababu ya ukosefu wa dawa na kuuza dawa zisizostahili. Madaktari wengi katika hospitali za umma huuza dawa hizo katika hospitali zao za kibinafsi. Jambo hili husababisha watu hasa tabaka la chini kukosa matibabu na wengi kufariki kwa sababu ya aina hii ya ufisadi wa madaktari. Katika kipidi cha *The night of the living dead*, Mat anasema kuwa maduka binafsi ya dawa yamegeuka karakana za sumu na kusababisha mauti ya wagonjwa. Wengi wa madaktari hao huuza *fake drug*(dawa bandia). Waliofanya kazi katika hospitali za serikali waliwaagiza wagonjwa kwenda kunua dawa katika hospitali zao. Anasema kuwa madaktari siku hizi wanafanya kazi ovyo kwa kuzidisha dawa na kusababisha mauti (Uk. 177-178). Madaktari hujali zaidi biashara kuliko afya.

Migomo mingi ambayo hufanyika shuleni au taasisi mbalimbali huibuka kwa sababu ya ufisadi. Mambo ambayo husababisha migomo hiyo ni kama vile matumizi mabaya ya mali ya umma au ukabila. Katika Chuo Kikuu cha Kuhisika wanafunzi wanagoma dhidi ya mfumo wa elimu uliowatweza Waafrika kuwa wao ni watwana mbele ya mabwana weupe (Uk. 121). Wanafunzi walionekana kubeba mabango yaliyoandikwa. *THE CORRUPT POLITICIAN CREED.* Wanafunzi hao walifyatuliwa risasi. Mmoja wa wanafunzi aliyeitwa Hikmat alibaki mahututi huku damu zikimtoka mdomoni. Hikmat anapigwa risasi kwa sababu ya kutetea haki za wenzake chuoni jambo ambalo linafanikisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa haja ya mafukara wa

ulimwengu ni kuimarisha udikteta wa makabwela. Kupigwa risasi kwa Hikmat kuliamsha hasira kwa wanafunzi ambapo askari walipigwa mawe na wengine kuuliwa. Mwandishi anasema mapambano hayo yalikuwa dhidi ya ufisadi.

> Nguvu mpya ya wazee iliungana na vijana kuelekeza mashambulizi kwa adui, mapambano yakaendelea usiku kucha-Mapambano dhidi ya ufisadi (Uk. 125).

Mapambano haya yakiendelea kulikuwa na ngoma iliyochezwa redioni ikitaka viongozi wa kiimla wa nchi fulani asongee mbele kujenga nchi. Mwandishi anasema nchi nyingi zilikuwa zimeanguka baada ya maandamano makubwa wakitumia *facebook* na *twitter*. Ni bayana kuwa maandamano yalikuwa yamesababisha mauti. Ufisadi ni janga ambalo limesababisha mauaji ya watu wengi. Wengi hujaribu kujificha kutokana na janga hili kwa kuua waliotambua uovu au uhalifu wao. Watu wengi hupotea kiholela holela na wengine kuangamia katika ajali za barabarani na angani kwa sababu zisizojulikana. Uchunguzi pia hufanywa kifisadi na matokeo huwa hayapatikani kamwe. Wauaji hawatambulikani kamwe. Ni jambo la kusikitisha kwa sababu mengi ya mauaji hutekelezwa na viongozi. Wananchi hivyo basi wanapaswa kuwa makini katika suala la upigaji kura na kuchagua viongozi bora bila kushawishiwa kwa vyovyote vile kuwachagua kwa misingi ya vitu fulani.Wanapaswa kuwa wahusika wa kimaendeleo katika nadharia ya Uhalisia wa kijamaa ambao wananuia kupindua au kubadilisha hali yao ya maisha.Wananchi wanapaswa kuchagua viongozi bila kuhongwa ndipo wachague viongozi halisi.

### 4.2.3 Kudhoofisha Maendeleo ya Kiuchumi

Njeri (2018) anasema kuwa kuzorota kwa uchumi usababishwa na matumizi mabaya ya fedha jambo ambalo husababisha umaskini na kuongezeka kwa bei ya vyakula na huduma zingine za umma. Uongozi mbaya husababisha uchumi kuzorota. Viongozi

wengi ujihusisha katika ubadhirifu hivyo raslimali nyingi kukosekana katika nchi. Njoroge (2014) anasema kuwa ufisadi usababisha pesa kupotea kwa njia zisizofaa. Sereti (2016) anasema kuwa viongozi wengi hunyakua ardhi ya umma jambo linalosababisha hali ya kutoaminiwa.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), Maotad anasema kuwa wakazi wa Bikareni-Msiige walikuwa saliti na waasi. Walikuwa wanalalamika kuwa hakuna dawa hospitalini, hakuna barabara, usalama na kuwa maji yalikuwa machafu na hayo machafu yalikuwa hayako. Anasema kuwa walikuwa wanalalamika kuwa kila kitu Maotad alichokuwa amepata alikuwa amenunua kutokana na sera ya mafamba (Uk. 16).

Katika hadithi ya mzee Twajua, utawala wa BORA umezorotesha uchumi hata baada ya kutawanya utawala wa NUKA. Mzee Twajua anaeleza ubadhirifu ambao unaendelezwa na utawala wa BORA ambao unasababisha kuzorota kwa uchumi. Anasema kuwa utawala huo uliandika hundi ya ngilishi bilioni 666 kwa muuzaji Engineer ambayo akaunti yake ilikuwa katika sayari moja ya nje. Ngilishi nyingi zilikuwa zimepotea katika hazina kuu ya BORA ambazo zilisababisha sayari kuanza kuyumbayumba. Zilisababisha ukosefu wa dawa hospitalini, bajeti ya kukarabati barabara ilipunguzwa, gharamu za kawi zilipanda juu maradufu na shida nyingi kuanza baada ya nyingine. Majengo yalianza kuporomoka. Kwa sababu ya mafamba, tume ya Kar pi Mangich iliidhinisha majengo hayo yaendelee. Baada ya muda, majengo hayo yaliporomoka na kuua watu wengi.

Utawala wa BORA ulishindwa kuwaokoa badala yake walituma ujumbe kutaka usaidizi kutoka sayari za mbali. Engineer alikuwa kiwakilishi cha mafamba. Kampuni yake haijulikana ni ya nani. Aliulizwa ni vipi alifanya biashara na mapepo. Walitaka

kujua vile alituma hela katika akaunti ya mapepo. Watu walitaka ajiuzulu. Walimlaumu kiongozi mpya wa BORA LiMioe kwa kuanzisha upya mafamba. Baadaye alisalimu amri na kumtoa Engineer katika wadhifa wake. Mwandishi anasema kuwa mafamba ilikuwa imeenea dunia nzima sio BORA tu. Kila siku vyombo vya magazeti vilichapisha habari za mafamba (Uk. 208-210).

> OVER 2000 FIRMS IN BRIBES SCAM Companies paid &18bn to SAHU regime under The oil for food deal (Uk. 211).

Baada ya hadithi hii ya Mzee Twajua, watu walijawa na huzuni na kusema kuwa aina hii ya viongozi wa BORA ndio ulikuwa chanzo cha umaskini wao. Sera hii ya Engineer ya mafamba na viongozi wenzake wa BORA kama vile LiMioe ilikuwa imezorotesha uchumi wa BORA hivyo kusababisha umaskini.

Katika sayari ya BORA, ukusanyaji wa ushuru ulifanywa kwa watu wachache hasa wa tabaka la chini. Mwandishi anasema kuwa ushuru ulikuwa unakusanywa na serikali ya BORA ingawa kuna watu ambao walikataa kulipa ushuru. Anasema kuwa licha ya haya yote, maendeleo yalikuwa machache sana licha ya ukusanyaji huu wa ushuru (Uk. 229). Wengi wa viongozi waliwekeza akiba katika nchi za nje bila kulipa ushuru. Hii ni suala ambalo lilichangia uchumi kuzorota katika nchi nyingi za Kiafra. Mwandishi pia anasema ubinafishaji wa raslimali za nchi ulifanywa kwa mlango wa nyuma. Ugavi wa mali ulikuwa kwa msingi wa kiongozi gani uliyemfahamu kule juu. Viongozi walifaidika ilhali wananchi walizidi kuwa maskini. Aliyekuwa na jina akawa ghafla hana jina. Nchi nzima ilitapika maskini na kurudi nyuma. Wananchi walikuwa maskini hadi walikosa senti za kusaga. Kujilimbikizia mali kwa viongozi kulirudisha nchi nyuma kimaendeleo na kusababisha ongezeko la umaskini.

Mzee Twajua alieleza kuwa silaha ya ukombozi ilikuwa ni kutegemea debe. Aliwahimiza kujipigapiga ili kupata dinari za kueneza mapambano ya kihistoria. Kujinusuru huku kungepanua hazina yao ya kuupindua uongozi mbaya. Aliwakumbusha kuwa viongozi walikuwa wameabudu mafamba na kusababisha wao kuwa nyuma na wangejiokoa tu katika debe (Uk. 245). Ukombozi wanaotafta kupitia debe unadhihirisha mhimili wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa binadamu huwa na matumaini juu ya maisha yake na kueleza jinsi atakua mshindi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa aina yoyote.

Katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012), hongo ni kikwazo kikuu cha maendeleo. Hikmat katika hotuba anasema kuwa wananchi hukandamizwa na kudhulumiwa kwa kukoseshwa huduma muhimu. Anasema kuwa viongozi walioko mamlakani huwa hawaelewi shida za wananchi wala hawaonekani kuguswa na dhiki walionayo raia wa nchi. Anasema kuwa chirimiri sio adui wa haki bali pia ni kikwazo cha maendeleo. Chirimiri ilikuwa imeathiri sekta zote za nchi (Uk. 156). Ondoro (2021) anasema kuwa uongozi mbaya hauleti maendeleo na kuzorota kwa Uchumi tu bali usababisha umaskini. Hikmat anasema kuwa kulikuwa hakuna maendeleo kwa sababu ya uongozi mbaya. Sekta ya afya ilikuwa imezorota. Hospitali zilikuwa hazina dawa. Wananchi waliambiwa wanunue dawa. Serikali ilikuwa haijatengeneza utaratibu wa kupeleka dawa kwenye hizi zahanati. Hali ya usafiri ilikuwa mbovu pia. Barabara zilikuwa mbovu ambazo zilikwamisha mawasiliano. Jambo hili ilisababisha baadhi ya kaunti kuonekana kama si sehemu ya taifa. Kodi ilikuwa inakusanywa lakini haikuchangia maendeleo. Hikmat anasema kodi inayokusanywa sasa na serikali haichangii maendeleo ya nchi tu bali inawanyanyasa wananchi wa chini. Anasema serikali inatoza kodi zilizoitwa za maendeleo lakini haikuwa na maendeleo. Chama

tawala kilitoza watu wa chini kodi na kuwasamehe watu wa juu na kuendeleza utabaka kimaksudi licha ya kusawiri matukio ya kihistoria kama ilivyo katika nadharia ya Uhalisia wa kijamaa ambapo wahusika hutekeleza matendo yao kitabaka. Tabaka la wanyonge ikiongozwa na Hikmat wanaweka juhudi kujipa mamlaka na nguvu za kiuchumi kwa kugoma dhidi ya uongozi mbaya. Anasema kuwa kodi za manyanyaso zinaingiza fedha chache mno ikilinganishwa na kodi zinazosamehewa watu wa tabaka la juu (Uk. 159). Katika ndoto, Hikmat anasema kuwa rushwa husitisha maendeleo ya nchi. Anasema rushwa ndio chanzo kikubwa cha umaskini katika jamii mbalimbali katika Kiafra. Anasema kuwa hakuna maendeleo kwa kuwa pesa zinazopatikana kwa rushwa nchi za Kiafra huhifadhiwa katika nchi tajiri. Jambo hili husababisha dunia kupoteza kiasi cha dola zisizopungua trilioni moja kwa mwaka kutokana na rushwa (Uk. 179).

Katika hotuba ya Munkari Gehenna, umaskini unawasumbua watu wengi vijijini na mjini Kiafra.Anasema kuwa ufisadi na rushwa ni adui namba moja wa haki za wananchi. Katika kudai uwajibikaji wa viongozi, vitendo vyao viovu uharibu kabisa dhana ya uadilifu katika uongozi na kuhatarisha maendeleo ya uchumi amani na mshikamano na umoja wa Kiafra (Uk. 223). Viongozi wengi wamezorotesha uchumi kupitia wizi. Viongozi wakuu wa nchi pia huzorotesha nchi kupitia mikopo. Wanasiasa wenyewe ujihusisha na kashfa ya ufisadi na wakizorotesha nchi wanakopa mikopo kutoka nchi za nje. Baadhi ya nchi wanazokopa wengi huwa wamewekeza akiba huko kutokana na mali waliyoiba bila kulipa ushuru. Ushuru umeachiwa mwananchi wa kawaida. Wengi wa viongozi na watu mashuhuri hukwepa kulipa ushuru. Jambo hili hukosesha nchi pesa nyingi ambapo uchumi huzorota na kusababisha pengo kubwa baina ya matajiri na maskini. Ni jukumu la viongozi kuwajibika na taasisi za kukusanya kodi kukusanya kokote bila kubagua yeyote. Sheria za nchi ni vizuri zifuatwe na

wawekezaji wa nchi za nje wafuatiliwe na kuchunguzwa. Itawezekana tu kipindi ambacho kutakuwa na viongozi waadilifu. Wamitila (2003) anasema kuwa ili kukabiliana na uongozi mbaya, lazima kuwe na mfumo wa kuhamasisha raia katika utawala ili kuboresha utawala na kuleta maendeleo endelevu.

#### 4.2.4 Dhuluma Dhidi ya Wanajamii

Wamitila (2003) anaeleza dhuluma kama nguvu inayotumiwa na wenye mamlaka dhidi ya wale wasiokuwa na mamlaka jambo linalofanya kukosekana kwa usawa wa haki katika jamii. Anyango (2016) anasema kuwa dhuluma hudhuru nafsi ya mtu na kumfanya kukosa matumaini na vilevile huacha pengo ambalo hujaribu kuzibwa kwa njia zozote zile. Ufisadi husababisha walio na hatia na wasiona hatia kufungwa jela. Wengi wa watu wa tabaka la juu wakipatikana na hatia hutoa hongo kisha kuachiliwa huru. Baadhi ya watu wa tabaka la chini hufungwa pasi na kosa hasa kwa kuekelewa shutuma na watu wa tabaka la juu.

Mwandishi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) anasema kuwa sheria za sayari zote hazikuwaruhusu watu kujitetea. Haki za binadamu hazikuheshimiwa na kuzingatiwa. (Uk. 25) Amrao ni mmoja wa watu ambao wanatiwa jela bila hatia. Maotad alimchukia Amrao kwa kuwa alifikiri Amrao alitaka kumnyanganya uongozi. Amrao alikuwa akipinga uongozi wa Maotad dhidi ya mafamba. Mafamba katika sayari ya NUKA ilikuwa sheria. Amrao naye alipinga mafamba hivyo kukawa na vurugu baina ya Amrao na Maotad.Mikinzano kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa ndio iliosababisha kuzuka kwa nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Nadharia hii hukusudia kuleta usawa hivyo kuathiri uhalisia wa maisha. Amrao alisukumwa ndani kwa kipindi cha miaka 30. Makosa yalikuwa tofauti. Alituhumiwa kutaka kumwaga mchanga ndani ya kitumbua. Katika miaka hiyo 30 haikutokea siku hata moja ambayo ilitolewa ushahidi wa kutosha kuwa alikuwa amemwaga mchanga. Kosa kama hili ilikuwa ni

adhabu ya kwenda jogomeo kupitia kifo (Uk. 24-25). Mwandishi pia anasema kuwa babake Amrao ndiye aliyekuwa wa kwanza kufungiwa kwa miaka mingi iliyopita. Haikujulikana sababu ya kukamatwa. Wakereketwa wake walisema kuwa bwana $O_2$ alikuwa ni kama hewa ya uhai ambayo kama haimo, maafa makubwa yangetokea. Yeye ndiye alikuwa simba wa kukabiliana na viongozi kama vile Maotad (Uk. 49) na kukua mhusika aliyenuia kubadilisha hali ya maisha ya NUKA na kufanikisha mhimili wa kwanza wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.

Katika mtaa wa Bikerani-Msiige, Ekari nyingi za misitu zilikuwa zimenyakuliwa na kasri za ajabu kujengwa humo na mbao za bei ghali kutoka aina nyingi za miti katika misitu hiyo. Wenye kuziuza walipeleka hela hizo katika sayari za mbali bila kulipa ushuru wowote. Aliyekamatwa na kufungiwa miaka saba alikuwa Sikujua tu. Sikujua hakuelewa sababu ya kufungwa baada ya kupatikana na hatia ya kukata miti kwa shughuli za kupata angalau fito za kujijengea nyumba. Aliokamatwa nao aliwaona baadaye wakiwa huru. Wengine walikuwa na hatia ya kukata ekari nyingi za miti. Wenye kuwashtaki walonekana kwenda zao wakicheka kicheko cha ushindi. Wenye kushtakiwa waliachiliwa huru baada ya kuonekana usiku wakibeba shanata au kutoa hongo. Kesi zilitupiliwa mbali. Baadaye Sikujua alijua ni mafamba. Scott( 2020) anasema kuwa kuna aina mbalimbali za dhuluma kama mauaji,unyanyasaji wa wafanyikazi na unyakuzi wa mali ya umma.

Waliochapisha magazeti kuhusu uharibifu wa misitu walishtakiwa na baadhi ya wateja. Mteja mmoja alidai gazeti lilimkebehi mbele za watu na kumchafulia jina na kukosa kupata alichokuwa akitafuta. Wenye magazeti na wateja hao walijikuta mahakamani siku ya kesi. Wenye magazeti walikuwa na tumaini la kupata ushindi. Walishangaa kupatikana na hatia ya kumchafulia mteja jina na kumpaka matope. Iliamuliwa mteja alipwe milioni saba. Wenye magazeti hawakuelewa mwelekeo huo. Baada ya kipindi

kifupi walielewa ilikuwa ni sera ya mafamba. Mteja alikuwa tayari kumpiga ganja hakimu (Uk. 173-175).

Katika hadithi ya mzee Twajua hongo ilikuwa aina ya ufisadi ambayo ilikuwa imesababisha wenye hatia kuachiliwa. Anasema kuwa kitovu cha ufisadi kilikuwa ni kushauriana na hakimu ili kesi ibatilishwe (Uk. 195). Mzee Twajua pia anaeleza aina mbalimbali za mafamba zilizokuwa zimetokea NUKA. Kulikuwa na *mfuko wa vito* na *sera ya Nopro.* Anasema hakuna aliyekamatwa kuhusiana na kashfa ya mfuko wa vito. Mwenye hatia alikwa huru kwa sababu ya mafamba na Nopro (Uk. 193-194). Sera hii ya Nopro pia iliwezesha wabakaji kuachiliwa huru. Iliwarejesha wauaji uhuru mpya wa kutekeleza mauaji mapya ilhali waliotekeleza mauaji waliku huru. Biashara haramu katika mji wa Tugor Amor ilipata ushindi mkubwa dhidi ya biashara halali yote sababu ya sera ya Nopro.

Katika mtaa wa Tugor Amor vileo hatari viliuzwa ambavyo vilipofusha watu na kufanya wanaume kuwa hanithi. Mwenye kuuza kileo hicho hatari alijulikana na wakazi wa Tugor Amor. Serikali ya BORA pia ilimfahamu vizuri. Alichukuliwa hatua. Mwandishi anasema kuwa alikuwa amekamatwa mara kadhaa na kuachiliwa huru kwa sababu ya sera ya Nopro (Uk. 191).

Katika riwaya ya *watu wa Gehenna* (Olali, 2012) kuna watu mbalimbali ambao wanashtakiwa kwa sababu ya ufisadi na wengine kufungwa jela. Katika ndoto ya sikujua, anaota akishtakiwa na mhusika Takosani akiwa na wapambe wake kwa sababu ya kukata maelfu ya miti kutoka ardhi iliyonyakuliwa. Hata baada ya kushutumiwa aliendelea kufanya vivyo hivyo. Anahukumiwa kuwa alipokuwa mamlakani alishiriki katika vita vya kikabila na kusababisha umwagikaji wa damu. Wapambe hao walimfunga kitandani na kumtandika bila huruma. Walizidi kumshtaki kuwa alikuwa

anatumia nguvu za kiume zilizotokana na wachawi kumwezesha kufanya mapenzi kwa muda mrefu na mtu asiye mke wake. Alitengeneza ubikira bandia wa wanawake ili kuzini nao na kufurahisha waume wao. Pia alikuwa ameua watu 666 alipokuwa mbunge alikuwa amehusika na mauaji ya albino. Mashtaka haya yanaibua aina mbalimbali za ufisadi ambazo sikujua alikuwa amejihusisha (Uk. 60-65).

Zoezi la upigaji kura husababisha ugomvi na baadhi ya watu kukamatwa hasa katika maeneo ambayo wizi wa kura huendelezwa. Ongarora (2020) anasema kuwa wananchi hujuta kwa kutumia haki zao za kidemokrasia vibaya na kuchagua viongozi ambao hujigeuza miungu wajeuri kwa maana ya kuwa na kiburi na kuwatesa. Faki Nahodha anasimulia Baadayadhiki kisa cha jambo lililosababisha kuwa IDPS. Anasema kuwa zoezi la uandikishaji wapiga kura katika kisiwa cha Al Jazeera Al Khadra lilisitishwa baada ya vurugu kujitokeza katika vituo vya kupiga kura na kusababisha baadhi ya watu kujeruhiwa na wengine kukamatwa. Zoezi hili pia lilikuwa limesababisha kulipuliwa kwa mabomu na raia kupambana na polisi (Uk. 69-70).

Wafanyakazi wengi wa nyumbani hudhalilishwa na waajiri wao na mwishowe waajiri hao hukamatwa. Kuna visa vingi vya waajiri ambao wameshtakiwa kwa sababu ya dhuluma dhidi ya wafanyikazi. Kuna wahusika ambao wameshtakiwa kwa sababu ya suala hili katika riwaya ya *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012) wahusika hao ni kama vile Bi. Saeeda Khan na Bi. Rabecca Balira. Bi. Saeeda Khan anashtakiwa kwa biashara ya kusafirisha watu ughaibuni kwa minajili ya kuwapunja kinyume na sehemu ya 4 ya sheria za ukimbizi na uhamiaji wa mwaka wa 2044 Uingereza. Anapewa adhabu ya kufungo cha miaka 14 (Uk. 95). Mhusika wa pili kutoka Uingereza ni Bi. Rabecca Balira. Rabecca anampunja mhusika Methodia kutoka Kenya. Methodia anatiliwa vikwazo vya kutembea, kutwaliwa mshahara, kudhulumiwa kimwili na kutukanwa. (Uk. 96).

Walimu shuleni pia wamehusishwa na ubakaji na kuwapa ujauzito. Walimu wengi wameweza kuachishwa kazi na wengine kufungwa jela kwa sababu ya unyanyasaji huu wa kijinsia. Katika nchi ya Kiafra, kunazuka uvumi dhidi ya mwalimu Richo na Dwanyryok wa shule ya Masira. Walituhumiwa kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi mwenye umri wa miaka kumi na minne katika shule ya msingi ya Huruma. Walikuwa wametarajiwa kupandishwa kizimbani ili kujibu mashtaka kwa mujibu wa sheria ya makosa ya kujamiana Kiafra na msichana yeyote mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane hata kama akiridhika kufanya tendo la kujamiiana. Mwanaume aliyefanya tendo hilo alifanya kosa la kubaka. Wanasema kuwa suala la ubakaji lilitokana na mfumo wa *Tuition.* Wanaonekana kuwa serikali irudishe hadhi ya elimu kwa kuipiga marufuku *Tuition* (Uk. 244-246) jambo ambalo wanaonelea kuwa litawapa matumaini na kuwa washindi dhidi ya unyanyasaji wa walimu hivyo kufanikisha mhimili wa nne wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.

Katika ndoto, kondakta mmoja wa gari za Nahegen anaota kuhusu wakili mmoja aliyetarajiwa kushtakiwa mbele ya mchezo wa *Gehenna Roulette.* Anatuhumiwa kwa kufahamu njama za mauaji ya kimbari nchini NdaRwa mnamo mwaka wa 2064. Angamizamtuwewe 11 alikana mauaji hayo. Anatuhumiwa pia kuchochea hisia za mauaji ya kimbari nchini NdaRwa. Mlevi pia anatuhumiwa kwa kushiriki kufanya mapenzi ya jinsia moja nchini na mwanaume mwenzake na kufanya sherehe ya uchumba. Anafahamishwa na Munkari kuwa alitenda uhalifu dhidi ya mila, dini na sheria (Uk. 250-252).

Makasisi pia wamehusika katika udhalilishaji wa kijinsia. Akilini mwa Faki Nahodha, Kasisi Taabu anashtumiwa kwa tuhuma za kumdhalilisha kijinsia binti mmoja katika madhabahu ya kanisa. Kinaya alisikika kupiga kelele huku akidai kunyanyaswa kijinsia na kasisi Taabu alipokuwa padre huko Chuo kikuu cha Kuhisika. Baadaye anafyatuliwa

risasi na Munkari na ubongo wake kuharibiwa. Faki Nahodha anamuona kasisi taabu akinywa chai ya maziwa akisoma gazeti la *The Tombstone Epitaph* yenye maandishi.

> Kiafra prosecutors said today they had charged a priest with raping an underage. Girl after a tip-off from a special body set up to combat abuse scandals that have rocked the church. The priest allegedily abused the girl aged 13 at the time, over three-year period from 2050, telling her she wouldn't go to heaven if she didn't comply (Uk. 256).

Mapadri wengi nchini wameweza kutuhumiwa na visa kama hivi. Wengi huwadhalilisha kijinsia mabinti na hata maghulamu. Wengi wameishia kukosa uaminifu katika viapo vyao vya useja. Suala la ufisadi limechangia watu wengi kukamatwa na kufungwa jela. Baadhi ya watu hasa wenye nacho uachiliwa huru kwa vile hutoa kitu kidogo.

### 4.2.5 Kudhoofisha Utawala Bora

Ondoro(2021) anasema kuwa uongozi mbaya ni ule ambao hauleti maendeleo.Kulingana naye,viongozi huongoza na tamaa na ubinafsi hivyo kupora raslimali za nchi yao.Wamitila (2003) anasema kuwa uongozi mbaya ni mchakato ambapo viongozi hushindwa kutimiza wajibu wao katika jamii.Anasema kuwa uongozi mbaya ujumuisha vitendo kama vile ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka.Ongarora(2020) anaeleza kiongozi mzuri ni yule ambaye hutenda haki kwa watu wote badala ya kuzingatia maslahi ya wachache wanaomzunguka.Baadhi ya sura za ufisadi husababisha uongozi mbaya. Viongozi hujihusisha na masuala kama vile matumizi mabaya ya mali ya umma, hongo, ubadhirifu, ulaghai, upokonyaji, upendeleo, unasaba na kudhalilisha wananchi hivyo kusababisha uongozi mbaya.

Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), ufisadi husababisha uongozi mbaya. Viongozi wa sayari ya NUKA na BORA wanajihusisha katika mafamba jambo ambalo linasababisha uongozi mbaya na kusukuma wananchi kuungana kwa pamoja na

kutafuta njia mwafaka za kuondoa viongozi hao. Kinyume ni kuwa hata baada ya kuondoa Maotad wa sayari ya NUKA na kumteua LiMioe wa Sayari ya BORA, ufisadi bado unakithiri na kufanya watu kukata tamaa dhidi ya viongozi. Viongozi hao wanajihusisha na mambo kama vile matumizi mabaya ya mali ya umma, hongo, upokonyaji, unyanyasaji, unasaba na kadhalika. Maovu haya yanaelekeza viongozi hawa kuongoza vibaya. Katika riwaya hii mwandishi anatumia sauti inayosikika ikisema;

> “Matatizo ambayo yanazikabili sayari zote yanatokana na uongozi mbaya. Kitovu cha uongozi huu ni mafamba. Sera ya mafamba huwafanya viongozi kuingiwa na kiburi. Kiburi kikiingia viongozi hupofuka. Wakipofuka hawaoni, na wanakuwa makatili” (Uk240)

Sauti hii inadhihirisha uongozi mbaya katika sayari ya NUKA ambao husababishwa na sera ya mafamba. Wanasema kuwa mafamba ikiondolewa mataifa mengi hayatazidi kuangamia. Sauti inasema kuwa NUKA iling’olewa kwa sababu ya mafamba. Wakati ilipong’olewa watu walikuwa na matumaini kuwa watakuwa washindi dhidi ya unyanyanyasaji wa sayari mpya ya BORA kama ilivyo katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Viongozi wa BORA walipoteuliwa walizidi kuongoza vibaya. Sauti inasema kuwa mafamba haijatawala tu BORA bali mataifa mengi ya Kiafra, na ulimwengu mzima. Sauti inasema kuwa suluhu la mafamba kutoka kwa viongozi ni kunyang’anywa wadhifa (Uk. 240-241) hivyo kuwa wahusika wa kubadilisha hali yao ya maisha; hili ni kulingana na muhimili wa kwanza wa nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.

Nchi nyingi zimerudi nyuma kimaendeleo kwa sababu viongozi wao hujihusisha katika suala la ufisadi hivyo kusababisha uongozi mbaya. Katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012), Mzee Twajua alijaribu juu chini kuelimisha wananchi dhidi ya kuchagua viongozi wabaya. Aliwaambia kuwa viongozi wengi walipenda mafamba hivyo

kusababisha nchi kurudi nyuma kimaendeleo. Anaonelea suluhisho la kuchagua viongozi wanaoendeleza uongozi mbaya ni kupitia debe.

> …. Namna ya kufanya hivyo ni kupitia debe. Debe la siri-siri ni kutoboa siri-siri ni kuwangoa kabisa viongozi walioshiriki mafamba na ukandamizaji (Uk. 246).

Uongozi mbaya unasababishwa na tamaa ya viongozi. Viongozi hujihusisha katika wizi wa raslimali za nchi hivyo kusababisha umaskini katika nchi husika. Katika riwaya ya *mafamba* (Olali, 2012) viongozi wanatumia raslimali za nchi vibaya. Mwandishi anasema wakazi wa Bikerani- Msiige hawakuwa na taifa huru. Walikuwa na utamaduni uliojaa umaskini. Walikosa raslimali muhimu kama vyoo, barabara, umeme (Uk. 134) Jambo hili ndilo linalowasukuma kutaka viongozi wapya.

Katika riwaya ya *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012) ufisadi umesababisha uongozi mbaya. Katika maongezi ya Hikmat na Nafsi ya Baingana, viongozi wengi hukua ndumakuwili kwa kuunga mkono kitu fulani na baadaye kupinga. Anasema kuwa viongozi ukiunga mkono kitu hicho kinapoonekana kuwapa unafuu au maslahi fulani japo ni maumivu kwa wengine. Viongozi nao basi hukua hawana msimamo. Mara wanasema hawataki utawala wa mikoa kesho wanataka mara mahakama ya *Eughh* kesho wanaikashifu na kudai wanataka *local tribunal*(mahakama za kienyeji). Vilevile, viongozi wengine huchaguliwa kwa njia za kishirikina hivyo kuchaguliwa bila sifa za uongozi. Viongozi hao huishia kutawala vibaya. Mwandishi anasema kuwa kuna vita dhidi ya mauaji ya albino na ukataji wa sehemu za siri za maiti kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti. Anasema watu hupata kura kutokana na uuaji wa albino. Anasema kuwa wanafanya hivyo kwa sababu katiba haigusii haki ya albino. Wanasiasa kama vile wagombea ubunge, useneta, udiwani na pia rais uenda kwa waganga kujisafisha ili kuepukana na balaa ya kushindwa kwenye uchaguzi wa viti hivyo. Upewa maagizo ya

kuua albino ili kusafisha nyota zao. Wengi hukua na hisia za hatia kwa sababu ya kupata ushindi usio halali. Ushindi wao hutokana na vitisho vya kishirikina. Hikmat anasema kuwa watoto wa wakubwa hupata nafasi ya uongozi wasipokuwa na sifa wala uwezo wa uongozi. Hupata uongozi tu kwa kubebwa na wazazi wao ambao tayari ni viongozi. Anasema analipinga kwa sababu hunyima watu fursa ya kupata viongozi bora na kunyima fursa ya uongozi watoto wa maskini wenye vipaji na sifa za uongozi (Uk. 208-211).

Katika nafsi ya Hikmat viongozi walinajizi raslimali ya nchi kwa kunyakua mashamba bila aibu. Ambrose (2014) anasema kuwa uongozi mbaya huongozwa na tamaa ya kujilimbikizia mali na kusahau mali hiyo kutokana na raslimali za wananchi. Hikmat anasema kuwa viongozi hutumia hazina ya uzeeni kujinufaisha wao wenyewe bila kuwajali wakongwe waliostaafu. Pesa zilizokusanywa kama ushuru hazikutimiza malengo yake. Ufisadi hivyo basi ulialalishwa na kufanywa kama taasisi na ukaingia kwenye kila sekta ya umma. Kulikuwa na imani kuwa kukua serikalini ilikuwa kujiingiza katika masuala ya kichinichini na ya kujinufaisha kwa watu wachache. Hikmat anasema suluhu la uongozi mbaya unaosababishwa na aina mbalimbali za ufisadi ilikuwa kuunda katiba mpya.Hikmat ni mhusika katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambao ni  mhusika wa kimaendeleo.Ananuia kupindua na kubadilisha hali ya maisha katika Chuo Kikuu cha Kuhisika kwa kuongoza katika migomo. Hikmat ana wasiwasi pia dhidi ya katiba mpya alijua kuwa kutekelezwa kwa katiba hio na viongozi ingekuwa ngumu. Wangekiuka sheria na kuteua mkuu wa sheria jasusi mkuu, jaji mkuu bila kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Hikmat pia anaelezea unyanyasaji wa viongozi wa dini. Unyanyasaji huo umewasukuma mapadri kuongoza vibaya. Anasema kuwa kila kukicha viongozi wa kidini hupatikana kwenye patashika za sex scandal nzito. Gazeti la *Haenea Times* lina

habari ya kasisi Taabu ambaye alihamishwa hadi parokia ya St. Reficul (Uk. 263-266). Akilini mwa Faki Nahodha kasisi Taabu anashtumiwa vikali kwa tuhuma za kumdhalilisha kijinsia binti mmoja katika madhabahu ya kanisa. Sauti ya taabu inasikika:

> "Kinaya, nakupenda"
> "Taabu, wewe ni kasisi!"
> "Usijali"
> "Ninajali"
> "Adam alishindwa kustahimili. Sembuse mie?"
> "Hapana kasisi taabu!"
> "Njoo hapa!"
> "Lakini…!"
> "Lakini nini?"
> "Hapa ni katika madhabahu matakatifu!"
> "Usijali. Hakuna atakayejua"
> "Twende chumba cha kubadilisha joha!"
> "Let's have sex in the pulpit!" (Uk. 253).

Faki Nahodha anasema kuwa Kinaya alikuwa uchi wa mnyama akipiga kelele huku akidai kunyanyaswa kijinsia na kasisi Taabu wakati alipokuwa padre huko chuo kikuu cha Kuhisika (Uk. 254). Huu ni uongozi mbaya wa kidini unaosababishwa na unyanyasaji wa kijinsia.

Ukabila na ubaguzi husababisha uongozi mbaya katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Katika mazungumzo ya Faki Nahodha na Baadayadhiki, wanasiasa kutoka vyama tofauti tofauti ushawishi wafanyabiashara kuwabagua wateja wanaowauzia bidhaa madukani kwa misingi ya chama cha kisiasa. Huwanyima huduma wateja wenye itikadi tofauti za kisiasa. Ushauriwa kutouza mazao yao kwingine na kubagua wateja kwa misingi ya kiitikadi. Baadayadhiki anamwambia Faki Nahodha kuwa suala hili husababisha kukiuka masharti ya leseni na haki za binadamu. Wanaeleza pia namna viongozi walivyokuwa wachochezi wakati wa kampeni za uchaguzi, jambo linaloibua ukabila. Baadayadhiki anasema kuwa wasiwasi ulikuwa umetanda kwao kufuatia kusambaa kwa vipeperushi vilivyowataka watu wa jamii yake

kuhama na kurudi kwao (Uk. 78-79). Ubaguzi na ukabila kutoka kwa wanasiasa hivyo basi husababisha uongozi mbaya unaosukuma wananchi kulalamika na kugura kwao.

Akilini mwa Bi. Saeeda Khan, Munkari anatoa hukumu dhidi ya viongozi wafisadi. Anasema kuwa ufisadi husababisha uongozi mbaya ambao husukuma watu kuwa maskini. Munkari anasema kuwa watu wengi Kiafra ni maskini. Munkari anasema;

> Ufisadi na rushwa ni adui namba moja wa haki ya wananchi katika kudai uwajibikaji wa viongozi kwa sababu vitendo hivyo viovu vinaharibu kabisa dhana nzima ya uadilifu katika uongozi na hivyo kuhatarisha maendeleo ya uchumi, mshikamano na umoja wa Kiafra (Uk. 223).

Munkari anasema kuwa ufisadi uhusiana na uongozi wa nchi unaotokana na siasa za vyama na dawa ya ufisadi itapatikana endapo tu wanasiasa wataweka maslahi yao binafsi na vyama vyao na kujali maslahi ya taifa. (Uk. 222-223).Kulingana na Munkari wanasiasa hawa ni wahusika ambao huendeleza utabaka licha ya kusawiri matukio ya kihistoria kama ilivyo katika mhimili wa pili katika nadharia ya Uhalisia wa kijamaa.

Baadhi ya sura za ufisadi husababisha uongozi mbaya. Wananchi huzidi kuteseka na pengo baina ya maskini na tajiri kukua pana. Nchi hufilisika na uchumi kuzorota na kusababisha chuki na ukataji tamaa kutoka kwa wananchi. Baadaye wananchi hulazimika kuungana na kuteua viongozi tofauti katu wabadilishe nchi yao.Hili uafikiana na nadharia ya Uhalisia wa kijamaa kuwa wahusika unuia kubadilisha hali yao ya maisha. Kinyume ni kuwa hata wengine wakichaguliwa mtindo huwa ni ule ule wa kujihusisha na ufisadi.

### 4.3 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameshughulikia madhara ya ufisadi. Mtafiti amebainisha madhara ya ufisadi kama vile umaskini, mauaji, dhuluma, kuzorota kwa uchumi na kadhalika. Ametumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa kufafanua madhara

hayo.Kiongozi wa sayari ya NUKA Maotad anashiriki mauaji ili kuwanyamazisha waliopinga sera yake ya mafamba.Ilikuwa jambo la kawaida kwa wafuasi wa vyama mbalimbali kuuliwa.Mauaji yalitokea hospitalini ambapo madaktari walikuwa wanauza *fake drugs(dawa bandia)* na wakati mwingine kulikosekana dawa kwa kuwa walikuwa wameiba madawa na kuuza katika hospitali zao za kibinafsi.Viongozi wengi wallitoa hongo na kusababisha kuzorota kwa Uchumi.Dhuluma pia inajitokeza.Sheria za sayari ya NUKA haikuruhusu watu kujitetea.Haki za binadamu hazikuzingatiwa na kuheshimiwa.Watu waliuliwa,kubakwa, na kuambukizwa ukimwi kimaksudi.Ufisadi ulisababisha uongozi mbaya.Vingozi wa sayari ya BORA na NUKA walijihusisha katika mafamba. Viongozi walifisidi raslimali za nchi kwa kunyakua mashamba bila aibu.Viongozi hao walikuwa na tamaa na ubinafsi hivyo kusababisha umaskini.Madhara haya yote yanaibuliwa na matajiri hivyo kufanikisha nadharia ya uhalisia wa kijamaa kuwa matajiri ndio uzalisha mali kwa kunyanyasa maskini katika uzalishaji mali hivyo kuibua matabaka tofauti.Sura inayofuata itabainisha muhtasari,matokeo na kutoa mapendekezo ya utafiti kwa watafiti wa baadaye.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO,MUHTASARI,MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia hitimisho la utafiti, mukhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, matatizo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehenna* (Olali, 2012). Malengo makuu ya utafiti yalikuwa kwanza kuelezea sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya teule. Pili, kufafanua vyanzo vya ufisadi katika riwaya hizo na tatu ni kutathmini madhara ya ufisadi katika riwaya ya *Mafamba* (Olali,2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali,2012).

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia wa kijamaa inayotokana na mawazo ya Karl Marx akitoa fikra zake kwa mwanafalsafa Hegel na nadharia ya Udenguzi iliyoanzishwa na mwanafalsafa wa Ufaransa Jacques Derrida (1976) na kuchangiwa na wengine. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa imetumika kwa sababu huelezea mfumo wa uzalishaji mali ambamo kuna tabaka la juu na la chini. Tabaka la juu ukiuka maadili ya kiutawala na kudhalilisha tabaka la chini na njia wanazotumia kumiliki mali ni za kifisadi. Nadharia ya Udenguzi imetumika ili kufidia upungufu wa nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa ambayo imekoleza itikadi na kupuuza masuala ya kisanaa. Hivyo basi nadharia ya Udenguzi imetumika kuibua fasiri tofauti za ufisadi kwa kutumia vigeu vya lugha, wahusika na maudhui.

Sura ya kwanza ya utafiti huu inaeleza kuhusu usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia za utafiti na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imetathmini muhtasari wa riwaya teule, pamoja na sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012 na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Lengo la kwanza limeafikiwa kutokana na kufafanua sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya teule. Mihimili ya nadharia ya Udenguzi ilifaa kwa kuwa sura za ufisadi zilizoibuka ni kama vile ubadhirifu, kumiliki mali inayohusishwa na ufisadi, unyanyasaji, ulaghai , ukwepaji ushuru na kuwekeza akiba nchi za nje.

Sura ya tatu imeshughulikia vyanzo vya ufisadi katika riwaya zilizoteuliwa. Uhakiki uliongozwa na vipengele vya wahusika na maudhui . Vyanzo vilivyoainishwa ni kama vile tamaa, umimi, utovu wa maadili, ushindani wa kupata madaraka, mapendeleo, udhaifu wa kisheria na uongozi mbaya.

Raslimali za nchi zilibinafsishwa kwa mlango wa nyuma.Vyombo vya habari vilitangaza kuhusu unyakuza wa ardhi,mito,maziwa na Barabara.Vile vile tamaa inaibuka kutoka kwa viongozi.Maotad wa sayari ya NUKA alipenda wale ambao haja zao zilitimizwa.Sakata zilizohusisha matumizi ya hongo kama *mfuko wa vito* na *Anglolasting* viliibuka.Mwandishi anadhihirisha tamaa ya viongozi katika serikali za kaunti.Bajeti na miundo misingi iligawanywa kwa upendeleo.Utovu wa maadili pia unabainika wakati wa kupiga kura.Viongozi waliiba kura.Kuna utovu wa maadili hospitalini ambapo madaktari wanauza *fake drugs*.Watu wanaenda kwa wapiga ramli,kuua,kubeba vibiritingoma,kusambaza ukimwi kimaksudi,kuavya mimba na kadhalika.Migogoro inaibuka dhidi ya viongozi.Kuna migogoro baina ya viongozi wa sayari ya NUKA na BORA kwa sababu ya uongozi.Kuna migogoro ya matajiri na wafanyikazi.Matajiri wanadhulumu wafanyikazi wa nyumbani.Tumeeleza vyanzo hivi kwa kuzingatia mawazo ya Karl Marx. Matajiri ndio uzalisha mali.Kwa kufanya hivi huwatumikisha maskini hivyo kuleta pengo baina ya maskini na matajiri

Mihimili ya nadharia ya Ujamaa ilionyesha vyanzo vya ufisadi ambavyo huibuliwa na wahusika wazalishaji mali na ambao uibua utabaka na kuibua vyanzo zaidi zya ufisadi.

Katika sura ya nne tumeshughulikia madhara ya ufisadi katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012). Lengo la tatu lilitumika kuchunguza sura hii. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa imetuwezesha kubainisha baadhi ya madhara ya ufisadi. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa huangazia mfumo wa kiuchumi ambapo tabaka la juu ukiuka maadili ya kiutawala na kudhalilisha tabaka la chini. Ukiukaji huu wa maadili ndio husababisha baadhi ya madhara ya ufisadi. Kama vile umaskini, mauaji, uongozi mbaya na kuzorota kwa Uchumi.

**5.3 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo matatu. Kwanza ni kutathmini sura mbalimbali za ufisadi, pili kuelezea vyanzo tofauti vya ufisadi na tatu ni kubaini madhara ya ufisadi. Lengo la kwanza limeafikiwa kutokana na kufafanua sura mbalimbali za ufisadi katika riwaya teule. Mihimili ya nadharia ya Udenguzi ilifaa.Sura za ufisadi zilizoibuka ni kama vile upendeleo,ubadhirifu, unyanyasaji ,ulaghai, ukwepaji ushuru na kuwekeza akiba nchi za nje . Tukielezea ubadhirifu,tumebainisha jinsi viongozi hutumia raslimali za nchi kama vile ofisi na mamlaka.Viongozi wengine pia ukatalia mamlakani na kujenga mandhari ya ofisi zao kama za kuogofya kama vile Maotad kiongozi wa sayari ya NUKA.Vile vile anateua viongozi wasiokuwa na sifa za uongozi ili kujinufaisha.Unyanyasaji umebainika pia ambapo wasiomuunga mkono Maotad wanapigwa na kudhulumiwa.Wengine wanakamatwa kwa makosa wasiyofanya.

Wengine pia wananyanyaswa kwa kunyiwa haki ya kijitetea kama vile Sikujua.Watu wanalipwa hili kupiga kura.Wanapewa zawadi ndogo ndogo kama hongo ya kuwapigia viongozi kura.Wanaohusika katika kashfa mbalimbali wanaachiliwa kwa sababu ya

hongo na kesi kuwaendea maskini.Viongozi tofauti wamewalaghai wananchi kwa kutolipa kodi.Viongozi wa sayari ya NUKA wanatoa bajeti hewa.Viongozi waliuza bidhaa bandia,kuuza viwiliwili vya albino na kuongeza bei ya bidhaa.Baadhi ya viongozi kama Avad mfuasi wa LiMioe anawekeza pesa nchi za nje bila kulipa ushuru.Wengine waliwekeza pesa walizopata kwa njia ya hongo.Wengine wanakwepa ulipaji kodi.Waliotozwa kodi ni watu wa tabaka la chini.Mtafiti ameeleza sura tofauti za ufisadi zaidi ya matumizi mabaya ya pesa za umma hivyo kufanikisha nadharia ya uhalisia wa kijamaa kuwa hakuna toleo la mwisho la kazi ya fasihi

Katika lengo la pili, mtafiti amebaini baadhi ya vyanzo vya ufisadi katika riwaya teule. Utafiti umezingatia mawazo ya Karl Marx kuwa matajiri ndio uzalisha mali hivyo kutumikisha maskini na kuibua vyanzo hivyo vya ufisadi. Baadhi ya vyanzo hivyo ni kama vile umimi, tamaa, utovu wa maadili, ushindani wa madaraka, mapendeleo, udhaifu wa sheria na uongozi mbaya. Raslimali za nchi zilibinafsishwa kwa mlango wa nyuma.Vyombo vya habari vilitangaza kuhusu unyakuzi wa ardhi,mito,maziwa na Barabara.Vile vile tamaa inaibuka kutoka kwa viongozi.Maotad wa sayari ya NUKA alipenda wale ambao haja zao zilitimizwa.Sakata zilizohusisha matumizi ya hongo kama *mfuko wa vito* na *Anglolasting* viliibuka.Mwandishi anadhihirisha tamaa ya viongozi katika serikali za kaunti.Bajeti na miundo misingi iligawanywa kwa upendeleo.Utovu wa maadili pia unabainika wakati wa kupiga kura.Viongozi waliiba kura.Kuna utovu wa maadili hospitalini ambapo madaktari wanauza *fake drugs*.Watu wanaenda kwa wapiga ramli, kuua, kubeba vibiritingoma, kusambaza ukimwi kimaksudi, kuavya mimba na kadhalika.Migogoro inaibuka dhidi ya viongozi.Kuna migogoro baina ya viongozi wa sayari ya NUKA na BORA kwa sababu ya uongozi.Kuna migogoro ya matajiri na wafanyikazi.Matajiri wanadhulumu

wafanyikazi wa nyumbani.Tumeeleza vyanzo hivi kwa kuzingatia mawazo ya Karl Marx. Matajiri ndio uzalisha mali.Kwa kufanya hivi huwatumikisha maskini hivyo kuleta pengo baina ya maskini na matajiri.

Lengo la tatu lilitumika kuchunguza sura hii. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa imetuwezesha kubainisha baadhi ya madhara ya ufisadi. Nadharia ya Uhalisia wa Kijamaa huangazia mfumo wa kiuchumi ambapo tabaka la juu ukiuka maadili ya kiutawala na kudhalilisha tabaka la chini. Ukiukaji huu wa maadili ndio husababisha baadhi ya madhara ya ufisadi. Baadhi ya madhara ya ufisadi yaliyopatikana katika fasiri zetu kwa kigezo cha mihimili ya Uhalisia wa kijamaa ni kama vile umaskini, mauaji, maasi, uongozi mbaya na kuzorota kwa Uchumi. Kiongozi wa sayari ya NUKA Maotad anashiriki mauaji ili kuwanyamazisha waliopinga sera yake ya mafamba.Ilikuwa jambo la kawaida kwa wafuasi wa vyama mbalimbali kuuliwa.Mauaji yalitokea hospitalini ambapo madaktari walikuwa wanauza *fake drugs* na wakati mwingine kulikosekana dawa kwa kuwa walikuwa wameiba madawa na kuuza katika hospitali zao za kibinafsi.Viongozi wengi wallitoa hongo na kusababisha kuzorota kwa Uchumi.Dhuluma pia inajitokeza.Sheria za sarari ya NUKA haikuruhusu watu kujitetea.Haki za binadamu hazikuzingatiwa na kuheshimiwa.Watu waliuliwa, kubakwa, na kuambukizwa ukimwi kimaksudi.Ufisadi ulisababisha uongozi mbaya.Vingozi wa sayari ya BORA na NUKA walijihusisha katika mafamba. Viongozi walifisidi raslimali za nchi kwa kunyakua mashamba bila aibu.Viongozi hao walikuwa na tamaa na ubinafsi hivyo kusababisha umaskini.Madhara haya yote yanaibuliwa na matajiri hivyo kufanikisha mawazo ya Karl Marx kuwa matajiri ndio uzalisha mali kwa kunyanyasa maskini katika uzalishaji mali hivyo kuibua matabaka tofauti

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umebaini kuwa watu wa tabaka la juu udhulumu watu wa tabaka la chini. Tabaka hili hudhulumu watu wa tabaka la chini kwa sababu ndio wamiliki wa mali na wazalishaji hivyo kuibua vyanzo na madhara ya ufisadi. Kulingana na maelezo yetu ufisadi ni wa aina mbalimbali ila si matumizi mabaya ya pesa tu. Ni utafiti ambao utafaa watafiti kuelewa vyanzo, madhara na aina za ufisadi, Tume la EACC katika kuongeza uwazi na uwajibikaji, Serikali kuu na Serikali za ugatuzi zitaweza kutoa ushahidi kwa maamuzi ya kisera na Taasisi mbalimbali ambazo zinahusika na haki za binadamu na wananchi kwa ujumla zitaongeza uwazi na uwajibikaji.

## 5.5 Matatizo ya Utafiti

Utafiti ulikumbwa na changamoto za utafsiri kwa sababu ya baadhi ya matini tuliyohitaji yalikuwa kwa lugha ya kingereza hivyo yalihitaji kutafsiriwa. Pili ilikuwa vigumu kumpata mtunzi wa kazi teule ili kumhoji kuhusu masuala aliyoibua hata hivyo utafiti ulikamilika.

## 5.6 Mapendekezo

Tumechunguza sura mbalimbali za ufisadi ambapo ni maudhui moja tu katika riwaya za *Mafamba* (Olali, 2012) na *Watu Wa Gehanna* (Olali, 2012). Riwaya hizi zilifaa kwa kuwa mwandishi huyu ana uzoefu wa kuandika matini zake kwa kuagazia maudhui ya ufisadi. Hata hivyo, bado tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu mambo yafuatayo.;

1. Tafiti zingine zifanywe kuhusu sura za ufisadi katika fasihi simulizi,ushairi na tamthilia.
2. Kwa kuwa baadhi ya mandhari yaliyohusika ni mandhari ya kimazingaombwe, utafiti ufanywe kuhusu mandhari ya kimazingaombwe kama yalivyotumika

katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* (Olali, 2012) kwa kutumia nadharia ya uhalisia ajabu.

## MAREJELEO


Ambrose, B. M. (2014).*Kuchunguza masuala ya kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert:Mfano wa Kusadikika na kufikirika.*Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.(Haijachapishwa)

Anyango, A, P, (2016).*Usawiri wa uovu katika riwaya teule za Ben P. Mtobwa.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyata. (Haijachapishwa).

TUKI (2015). *Kamusi kuu ya Kiswahili sanifu.*Nairob*i.*Oxford university press.

Barthes, R. (1997). *The death of the Author,* in readings in the theory of religion. Routledge.

Bisztray, G. (1978). *Marxist Models of literary Realism*.Newyork:Colombia University press.

Baxandall, L. (1972).*Radical perspectives in the arts*.Middlesex:Penguin Books.

Derrida, J. (1976). *Of grammatology and writting and diffrence. Routledge*

Ethics and Anti-corruption commission.(2016)*. The Ethics and Anti-Corruption commission the fourth Quarterly report.*

FOKUS, (2011). *Kijitabu cha mwongozo wa kuzuia ufisadi.*

Hegel,G (1971) *Introduction to Aesthetics:Oxford:Clerendon*

James ,C .V. (1973*) Soviet socialist Realism*:Origins and Theory.London: Macmillan Press.

Kariuki, M, M.,Ogola, J. O., & Wendo, N.(2025).*Tathmini ya athari ya utabaka na ukengeushi katika tamthilia ya Kigogo*.Jarida la Afrika Mashariki la masomo ya kiswahili,8(1),105-116

Kausi, B. G. (2021). *Dhuluma za kitabaka katika riwaya za Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Hajachapishwa).

Kerre, E. (2020). *Maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya za chozi langu na dunia mashaka makuu*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Kimalu, P. K., & Marimba, K. (2014). *Research methods monitoring and evaluation.* Nairobi, Kenya: Kamami Enterprise limited.

Government of Kenya(GoK).(2010).*The constitution of Kenya* 2010.

.Nairobi:Government printer.

Kimeu, A. N. (2016*). Maudhui ya ukombozi katika wimbo mpya na msururu wa usaliti.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Lomatoro, J. P. (2014). *Viwango vya uhalisi na ubunifu katika riwaya teule za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Hajachapishwa).

Macharia, F. M. (2021). *Tathmini ya hadithi fupi zilizowasilishwa katika British Broadcasting Corporation:Mtazamo wa Edgar Allan poe na Leech*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Maithya, J. K. (2022). *Uhalisia katika mashairi ya kezilahabi (Dhifa).*Eastern Africa Journal of Kiswahili (EAJK),1(1),43-49.

Muthumbi, F. M. (2005*). Mikakati na mbinu za usimilishwaji katika fasihi ya watoto*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Muusya, J. K., $ Kingei, K. K. E.(2017) *Maadili ya kisiasa katika riwaya za kiswahili:Kufa Kuzikana na Babu Alipofufuka.*Mulika Journal.

Mayieka, M. N.(2015). *Masuala ibuka katika riwaya za kisasa:Kidagaa kimemwozea na mhanga nafsi yangu*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Miller,E .F. (1979).Metaphor and political knowledge.*American Political Science Review* 73(1),155-170.

Mugenda, O. M., $ Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods:Quantitative and qualitative approaches.*(Vol.2,No.2).Nairobi:Acts press

Mugwika, F. (2012*). Dhana ya uchimuzi katika uendelezaji wa Riwaya ya kimajaribio ya mafamba*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Murumba, J. (2013). *Mtindo katika Watu Wa Gehenna*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Nairobi.(Hijachapishwa)

Muthui, E. K. (2019). *Tathmini ya maudhui katika tamthilia teule za Kiswahili zinazotahiniwa shuleni za upili nchini Kenya:MstahikiMeya(2009) na Kigogo (2016).*Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha South Eastern Kenya.(Haijachapishwa)

Mutuku, K. M . (2016). *Ukiushi katika tafsiri ya mashairi ya Kingereza:Mfano wa when the bullets begin to flower na risasi zianzapo kuchanua*.Tasnifu ya Uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Mwangi, J. W. (2013).*Uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya mpya: Babu alipofufuka(Said A Mohammed) na Watu wa Gehenna.(Tom Olali)* .Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Mwaniki ,J, M. (2018). *Athari za mtagusano kati ya jamii na ekolojia katika ushairi wa Kithaka wa Mberia:Bara jingine na Rangi ya anga*.Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Mwaniki, P. (2011). *Vichekesho vya machangi na kihenjo:mtazamo wa sanaa ya ubwege*.Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta .(Haijachapishwa)

Nasimiyu, C. N. (2016). *Athari ya mazingira ya kihistoria na kijamii katika uwasilishaji wa maudhui ya dhifa(E.Kezilahabi).*Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta .(Haijachapishwa)

Njenga, A, W. (2021):*Uongozi unavyojitokeza katika fasihi ya kisasa:Uchunguzi wa riwaya mpya ya miaka ya 2000*.Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Njeri,W,F. (2018) *Mchango wa vijana wa kuleta ukombozi katika Yasinya,Zinguo la Mzuka na Mwavyaji wa Roho*.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi .(Haijachapishwa)

Ndung'u ,B. W.(2022). *Athari za matukio ya kihistoria katika riwaya za Nyongo Mkalia Ini na Mafamba.*Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta .(Haijachapishwa)

Nyandwaro, L. K., $ Malugu, A.(2024) .*Nafasi ya nyimbo za kizazi kipya katika ufundishaji masuala mtambuka katika mtaala wa umilisi*.|Jarida la mwanga wa lugha, 9(1), 117-128.

Njogu, K., & Chimerah, R.(1999).*Ufundishaji wa fasihi na mbinu*.Jomo Kenyatta foundation

Njoroge, A. W. (2014). *Viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya za Mwenda Mbatiah:Vipanya vya maabara na majira ya tufani*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa).

Ochenja, R. (2008). *Maigizo kama mbinu ya maudhui katika riwaya mbili za Ken Walibora*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Okemwa, M. K. (2017). *Mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi: Mfano wa visasili katika mafuta(1984) na walenisi(1995)*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Olali, T. (2012). *Watu wa Gehenna*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Olali, T. (2012). *Mafamba*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omoga, R.G. (2018). *Mwananchi wa kawaida kama mdhulumu wa maslahi yake katika tamthlia za kilio cha haki,amezidi na mstahiki meya*. Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Ondoro, V. J. (2021). *Maudhui ya siasa na athari zake katika jamii;mifano kutoka diwani ya kaza macho*.Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Ongarora (2020),*Usasa katika ushairi wa Mberia*:Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Maasai Mara.(Haijachapishwa)

Sereti, C. (2016). *Taswira ya mwamko wa kisiasa miongoni mwa vijana katika tamthilia za Pango (2003) na Mstahiki Meya* (2009). Tasnifu ya uzamili.Chuo kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Njogu,K,na R.M Wafula (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.Nairobi.

Wamitila,K.W.(2003). *Kamusi ya fasihi istilahi na nadharia*.Nairobi:Focus publishers.

Wamitila,K.W.(2007).*Narrative structure and Metaphor:Towards a new aesthetics of the kiswahili novel*.Kiswahili,70,67-75.

Yovo,P.N(2021) *Uchunguzi wa jinsi masuala ibuka yalivyoigizwa katika ngojera za kiswahili katika tamasha za drama za kitaifa nchini Kenya(2010-2017).*Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Keyatta .(Haijachapishwa)

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho A: Idhini

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 501079

Date of Issue: 30/June/2025

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Ms.. PAULINE KAMANTHE MUSYOKI of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Makueni on the topic: TATHMINI YA SURA ZA UFISADI KATIKA RIWAYA ZA TOM OLALI MAFAMBA (2012) NA WATU WA GEHENNA(2012) for the period ending : 30/June/2026.**

License No: NACOSTI/P/25/4175798

501079

Applicant Identification Number

Deputy Director
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**